# Nipashe

Jumatatu Novemba 14, 2022 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0581129

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710

LIKE & FOLLOW US





UKURASA 13








RIPOTI MAALUM

**Maji** ya bahari yanavyovamia visima Zanzibar

UKURASA 4

# Kikokotoo mafao bado kaa la moto

• **Mkutano** wa mashauriano wavunjika, wajumbe wataka waziri... *Endelea ukurasa 2*

## YALIYOMO

UKURASA WA 8

**'TUNDU LISSU ASIENDELEE KUWA MKIMBIZI UBELGIJI'**

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Singida...

UKURASA WA 9

**TAKUKURU YAREJESHA FEDHA ZILIZOFUJWA**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Lindi...

UKURASA WA 25

**CCM YATEUA WAGOMBEA WA NAFASI NYETI**

VIGOGO mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wameteuliwa kugombea...

## Ajali ya basi ilivyoua watu 6, kujeruhi 22

UKURASA 3



Mwendesha bodaboda maeneo ya Tegeta wilayani Kinondoni akipakia maji aliyochota kwa ajili ya kuwauzia watu majumbani kwa gharama ya Sh. 700 hadi Sh. 1,000 kwa dumu kulingana na umbali. **PICHA: ELIZABETH ZAYA**

## Maji yageuka fursa na maumivu wakazi Dar

UKURASA 2








Mkurugenzi wa Manunuzi wa Benki ya CRDB, Pendason Philemon (kulia), akipokea tuzo ya Huduma Bora za Kidijitali katika Sekta ya Benki Afrika Mashariki kutoka kwa Mkurugenzi wa Biashara na Masoko Vodacom, Linda Riwa, katika Tuzo za Consumer Choice Awards zilizofanyika ukumbi wa Diamond Jubilee mwishoni mwa wiki. Benki ya CRDB pia ilitunukiwa tuzo ya Benki Bora katika kipengele cha Huduma kwa Wateja. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Maji yageuka fursa na maumivu wakazi Dar

**Na Waandishi Wetu**

KUFA kufaana! Ni msemo unaoonekana kuakisi kinachojiri Dar es Salaam kutokana na uhaba wa maji ulioukumba mkoa huo.

Wakati shida hiyo ikiwa maumivu kwa wakazi wengi wa Dar es Salaam, kwa baadhi ya watu, wakiwamo madereva pikipiki za kubeba abiria (bodaboda), imegeuka fursa.

Kwa wanaonunua maji kwa ajili ya matumizi ya nyumbani, sasa wanauziwa na bodaboda galoni la lita 20 kwa wastani wa Sh. 1,000 hadi 2,000, Nipashe ikishuhudia utaratibu huo kwenye maeneo ya Bunju A, Bunju B, Tegeta, Mbezi Beach, Mabwepande na Mbweni.

Nipashe imebaini baadhi ya vijana wanaofanya biashara ya bodaboda sasa wamechana na kusafirisha abiria na kuhamia katika kuuza maji, wakitamba biashara hiyo mpya kwao inawalipa zaidi kulinganishwa na kubeba abiria.

"Kubeba maji kwa sasa ndiyo habari ya mjini, inalipa zaidi kuliko kubeba abiria. Na kwa sisi ambao tunapeleka hesabu kwa mabosi wetu kwa sasa hatuumizi kichwa kabisa," alisema Sudi Mavinzo anayefanya biashara hiyo ya maji katika eneo la Bunju B.

Katika mazungumzo na Nipashe jana, Mavinzo alisema ana wiki tatu tangu aanze biashara hiyo ya kuuza maji, akibainisha kuwa kwa sasa anao uhakika kupata si chini ya Sh. 50,000 kwa siku.

"Na sio kwamba unatafuta wateja, hapana! Ni wengi mpaka unawakataa mwenyewe. Kwa hiyo, inanilazimu niamke alfajiri, ili nipambane nao.

"Na wateja wangu ni wa aina mbili, wa kwanza ni hawa wanaotaka ukachote mwenyewe halafu uwauzie, lakini kuna wengine ambao wanatafuta maji yanakotoka au wanachota kwa kwenye visima madumu mengi halafu unawabebea kuwapelekea nyumbani," alisema.

Dereva bodaboda huyo alibainisha kuwa wateja wanaonunua kwa dumu moja, huwauzia kwa Sh. 700 na wale wa kuwapelekea nyumbani baada ya kuchota wenyewe huwatoza kulingana na umbali wa eneo wanakoishi.

"Kwa mfano, kwa mita 200 kwa madumu sita ninawatoza Sh. 3,000, ikiwa mbali zaidi, ni Sh. 6,000 kwa madumu sita," alifafanua.

Eliya Lucas, mkazi wa Mbweni anayejishughulisha na udereva wa bodaboda, alisema wateja wake wengi ni wanaotoa oda ya kupelekewa maji nyumbani.

"Mwingine anaweza kukuagiza umchotee madumu 30 au 20, na kwa siku ninaweza kupata oda ya watu watano, wanane hadi 10.

"Kwa sababu wengi nimewazoea, ninawatoza dumu kwa Sh. 500 mpaka 600, na kule ninakochota mimi ninalipia Sh. 200 kwa dumu. Kwa hiyo, kinachohitajika ni nguvu yangu inapoishia.

"Kuna wakati ninabeba maji mpaka kiuno kinagoma, ukiinama unapata maumivu makali, kwa sasa nikiona oda inanizidia, ninawaomba wenzangu tunasaidiana, wananipa fedha kidogo kwenye kila dumu halafu wanabaki na chao. Kwa siku mapato yangu sasa hayapungui Sh. 40,000 mpaka 60,000," alisema.

Theophil Thomas, dereva bodaboda eneo la Mbezi Beach, alisema kwa sasa amepunguza idadi ya abiria na nguvu yake amewekeza zaidi katika kuuza maji.

"Huu uhaba wa maji kwa kweli kwa namna moja au nyingine kwetu sisi tumefaidika, hatufurahii kwa sababu imekuwa hivi lakini hatuna namna inabidi tuwasaidie na sisi tupatie japo kipato chetu.

"Mimi sijaacha kabisa kubeba abiria, nina wateja wangu wa kudumu ambao siwezi kuwaacha. Kwa hiyo, ninawabeba kama kawaida," alisema Theophil na kubainisha kuwa dumu moja la maji ananunua kwa Sh. 200 hadi 250 na kuyauza kwa Sh. 700 na kipato chake kwa siku kinaanzia Sh. 30,000 hadi 40,000.

**MAUMIVU**

Baadhi ya wananchi waliozungumza na Nipashe mkoani hapo mwishoni mwa wiki, walisema pamoja kutangaziwa kwamba watakuwa wanapata maji kwa mgawo, wengi hawafikiwi na mgawo huo.

"Mimi ninaishi hapa Bunju A, nina mwezi sasa huo mgawo wa maji sijawahi kuupata, nina familia kubwa, ninalazimika kutumia fedha nyingi kila siku kununua maji kwa hawa bodaboda wanaouza kwenye madumu," alisema mkazi huyo aliyejitambulisha kwa jina la Mama Junior.

Mkazi mwingine wa mkoa huo aliyejitambulisha kwa jina moja la Hanifa, alisema anaishi Mbweni Mpiji na hajapata maji ya mgawo tangu ulipotangazwa.

"Nilichobakiza ni kuomba neema ya Mungu tu ashushe mvua, la sivyo sijui itakuwaje. Nina familia ambayo inanilazimu nitumie si chini ya Sh. 15,000 kila siku, maana vyoo vyangu ni vya kutumia maji zaidi na nisipofanya hivyo tutapata maradhi," alisema Hanifa.

Joseph Birundula, mkazi wa Tabata jijini Dar es Salaam, alidai wana wiki mbili pasi na kupata maji ya bomba, hivyo wamehamia katika matumizi ya maji ya visima ambayo anaona si salama kiafya, akiomba mamlaka kupima maji hayo ili wananchi wasiathirike.

"Sio mimi tu niliyeshtukia hili suala, kuna baadhi ya maeneo wanakouza chakula wanalalamikiwa kwamba wanalisha watu chakula kilichopikwa kwa maji ya chumvi, pia juzi pale ninapofanyia kazi kuna mtu alimuuzia kijana uji wa mchele alipounywa alikuta una chumvi nyingi ilibidi aumwage," alidai Birundula.

Zainabu Rashidi, mkazi wa Tabata, aliomba watumishi wa Mamlaka ya Maji (DAWASA) wanaoratibu utaratibu wa mgawo wa maji, kuhakikisha wanasimamia suala hilo kwa weledi bila upendeleo kwa kuwa mitaa yao yaijaona maji ya mamlaka hiyo kwa wiki mbili sasa.

Issa Mduma, dereva bodaboda anayeuza maji, alisema anatumia muda mwingi kuuza maji kuliko kubeba abiria kwa kuwa anapata fedha nyingi.

"Biashara ya maji imekuwa ikiniingizia fedha zaidi kwa kipindi hiki, muda wote unakuwa unauza maji tofauti na kubeba abiria ambao tulikuwa tunawasubiria kituoni kwa muda, japokuwa wamiliki wa pikipiki wanakuwa hawataki tubebe maji lakini tunapita katika mitaa ambayo sio rahisi kutuona," alisema Mduma.

Hivi karibuni viongozi walibainisha njia mbalimbali za kukabiliana na upungufu wa maji katika Mkoa wa Dar es Salaam ikiwamo kufufua visima.

Kwa mujibu wa Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, Dar es Salaam sasa inakabiliwa na upungufu wa maji lita milioni 120 kutokana na uzalishaji wa sasa kuwa lita milioni 400 kwa siku.

# Kikokotoo cha mafao wastaafu kaa la moto

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MKUTANO wa Chama cha Walimu Tanzania (CWT) uliokuwa umeandaliwa kwa ajili ya kuwapa elimu ya kikokotoo iliyokuwa itolewe na maofisa wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumishi wa Umma (PSSSF), haujafanyika baada ya wajumbe kuwagomea, wakimtaka waziri mwenye dhamana ya mifuko ya hifadhi ya jamii.

Sintofahamu hiyo iliibuka mwishoni mwa wiki iliyopita jijini Dodoma na kusababisha mkutano kuvunjika kutokana na kile wajumbe walichodai wanataka mjadala urudi upya mezani katika sheria ya Bunge, ili kurudisha asilimia 50 badala ya asilimia 33 ya kikokotoo kipya.

Vilevile, baadhi ya wajumbe ndani ya kikao hicho, waliwashutumu viongozi wao kuwa wanashindwa kuendesha mikutano yao kutokana na mgawanyiko uliopo ndani yao.

Mmoja wa waliibua hoja ya kukataa kuzungumza na maofisa hao, Mwenyekiti wa CWT Mkoa wa Kagera, Costa Rwamugila, alisema waliwataka maofisa hao waondoke kwa kuwa walijua hawana majibu ya moja kwa moja kwa wanachokitaka.

"Wale waliokuja ni waathirika wenzetu, kwa hiyo tuliwakataa siyo kwa nia mbaya lakini tulilenga kumpata kiongozi wa juu aje kama waziri kutoa ufafanuzi, lakini sisi bado ni wamoja ndani ya chama chetu," alisema Rwamugila.

Alipotafutwa kuzungumzia suala hilo, Kaimu Rais wa CWT, Dinnah Mathamani, kujua, alikiri kutokea kwa mvutano huo wakati wa mkutano kati yao na maofisa PSSSF ulioitishwa kwa lengo la kutoa elimu hiyo lakini wajumbe wakapinga kuzungumza nao.

"Katika kikao na Rais Samia Suluhu Hassan tulikubaliana viongozi wa vyama kuendelea kutoa elimu juu ya asilimia 33 ya sera ya kikokotoo iliyofikiwa ili wanachama wapate uelewa.

"Lakini kwenye mkutano huu baada ya kufungua mkutano, nilitaja ajenda lakini niliwaambia kubwa ni kuhusu sera ya kikokotoo kabla ya kuhoji au kuuliza inabidi tupate elimu kwanza ndipo tuendelee na mkutano. Hapo ndipo watu walianza kuguna na kutokea kutoelewana na mkutano haukuendelea," alisema.

Mathamani alibainisha kuwa waliamua kuahirisha mkutano huku wajumbe wakimshinikiza atoe tamko kwenye vyombo vya habari kushinikiza asilimia 50 badala ya 33 ambayo imefikiwa kwa makubaliano ya serikali na vyama vya wafanyakazi.

"Nilikataa kutoa tamko ambalo walikuwa wanataka kwa sababu kanuni haziniruhusu kufanya hivyo, ndipo wakataka tumtafute waziri ambaye niliongea naye kwa simu akasema yuko Dar es Salaam, hivyo mkutano uahirishwe. Kwa kifupi, hakukuwa na maelewano," alisema Mathamani.

Hata hivyo, alisema kutokana na hali hiyo wametuma maombi ya kukutana na viongozi wa juu akiwamo Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako ili kufikisha kilio na tamko lao kuhusu nini wanawaza.

Nipashe ilimtafuta, Ofisa Uhusiano Mkuu wa PSSSF, Abdul Njaidi, kuzungumzia suala hilo, akidai kutokuwa na taarifa kuhusu mkutano huo na kuahidi kufuatilia ili kutolea ufafanuzi kinachodaiwa kujiri.

Sakata la kikokotoo cha mafao ya wastaafu liliibuliwa na gazeti hili mwaka 2018 baada ya kuandika kwa kina kuhusu kanuni ya sheria iliyoanzisha mfuko wa PSSSF baada ya kuunganisha mifuko ya PPF, PSPF, LAPF na GEPF, uamuzi ambao pia uliwezesha nchi kuwa na mifuko miwili ya PSSSF na NSSF.

Kutokana na habari zilizoandikwa mfululizo, aliyekuwa Rais kipindi hicho, Hayati Dk. John Magufuli, aliagiza kusitishwa kutumika kwa kanuni za sheria hiyo hadi mwaka 2023, lakini kabla ya kufikia wakati huo serikali kwa kushirikiana na wawakilishi wa wafanyakazi walifikia uamuzi wa kuwa na kikokotoo kimoja cha asilimia 33.

Kikokotoo kilichokuwa kimependekezwa awali kwenye kanuni za sheria mpya ya NSSF ambao ni mfuko wa sekta binafsi, ni kuwa mkupuo wa asilimia 25 na mifuko mingine ya watumishi wa umma asilimia 50, sasa watumishi wote wanapostaafu wanapata mkupuo unaofanana wa asilimia 33.

## HABARI KITAIFA



Mwenyekiti wa Shirika lisilo la Kiserikali la Eden Twins Foundation, linalohudumia wazazi wenye watoto mapacha wasio na uwezo kiuchumi, Diana Mbena (mbele kulia), akitoa msaada kwa Monica Marko mzazi wa mapacha asiyeona, nyumbani kwake Saku Chamazi, Dar es Salaam jana. **PICHA: SABATO KASIKA**

# Ajali ilivyoua sita kujeruhi 22

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WATU sita wamefariki dunia papo hapo na wengine 22 wamejeruhiwa kutokana na basi la Arusha Express kugongana uso kwa uso na lori la mchanga la kampuni ya Sinohydro.

Ajali hiyo ilitokea jana jijini hapa kwenye eneo la Mzakwe, Kata ya Makutupora baada ya basi lenye namba T 530 AGG lililokuwa likitokea Arusha kuelekea Mbeya kugongana uso kwa uso na lori lenye namba T 939 DZE.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Dodoma, Martin Otieno, alithibitisha kutokea kwa ajali hiyo huku akieleza chanzo chake hakijajulikana.

Alisema kwenye ajali hiyo watu sita wamepoteza maisha papo hapo na majeruhi wamekimbizwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Rosemary Senyamule, alisema miili ya watu wanne imetambuliwa na wawili hawajatambuliwa, mmoja akisadikiwa kuwa dereva wa lori na abiria wa basi hilo.

"Wapo majeruhi 22 ambapo wanawake ni 10 na wanaume ni 12, wengine wapo Hospitali ya Rufani na mmoja amepelekwa Hospitali ya Benjamin Mkapa. Nitoe wito kwa madereva eneo lililotokea ajali hakukuwa na mwinuko wowote, kilichotokea ni dereva wa lori alikuwa anataka kupita eneo lisilo sahihi na kusababisha ajali hii mbaya," alifafanua.

Aliwaomba wananchi kujitolea damu kuwasaidia majeruhi wa ajali hiyo.

Naye, Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani Dodoma, Dk. Ibenzi Ernest, alisema majira ya saa saba mchana jana walipokea majeruhi 21 na miili ya marehemu waliofariki kwenye ajali hiyo.

"Hali zao zinaendelea vizuri na miili imehifadhiwa kwenye chumba cha kuhifadhia maiti katika hospitali hii, tunaomba madereva wanapoendesha vyombo vya moto wajiepushe na vitu vinavyosababisha ajali kwa kuwa matibabu yake huwa ni gharama kubwa," alisema.

Alitaja marehemu waliotambuliwa kuwa ni Kurwa Awadh, ambaye ni dereva wa basi hilo, Amani Athumani, Yohana Paulo na Humphrey Mdoe wanaosadikiwa kuwa ni mawakala wa basi hilo.

Mmoja wa majeruhi, Salma Juma, alisema alishtukia lori lipo mbele yao na waliojeruhiwa zaidi waliokuwa wamekaa siti za mbele.

Alisema basi la abiria la kampuni ya Machame liliwapa msaada wa kubeba majeruhi na kuwawahisha hospitali.

# Othman aziona fursa uwekezaji sekta utalii

**Na Mwandishi Wetu**

MAKAMU wa Kwanza wa Rais wa Zanzibar, Othman Masoud Othman, amesema Tanzania inaweza kuwa kiongozi kwa kunufaika na pato la uwekezaji litokanalo na sekta ya utalii iwapo nchi itajipanga kuvitumia vyema vivutio vilivyoko maeneo tofauti ya Tanzania Bara na Visiwani.

Othman alisema hayo alipokuwa mkoani Iringa kumwakilisha Rais wa Zanzibar, Dk. Husein Mwinyi, kufungua kongamano la uwekezaji katika sekta ya utalii lililoandaliwa kwa pamoja na mikoa 10 ya Nyanda za Juu Kusini ikiwa ni sehemu ya maonyesho ya utalii ya 'Karibu Kusini 2022 kuutangaza utalii Tanzania'.

Alisema Tanzania ina vivutio vingi vya maumbile na vya kiutamaduni ambavyo vinahitaji kutangazwa vyema ili kuwavuta wawekezaji wa aina mbalimbali na hatimaye nchi iweze kunufaika zaidi na mapato yatokanayo na biashara ya utalii.

Alisema kuwapo kwa kongamano hilo lililowashirikisha wawekezaji wa sekta hiyo kutoka ndani na nje ya Tanzania ni muhimu kutokana na kusaidia kubadilishana uzoefu na kuchangia mawazo bora ya uwekezaji katika maeneo yanayohitajika Tanzania Bara na Visiwani.

Alitahadharisha, licha ya taifa kuhitaji uwekezaji wenye tija kwenye sekta hiyo, ni vyema kuwa makini kuhakikisha mazingira ya nchi hayaharibiwi na yanatunzwa vyema ili vivutio vya asilia na vya kiutamaduni vilivyoko visiharibiwe.

Aliwataka Watanzania hasa viongozi wanaosimamia sekta hiyo kutoogopa ushindani na kwamba jambo muhimu ni kujitahidi kuutangaza vyema utalii wa Tanzania Bara na Zanzibar na kwa kutumia uzoefu wa sehemu mbalimbali nchi inaweza kupiga hatua kubwa katika kuwa na tija bora itokanayo na utalii.

Alisema sekta za benki inaweza kutumika kuingia ubia wa uwekezaji au mitaji ya kuendesha biashara hiyo kwa kuwa zipo nchi nyingi zimenufaikia na utaratibu huo.

Naye Waziri wa Utalii na Maliasili wa Jamhuri ya Muungano, Balozi Pindi Chana, alisema Tanzania inatekeleza kwa vitendo maono ya Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Samia Suluhu Hassan katika kuutangaza vyema utalii duniani.

Alisema imeweka malengo na mikakati kadhaa na ndiyo maana kupitia filam ya Royal Tour iliyoandaliwa na Rais Samia imeanza kuonesha mafanikio makubwa na tayari watalii wengi wanaendelea kuingia nchini.

# Wataka fidia nyumba 11 zilizobomolewa na tembo

**Na Thobias Mwanakatwe,** IKUNGI

DIWANI wa Iglason ameitaka Wizara ya Maliasili na Utalii kuharakisha kuwalipa fidia wananchi ambao nyumba zao 11 zilibomolewa na tembo waliovamia Kitongoji cha Ikomba, Kata ya Iglason wilayani Ikungi mkoani Singida.

Yusuph Athuman, akizungumza na Nipashe baada ya kikao cha Baraza la Madiwani wa Halmashauri ya Wilaya ya Ikungi mwishoni mwa wiki, alisema wananchi waliothirika wanahangaika kwa kuwa hawana sehemu za kuishi.

Athuman akielezea tukio hilo, alisema kuwa Septemba mwaka huu, kundi la tembo lilivamia Kijiji cha Ikomba na kuvunja nyumba 11 na kuharibu mazao yaliyokuwa yamehifadhiwa kwenye maghala.

Alisema tembo hao ambao wanatoka katika pori la Itigi walikivamia kitongoji hicho kuanzia saa 12 jioni hadi asubuhi siku iliyofuata ambapo wananchi walipiga yowe lakini hawakuondoka hadi walipomaliza kuzibomoa nyumba hizo na kula mazao.

Diwani huyo alisema kufuatia tukio hilo, wataalamu kutoka Idara ya Maliasili walifika katika kitongoji hicho na kuweka kambi na kufanikiwa kuwaondoa tembo hao na kuwarudisha katika Pori la Itigi.

Alisema baadaye wananchi walioathirika walichukuliwa majina yao kwa ajili ya kuandaliwa kulipwa fidia lakini hadi sasa imepita miezi miwili hawajalipwa.

Athuman aliwaomba wananchi wanapowaona tembo katika makazi yao kutoa taarifa haraka katika Idara ya Maliasili ili taratibu za kuwaondoa zifanyike haraka kabla hawajafanya uharibifu.

Mara kadhaa wananchi wa wilaya za Ikungi na Manyoni katika Mkoa wa Singida wamekuwa wakivamiwa na tembo katika makazi yao, wakiharibu mazao, kuua na kujeruhi watu.


**KUPOTEA KWA PASSPORT**



**JULIANA PATRICK LEWANGI** anatangaza kupotea kwa hati yake ya kusafiria (Passport) yenye namba TAE 358106 iliyotolewa na Idara ya Uhamiaji Dar es salaam tarehe 08/9/2020. Muda wake wa kuisha matumizi ni tarehe 07/9/2030. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha Polisi kilicho karibu naye. Taarifa ya Polisi: **DAR/CHA/RB/436957/2022.**

**KUPOTEA KWA KADI YA BAJAJI**

**DANIEL MATHIAS KALINGA** anatangaza kupotea kwa kadi ya bajaji aina ya **TVS KING** yenye usajili namba **MC 563 AZM,** CHASSIS NAMBA: **MD6M14PK2F4K13586** na ENGINE NAMBA: **0K4KF4283200.** Kwa yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha polisi. POLISI TAARIFA: **MKO/TR/RB/191/2022**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA UJENZI, NA UCHUKUZI**

Simu: +255 26 2324455
Fax: +255 26 2323233
Barua Pepe:@mow.go.tz
Tovuti: www.mwtc.go.tz

Mtaa wa Mtumba,
S.L.P. 2888,
DODOMA,
14.11.2022

**TAARIFA KWA UMMA**

1. Wizara ya Ujenzi na Uchukuzi (Sekta Ujenzi) inapenda kuutaarifu umma kuwa siku ya Jumanne tarehe **15-11-2022** kampuni ya **Mainline Carriers Ltd** itasafirisha Mizigo yenye vipimo vikubwa kutoka **Dar-Es-Salaam Port kuelekea Rufiji,** gari hizo zina namba za usajili: **T 624 DFA / T 137 CHN T 111 EAG / T 269 DUH T 204 DYG / T 499 DXZ T 859 DXS / T 139 CHN T 649 BZU / T 146 CHN**

2. Gari hizo zina vipimo vifuatavyo:
   **Urefu - mita 24.00**
   **Upana - mita 4.35**
   **Kimo - mita 5.20**

3. Njia itakayotumika: **Dar-Es-Salaam, Pwani hadi Rufiji** kupitia Kibiti, gari zitasafiri muda wa mchana tu ***(Kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12:00 Jioni)***

***Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.***

217146302

# Maji ya bahari yanavyovamia visima vya wananchi Zanzibar

## ●Kiini cha tatizo: Wakazi kukata mikoko

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR



Wanakikundi cha Uhifadhi wa Mikoko Kijiji cha Kibele, Mkoa wa Kusini Unguja wakiwa katika hifadhi yao yenye mikoko wiki iliyopita. **PICHA ZOTE : RAHMA SULEIMAN**

"KAMA tusingechukua hatua hizi, hali ingekuwa mbaya zaidi. Tulifikia hatua mbaya, maji ya bahari kuyavamia maeneo ya makazi," Issa Mussa (80), mkazi wa Kijiji cha Kisakasaka, Mkoa wa Mjini Magharibi Unguja anasimulia kinachowasibu.

Mussa ambaye wajihi wake unaonesha amekula chumvi nyingi, anabainisha namna mabadiliko ya tabianchi na uharibifu wa mazingira uliofanywa na jamii, ulivyoathiri maisha yao kijijini huko.

"Kinachotokea hapa wa kulaumiwa ni sisi wakazi wa hapa. Wanakijiji wategemea mikoko kwa ajili ya kujipatia kipato kwa biashara ya kuni na mkaa.

"Athari hizi zilianza kujitokeza mwaka 2000 baada ya idadi ya wanakijiji kuongezeka huku harakati za biashara ya kuni na mkaa zikishamiri.

"Wakati wa ujana wangu tulikata mikoko lakini idadi ya wakazi wa Kisakasaka haikuwa kubwa kama iliyoko sasa na ndiyo maana athari kwa wakati huo hazikujitokeza kwa sababu kulikuwa na mikoko ya kutosha," anasema.

Kijiji hicho ni miongoni mwa maeneo yaliyokumbwa na athari mabadiliko ya tabinchi kutokana na uharibifu wa mazingira uliofanywa na wakazi wake, kiini cha tatizo kikiwa ni ukataji wa miti hasa mikoko ambayo husaidia kuzuia mmong'onyoko wa fukwe.

Kwa mujibu wa Idara ya Misitu Zanzibar, asilimia 65 ya wananchi wa visiwa hivyo vilivyozungukwa na bahari wanatumia nishati ya kuni na mkaa, hali inayoathiri mazingira.

Idara hiyo inabainisha kuwa hekta 1,000 za msitu huharibiwa kila mwaka kutokana na kuongezeka shughuli za kijamii ikiwamo ujenzi, uchomaji mkaa na matumizi ya kuni.

Ni dosari inayotajwa kusababisha athari mbalimbali za kimazingira ikiwamo maji ya bahari kuvamia makazi ya watu, huku visima vya maji na maeneo ya kilimo vikiathiriwa zaidi.

Katibu wa Jumuiya ya Uhifadhi Mikoko kijijini huko (JUMUKISI), Khatib Ali Vuai (34), anasema baada ya kubaini athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kijiji chao, wameamua kupanda na kuhifadhi mikoko ambayo imesaidia kuzuia mmong'onyoko wa ardhi.

Anazitaja athari zilizojitokeza kutokana na mabadiliko ya tabianchi zinajumuisha maji ya bahari kuvamia visima vya majisafi, uhaba wa samaki na nyumba kuezuliwa na upepo.

Anasema baada ya athari hizo kutokea, walijikusanya na kuazisha jumuiya hiyo ambayo wanachama wake ni vijana. Kati yao, wanaume ni 10 na wanawake wanane.

Katibu huyo anasema eneo walilopanda mikoko lina ukubwa wa hekta 70 ambazo kwa sasa mafanikio yameanza kupatikana ikiwamo kuzuia maji ya bahari kupanda katika makazi ya watu na athari zilizosababishwa na upepo zimepungua.

"Katika miaka ya 1990, hali ya kimazingira ilikuwa mbaya kwa sababu maji yetu hapa tunayotumia ni ya visima, hivyo yalibadilika ladha na kuwa ya chumvi kutokana na maji ya bahari kuvamia maeneo ya wakazi, lakini kwa sasa maji yamerejea katika hali ya kawaida," anapongeza jitihada zao.

Vuai anarejea historia ya kijiji chao kwamba miaka 40 iliyopita kilikuwa na mikoko mikubwa lakini hali ilibadilika katika miaka ya 2000 kutokana na miti mingi kukatwa.

"Licha ya mafanikio tuliyayopata katika kukabiliana na shida hii, bado kuna vikwazo kadhaa, hasa uharibifu wa mikoko ingawa kiwango si cha kutisha kulinganishwa na awali," anasema.

Sabiha Abdallah (33), Mwenyekiti Msaidizi wa jumuiya hiyo, anasema wanawake hawako nyuma katika kupanda na kuhifadhi mikoko kwa kuwa athari za kimazingira hazichagui jinsia.

"Athari za kimazingira zilizojitokeza kijijini kwetu, wanawake ndiyo walioathirika zaidi kwa sababu maji tuliokuwa tunatumia yalikuwa ya chumvi, hivyo tulilazimika kutembea masafa marefu kutafuta maji ya kunywa.

"Kutokana na shida hizo tulizopitia, sasa tumekuwa wadau wazuri wa kulinda na kuhifadhi mikoko, faida imeanza kupatikana ikiwamo ufugaji nyuki," anasema.

Mjumbe wa Shehia ya Kombeni, Kijiji cha Kisakasaka, Pili Issa (40), anasema uhifadhi wa mazingira kwa sasa umeimarika na kuwapongeza vijana wa jumuiya hiyo kwa kukinusuru kijiji hicho ambacho kilikaribia kuzama. Athari hizo za kimazingira katika kijiji hicho hazitofautiani na hali iliyoko Kijiji cha Kibele, Mkoa wa Kusini Unguja ambacho baada ya mikoko kukatwa, maji ya bahari yamevamia maeneo ya kilimo.

Katibu wa Kikundi cha Uhifadhi wa Mikoko cha Uvivu si Mtaji, Kheri Ali Salum (35), anasema hali hiyo ilisababisha maji ya bahari kuvamia shamba la migomba na kushindwa kupata mavuno baada ya migomba hiyo kuharibika.

Anasema mikoko katika kijiji hicho ilikatwa kwa kiwango kikubwa, akifafanua mikakati yao kwa kauli: "Ili uvuvi ukue ni lazima kuhifadhi mazingira ya bahari ikiwamo uhifadhi wa mikoko ambayo ni mazalia ya samaki na viumbe wengine wa baharini ikiwamo kaa."

Mwajuma Nassir (38), mjumbe wa kikundi hicho, anasema wanafanya doria katika hifadhi hiyo ingawa hawana zana za kukabiliana na wahalifu.

"Wakati mwingine unawakuta wahalifu wanakata mikoko lakini wanatuzidi nguvu maana hatuna zana zozote za kukabiliana nao," analalamika.

Awesu Shabani Ramadhani, Naibu Katibu wa Hifadhi ya Mazingira Msitu wa Hifadhi Jozani, Mkoa wa Kusini Unguja (JECA), anasema hali ya utunzaji wa mazingira si ya kuridhisha licha ya juhudi wanazochukua ikiwamo kuhamasisha jamii kutumia majiko sanifu yanayotumia kuni au mkaa kidogo.

Kiongozi huyo anakiri wakazi wengi wa vijijini bado wanatumia kuni na mkaa kuliko nishati mbadala kama gesi kutokana na hali duni kiuchumi.

Anasema jamii inaharibu mazingira kwa kukata miti kwa kisingizio cha hali ngumu ya maisha kwa lengo la kupata fedha kutokana na biashara ya kuni na mkaa. "Sasa hivi tunahamasisha shughuli za uzalishaji mali ambazo haziharibu misitu ikiwamo ufugaji wa nyuki, kaa, samaki na mazao mengine ya baharini," anataja mikakati yao kukabiliana na uharibifu wa mazingira.

Ofisa wa Mikoko kutoka Idara ya Misitu Zanzibar, Daud Dugoha Songwa, anaeleza kuwa uharibifu mikoko ni mkubwa kwa kuwa zaidi ya asilimia 80 ya miti hiyo imekatwa.

Anarejea Sensa ya Mikoko ya Mwaka 2014, iliyobainisha kuwa Zanzibar ina hekta 16,488 za mikoko. Kati yake, hekta 11,214 ziko Pemba na hekta 5274 ziko Unguja.

Anayataja maeneo yaliyokithiri kwa ukataji mikoko ni Chwaka, Ukongoroni, Charawe, Michamvi na Bwejuu.

Rahika Hamad Suleiman, Ofisa Kitengo cha Elimu ya Misitu kwa Wanajamii katika Idara ya Misitu Zanzibar, anasema miti ya asili ambayo imekuwa ikitegemewa kwa shughuli mbalimbali ikiwamo kutibu maradhi, imeanza kutoweka, akiitolea mifano mikoko na minyusi ambayo inasaidia kutibu pumu na maumivu ya tumbo.

Anasema Idara ya Misitu inatoa elimu kwa jamii kuhusiana na usimamizi wa rasilimali ya misitu, akisisitiza nishati ya gesi ni salama na muhimu katika kuhifadhi mazingira, hivyo wananchi waitumie na kuachana na matumizi ya kuni na mkaa.

Mkurugenzi wa Mamlaka ya Udhibiti Mazingira Zanzibar (ZEMA), Sheha Juma Mjaja, anasema wana mikakati ya kukabiliana na mabadiliko ya tabinachi na athari za kimazingira ikiwamo kupanda na kuhifadhi mikoko na kujenga matuta ya kuzuia maji ya bahari kuvamia maeneo ya kilimo na makazi ya watu.

"Mamlaka pia tunaijengea uwezo jamii kwa sababu ndiyo wanaoishi katika maeneo hayo, hivyo lazima wawe walinzi wa mikoko na rasilimali zingine.

"Mabadiliko yamesababishwa na kuongezeka kwa shughuli za kibinadamu ikiwamo matumizi ya nishati ya kuni na mkaa na sababu za kimaumbile kama ukataji mikoko, uchafunzi wa mazingira, kuongezeka kwa joto na kupanda kina cha maji ya bahari," anasema.

Mjaja anabainisha kuwa maeneo 148 yameathirika kutokana na maji ya bahari kuvamia makazi ya asili ya watu. Kati yake, maeneo 23 yako Unguja na 125 yako Pemba.

Sheria Na. 10 ya Misitu ya Mwaka 1996, inaelekeza ni kosa kukata mti au kufanya shughuli yoyote kwenye msitu bila kibali maalum kutoka Idara ya Misitu.



Mwajuma Nassir, mwanakikundi cha uhifadhi wa mikoko Kibele, Mkoa wa Kusini Unguja akionyesha maji ya bahari katika hifadhi hiyo ambayo awali yalivamia maeneo ya kilimo.

## TANGAZO






**Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Hamad Hassan Chande, afungua Wiki ya Shukrani kwa Mlipakodi kwa kuongoza watumishi wa TRA katika mbio za umbali wa Km 10 na matembezi ya Km 5 yaliyofanyika Viwanja vya Gymkhana jijini Dar es Salaam.**



Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Uwekezaji zaidi unahitajika Simba Queens kutisha CAF

**MSIMU** wa Ligi ya Mabingwa Afrika 2022/23 kwa Wanawake ulifikia tamati mwishoni mwa wiki baada ya fainali iliyowakutanisha mabingwa watetezi, Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini dhidi ya wenyeji wa michuano hiyo, ASFAR FC ya Morocco, kupigwa jana.

Katika michuano hiyo iliyokuwa ikifanyika Morocco, ilijumuisha mabingwa wa Kanda Nane za Afrika, ambapo kwa Afrika Mashariki na Kati, iliwakilishwa vema na Simba Queens iliyomaliza nafasi ya nne baada ya kukubali kipigo cha bao 1-0 dhidi ya Bayelsa Queens FC ya Nigeria katika mechi ya kuwania mshindi wa tatu juzi usiku.

Kwa ujumla ilikuwa ni michuano migumu na ya ushindani mkubwa kwani timu zilizoshiriki mbali na kwamba ni mabingwa wa nchi zao, lakini pia ndizo mabingwa wa kanda zao.

Kwa upande wa Simba Queens ambayo ilikuwa Kundi A lililokuwa likiundwa na Green Buffaloes ya Zambia, Determine Girls ya Liberia na wenyeji ASFAR FC, hadi inashika nafasi ya nne ilishinda jumla ya mechi mbili na kupoteza tatu kwa mbinde.

Simba Queens ilianza kwa kupoteza kwa bao 1-0 katika mechi ya ufunguzi dhidi ya ASFAR FC kisha ikashinda 2-0 dhidi ya Determine Girls kabla ya kuichapa Green Buffaloes 2-0 na kutinga nusu fainali.

Nusu fainali Simba Queens ilikutana na bingwa mtetezi, Mamelodi Sundowns Ladies na kutolewa kwa tabu baada ya kufungwa bao 1-0, hivyo kuangukia kuwania nafasi ya tatu ambapo ilipokea kipigo kingine kama hicho kutoka kwa Bayelsa Queens FC .

Hata hivyo, kwa namna Simba Queens ilivyoonyesha uwezo mkubwa katika michuano hiyo, tunaamini kama uongozi wa klabu hiyo utafanya uwekezaji mkubwa inaweza kuutwaa ubingwa huo msimu ujao.

Katika hili, tunashawishika kusema kwamba umefika wakati kwa klabu zetu kuweka nguvu kubwa na kutoa kipaumbele kwa timu za wanawake kama ilivyo kwa zile za wanaume kwani hilo likifanyika Tanzania inaweza kuanza kuimbwa kwa ubora wa soka la wanawake ndani ya kipindi kifupi.

Ni wazi kwa kipindi hiki ambacho soka la wanawake linashika kasi kwa haraka barani Afrika, Tanzania inapaswa kukimbia kwani kuna vipaji vingi na kilichobaki ni kuhamasisha mchezo huo na kuwekeza zaidi ili kupata mafanikio mapema.

Hilo tumeliona pia kwa uwezo ulionyeshwa kwenye kikosi cha Timu ya Taifa ya Wanawake chini ya miaka 17, Serengeti Girls, ilipofanya maajabu kwenye Kombe la Dunia mwaka huu kwa kutinga robo fainali huku ikizifunga timu ngumu za Canada na Ufaransa.

Hilo linatufanya tuamini pia kwa uwezo ulioonyeshwa na kikosi cha Simba Queens kwenye michuano ya CAF, kinahitaji maboresho kidogo tu ili kwenda kufanya makubwa msimu ujao wa mashindano hayo, hivyo ni wakati sasa kwa klabu hiyo kuanza kuijenga kwa ajili ya msimu ujao.

Lakini wadau wa soka hawana budi kujitokeza kwa wingi kuwekeza kwenye Ligi Kuu ya Wanawake nchini kwa kutoa udhamini hadi kwenye klabu shiriki ili kuongeza ushindani zaidi jambo ambalo litasaidia kupata mwakilishi bora wa Tanzania kimataifa katika mashindano yajayo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com






## Muungwana Lazima Nilonge

# Mechi za usiku zinapunguza mashabiki wengi viwanjani

Na Adam Fungamwango

**NI** ukweli usiopingika kuwa idadi ya mashabiki kwenye viwanja vya soka inazidi kupungua siku hadi siku. Mashabiki kwa sasa wamekuwa wakijazana hotelini, baa, majumba mengine ya starehe, majumbani mwao na hata kwenye vibanda vya kuonyesha michezo maarufu 'vibanda umiza' ili kufuatilia mechi hizo.

Kutokana na hali hiyo, Bodi Ligi Tanzania Bara, imesema ipo katika mchakato wa kupata mshauri wa kufanya tathmini kugungua kwa nini idadi ya watu wanaohudhuria mechi uwanjani inashuka, hivyo kusababisha mapato ya mlangoni kupungua katika michezo ya Ligi Kuu Tanzania Bara.

Mtendaji Mkuu wa TPLB, Almasi Kasongo, anasema idadi ya mashabiki uwanjani imepungua na bodi ipo katika kufanya tathmini na kutafuta ufumbuzi wa sababu ya watu kutoingia uwanjani kama ilivyo miaka ya nyuma.

Alisema wapo kwenye kipindi cha mpito, hivyo watakiwa kutafakari na kuangalia jinsi ya kupunguza viingilio.

Hata hivyo, wakati bodi inaendelea kutafuta mshauri, ngoja mimi nianze kuwapa ushauri ambao unaweza baadaye ukawasaidia kujua ni kwa nini mashabiki wengi kwa sasa wamepungua kwenda viwanjani.

Kwanza kabisa naweza kusema pamoja na kwamba Kasongo amelichukulia kwa ujumla, lakini suala hili linawahusu zaidi mashabiki wa Dar es Salaam.

Mashabiki wa mikoani tunaona huwa wanajazana viwanjani na hasa zinapokwenda klabu kubwa mbili maarufu na kongwe nchini Simba na Yanga. Mechi zingine zikichezwa hata huko mikoani kama vile Kagera Sugar dhidi ya Ihefu huwezi kuona idadi kubwa ya mashabiki.

Hata hapa kinachozungumzwa, mashabiki wanaotajwa kuwa wamepungua viwanjani si wa Singida Big Stars, wala Coastal Union, ni wa Simba na Yanga tu. Huu ndiyo utamaduni wa soka la Tanzania tangu enzi na enzi.

Tuje sasa kwenye muktadha wa kwa nini mashabiki wengi hawaendi viwanjani. Nawatetea wa mikoani, wao huwa wanaenda zinapokwenda timu pendwa. Nawaongelea wa Dar es Salaam ambao kwa sasa hata timu zao Simba na Yanga zikicheza hawajazani kama zamani. Na Bodi imeshindwa kuweka bayana hili.

Sababu zipo nyingi sana kama vile mazingira magumu ya kupata tiketi, usumbufu milangoni na kuchukuliwa kama mhalifu na si mteja, mazingira ya vyoo, pamoja na shabiki kutokuwa na kitu kipya kigeni kinachoweza kumvutia kuwa uwanjani zaidi na zile dakika 90 tu, lakini kwa sasa kuna kitu kingine kinaitwa muda wa mechi.

Kwa sasa asilimia 90 au zaidi mechi zote za Ligi Kuu au Kombe la FA za Simba na Yanga zinazochezwa Uwanja wa Benjamin Mkapa muda wake ni saa 1:00 usiku. Hii ni moja ya sababu kubwa kupungua kwa mashabiki viwanjani.

Zamani mashabiki walioku-wa wakija viwanjani walikuwa wanatoka Temeke, Tandika, Magomeni, Mwananyamala, Kigogo, Mburahati, Ilala na sehemu zilizo ndani ya Jiji la Dar es Salaam, hivyo walikuwa wanajazana viwanjani.

Kwa sasa jiji limekuwa kubwa, kuna wakazi wa Goba, Mbezi Louis, Mbezi Beach, Bunju, Boko, Kisemvule, Chanika na sehemu nyingine nyingi zilizo nje ya jiji.

Kuna mashabiki wengine wanatoka Bagamoyo mkoani Pwani hadi Chalinze kuangalia mechi. Hawa ukiwawekea mechi ya saa moja usiku tatizo lao inakuwa ni usafiri wakati wa kurejea makwao. Kutoka Benjamin Mkapa usiku wa saa tatu, hadi kufika kwao ni usiku wa manane kutokana na umbali pamoja na shida ya usafiri. Atapanda daladala ambayo bei imeongezwa mara mbili ya kawaida, akishuka anapokwenda anaweza kupanda tena daladala nyingine ya kuingia kwenye viunga vya ndani. Halafu pia atashuka na kupanda bodaboda ili kumfikisha nyumbani kabisa. Gharama za usafiri usiku mara nyingi inakuwa kubwa. Halafu muda atakaolala kesho yake anatakiwa aamke alfajiri kwenda kibaruani. Shabiki huyo ni lazima aamue kubaki mitaa yake ya nyumbani na kuangalia kwenye kibanda umiza.

Cha kushangaza wakati Bodi kwa sasa inaonekana kupenda sana mechi za usiku, Ulaya hasa kwenye Ligi za England wameonekana kupunguza sana mechi za usiku mnene. Hispania nao wamefanikiwa sana, kwa sasa hata Watanzania wamekuwa wakishuhudia Barcelona na Real Madrid zikicheza hata saa mbili za usiku, tofauti na zamani mechi zao zinakuwa usimu mnene kuanzia saa nne, tano hadi sita. Hii ina maana nao wamezipunguza mechi za usiku mwingi kutokana na masaa ya kwao. Bodi ya Ligi inapaswa kuliangalia hili. Hakuna ulazima wa mechi za Dar es Salaam kuchezwa usiku hasa zile za kawaida sana. Labda za kimataifa na zile mechi muhimu na zenye mvuto tu.

# Angalizo latolewa mtihani kidato cha IV ukianza leo

**Na Romana Mallya**

BARAZA la Mitihani la Tanzania (NECTA) limetangaza kuanza Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne (CSEE) na Maarifa (QT), ukifanyika kwa siku 18 kuanzia leo, huku likionya yeyote atakayejihusisha na udanganyifu wa aina yoyote hatabaki salama.

Onyo hilo limetolewa wakati kukiwa na hatua zilizochukuliwa dhidi ya waliodaiwa kujihusisha na vitendo vya udanganyifu katika Mtihani wa Taifa wa Darasa la Saba mwaka huu, baadhi ya walimu wakifikishwa mahakamani.

Kaimu Katibu Mtendaji wa NECTA, Athumani Amasi, alitoa onyo hilo jana mkoani Dar es Salaam wakati akitangaza idadi ya watahiniwa watakaofanya mtihani huo ambao alisema maandalizi yote yamekamilika.

Alisema idadi ya waliosajiliwa kufanya Mtihani wa Taifa wa Kidato cha Nne mwaka huu ni 566,840, kukiwa na ongezeko la watahiniwa 28,816 sawa na asilimia 5.36 kulinganishwa na mwaka jana ambao ulikuwa na watahiniwa 538,024.

Alisema kati ya watahiniwa wa mwaka huu watakayofanya mtihani huo, wa shule ni 535,001 na wa kujitegemea ni 31,839.

"Kati ya watahiniwa waliosajiliwa, wavulana ni 247,131 sawa na asilimia 46.19 na wasichana ni 287,870 sawa na asilimia 53.81. Wenye mahitaji maalum idadi yao ni 852. Kati yao, 480 ni wenye uoni hafifu, 62 wasioona, 19 wenye ulemavu wa kusikia, 152 wenye mtindio wa akili na 139 ni wenye ulemavu wa viungo vya mwili," alisema.

Amasi alisema kati ya watahiniwa wa kujitegemea 31,839 waliosajiliwa, wavulana ni 13,556 sawa na asilimia 42.58 na wasichana ni 18,283 sawa na asilimia 57.42 na wenye mahitaji maalum wako 13 ambapo wenye uoni hafifu ni wawili na wasioona ni 11.

Kwa upande wa Mtihani wa Maarifa, Amasi alisema watahiniwa waliosajiliwa ni 12,090, ambapo kati yao wanaume ni 4,096 sawa na asilimia 33.88 na wanawake ni 7,994 sawa na asilimia 66.12 na wenye mahitaji maalum jumla yao ni 36, wote wenye uoni hafifu.

"Wazazi, walimu, wasimamizi wa mtihani na wenye shule kutojihusisha na vitendo vyovyote vya udanganyifu wa mtihani. Wadau wote wanaombwa kutoa taarifa katika vyombo husika wanapobaini kuwapo mtu au kikundi cha watu kujihusisha na udanganyifu wa aina yoyote," alisisitiza.




Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandiliwa (katikati) ambaye amemwakilisha Mkuu wa Mkoa wa Tanga, Omari Mgumba, akikata utepe kuashiria kuzinduliwa kwa Mpango Mkazi wa Safari Salama na Endelevu kwa Jiji la Tanga uliondaliwa kwa ushirikiano wa wadau wote wa usalama barabarani na Shirika la Amend. Kulia ni Meya wa Jiji la Tanga, Abdulrahman Shilow, Meneja Miradi wa Shirika la Kimataifa la GRST kutoka Geneva, Uswis, Atsani Ariobowo (wa pili kulia). **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# HESLB yatangaza siku saba rufani za mikopo

**Na Mwandishi Wetu**

BODI ya Mikopo ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu (HESLB) imetangaza kufunguliwa kwa dirisha la rufani ili kutoa fursa kwa wanafunzi ambao hawakuridhika na viwango vya mikopo walivyopangiwa, kuwasilisha taarifa za uthibitisho ili kuongezewa viwango vya mikopo kulingana na uhitaji wao.

Mkurugenzi Mtendaji wa HESLB, Abdul-Razaq Badru, alisema jana jijini Dar es Salaam kuwa dirisha hilo la rufani litakuwa wazi kwa siku saba kuanzia jana na kuwa rufani kutoka kwa wanafunzi zinapaswa kuwasilishwa kwa njia ya mtandao.

"Hadi leo (jana), tumeshawapangia mikopo wanafunzi wa mwaka wa kwanza wapatao 68,422 na tunafahamu kuwa kuna wanafunzi ambao kwa sababu mbalimbali, hawakukamilisha nyaraka muhimu kuthibitisha uhitaji wao, dirisha la rufani ni fursa kwao," alisema Badru.

Kwa mujibu wa Badru, lengo ni kutoa mikopo kwa wanafunzi wapya 71,000 katika mwaka wa masomo 2022/23, akiwataka wanafunzi wanaowasilisha rufani, kusoma na kuzingatia maelekezo yaliyoko kwenye mfumo wa kuwasilisha rufani.

Kuhusu malipo, Badru alisema walishaanza kutuma fedha vyuoni hata kabla ya wanafunzi kufika vyuoni na kuwa kazi hiyo ni endelevu na kuwashauri wanafunzi waliopangiwa mikopo kufika kwa maofisa mikopo wa vyuo vyao ili kukamilisha taratibu za kupokea fedha.

"Pale mwanafunzi anapoona amepangiwa mkopo kupitia akaunti yake ya SIPA (Student's Individual Permanent Account), basi afike kwa ofisa mikopo wa chuo chake ambaye yupo palepale chuoni ili awasilishe taarifa zake za benki na kupokea fedha," alielekeza.

Badru alizishukuru taasisi za elimu ya juu na serikali za wanafunzi kwa ushirikiano wanaoipatia HESLB ambao umeendelea kuimarisha ufanisi katika kuwahudumia wanafunzi wanaonufaika na mikopo ya elimu ya juu inayotolewa na serikali kupitia bodi hiyo.

"Kwenye huu mnyororo wa kuwahudumia wanafunzi, uongozi wa vyuo, serikali za wanafunzi na jumuiya yao ya TAHLISO ni wadau muhimu, na wamekuwa wakitupatia ushirikiano mkubwa, tunawashukuru sana," alisema Badru.

HESLB ilianzishwa mwaka 2005 ikiwa na majukumu makuu mawili ya kutoa mikopo kwa wanafunzi wahitaji wa elimu ya juu na kukusanya mikopo iliyoiva ambayo ilianza kutolewa na serikali mwaka 1994/1995.

## KABWELA

Fadhili Mohamed



# CHADEMA: Tundu Lissu asiendelee kuwa mkimbizi

**Na Thobias Mwanakatwe,**
SINGIDA

CHAMA cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Mkoa wa Singida kimesema kimechoka kumwona Makamu Mwenyekiti wa chama hicho, Tundu Lissu akiishi ughaibuni kama mkimbizi, hivyo kuitaka serikali kumhakikishia usalama wake ili arejee nchini.

Mwenyekiti wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Emmanuel Jingu, alitoa kauli hiyo jana alipokifunga kikao cha viongozi wa majimbo kilichofanyika mjini hapo kwa lengo la kujadili mustakabali wa chama kuelekea uchaguzi wa ndani wa chama pamoja na uandikishaji wanachama kwa mfumo wa kidigitali.

"Tunatoa rai kwa serikali imhakikishie usalama Lissu arudi nchini maana anaishi ughaibuni kama mkimbizi, tumechoka mtu wetu kuwa mkimbizi huko, serikali itoe tamko Lissu arudi," alisema.

Jingu alisema chama kinapata athari kutokana na Lissu kuendelea kuishi nje kwa kuwa ni Makamu Mwenyekiti wa chama, hivyo kuwapo kwake nchini kutakisaidia chama.

"Wananchi wana shauku ya kumwoana Lissu hasa ikizingatia alikuwa mgombea urais mwaka 2020 na wanataka kujua nini kitafuata kama atarudi tena ulingoni mwaka 2025 au hataki, anapumzika au atarudi jimboni, sasa yeye akirudi ndiye aje awaeleze wananchi," alisema.

Mwenyekiti wa Baraza la Wanawake wa CHADEMA Mkoa wa Singida, Josephine Lemoyan alisema chama hicho kimeingia katika mfumo wa kuandikisha wanachama kidigitali ili kwenda na wakati wa sayansi na teknolojia.

"CHADEMA ni chama ambacho kinakwenda na teknolojia ya kiuchumi, huu ni ulimwengu wa TEHAMA, hivyo uandikishaji wanachama unakuwa rahisi," alisema.

Aliongeza kuwa kupitia mfumo huo wa kuandikisha wanachama upya na kutolewa kwa kadi za kielektroniki, kwa Mkoa wa Singida wanalenga kuandikisha wanachama zaidi ya asilimia 70 ya wapigakura.

Machi 2019, Rais Samia Suluhu Hassan akihojiwa na Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kuhusu suala la Lissu kurejea nchini, alisema akirejea nchini, ataishi kama Watanzania wengine wanavyoishi.

Kauli hiyo ya Rais Samia ilifuatia maombi ya mara kwa mara ya Lissu ambaye anaishi Ubelgiji kutaka serikali impe uhakika wa usalama wake atakaporejea nchini.

"Nihakikishie usalama wake kwani ana wasiwasi gani? Kwani nani hana usalama ndani ya nchi? Sisi sote tupo humu ndani tuko salama, akirudi ataishi kama Watanzania wanavyoishi, uamuzi wake," alisema Rais Samia baada ya mtangazaji kumtaka atoe kauli ya kumhakikishia usalama Lissu atakaporejea Tanzania.

Rais Samia alipoulizwa kuwa wasiwasi wa Lissu unatokana na watu waliomshambulia hawajapatikana na hakuna kesi iliyofunguliwa dhidi yao, alisema "uchunguzi utakamilikaje kama yeye (Lissu) ambaye ndiye mhusika hayupo nchini?"

Lissu, mgombea urais katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, yuko Ubelgiji tangu jaribio la kuuawa kwa risasi mjini Dodoma Septemba 2017 japo alirejea wakati wa kampeni za Uchaguzi Mkuu wa Mwaka 202o na kuondoka siku chache baada ya kutangazwa kwa matokeo yaliyompa ushindi Dk. John Magufuli (hayati).




Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, akibonyeza kitufe cha kompyuta kuchezesha droo ya kwanza ya Kampeni ya NMB MastaBata 'Kote Kote' jijini Dar es Salaam, mwishoni mwa wiki. Kushoto ni Meneja wa NMB Mlimani City, Deogratius Kawonga na Meneja Mwandamizi Idara ya Kadi na Biashara, Manfredy Kayala. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wakabidhiwa mamilioni, pikipiki kampeni ya NMB

**Na Mwandishi Wetu**

ZAWADI zenye thamani ya Sh. milioni 10.5 za droo ya kwanza ya kampeni ya NMB MastaBata 'Kote Kote' zilipata washindi mwishoni mwa wiki, 75 wakijishindia fedha Sh. milioni 7.5, huku Asumwisye Stallone akiibuka na zawadi ya bodaboda yenye thamani ya Sh. milioni tatu.

Kampeni hiyo inayoendeshwa na NMB kwa ushirikiano na MasterCard International, inatarajiwa kutoa zawadi mbalimbali zenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 350 katika kipindi cha miezi mitatu.

Akizungumza kabla ya droo hiyo, Meneja Mwandamizi wa Biashara ya Kadi wa NMB, Manfredy Kayala, alisema malengo makuu ya kampeni hiyo iliyoanzishwa mwaka 2018 ni kuihamasisha jamii katika kuachana na matumizi ya fedha taslimu, pia kurejesha sehemu ya faida yao kwa wateja.

"Kupitia kampeni hii ambayo ilianza kama NMB MastaBata (2018), ikaja NMB MastaBata Sio Kikawaida (2019), ikafuata NMB MastaBata Kivyako Vyako (2021), wateja wetu wanashauriwa kudumisha utamaduni wa matumizi ya kadi katika kufanya miamala na malipo yao, badala ya fedha taslimu ambazo ni changamoto kutembea nazo.

"Kampeni hii itaendelea kwa takribani miezi mitatu na washindi mbalimbali watapatikana. Kutakuwa na washindi wa kila wiki, kila mwezi na wale wa Grande Final. Wateja wanapaswa kufanya miamala yao na kulipa kwa kadi ili kujiwekea nafasi ya kushinda," alisema.

Kayala alifafanua kuwa, ukiondoa bodaboda moja na Sh. fedha kwa washindi 75 wa kila wiki, NMB MastaBata Kote Kote itatoa zawadi kwa washindi 49 wa droo za mwisho wa mwezi, sambamba na bodaboda mbili na droo ya fainali itazawadia safari za Dubai kwa washindi na wenza wao kwa siku nne.

Mbele ya Ofisa wa Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (GBT), Meneja wa NMB Kanda ya Dar es Salaam, Donatus Richard, alisema NMB MastaBata Kote Kote ni mwendelezo wa benki yake katika kuwafanya wateja wa Watanzania kugeukia utamaduni channya wa matumizi yasiyohusisha fedha taslimu.

Alifafanua kuwa, MastaBata Kote Kote inagusa wateja wote wa ndani na nje ya nchi wanaotumia kadi za MasterCard katika kufanya malipo na kwamba droo za kampeni hiyo zitakuwa kila wiki, huku akitoa wito kwa Watanzania kuhakikisha wanatumia kadi zao katika kufanya malipo na miamala mbalimbali ili kushinda.

"Tutafanya droo kila wiki na wateja watashinda fedha na bodaboda. Droo za mwisho wa mwezi zitawazawadia washindi wawili bodaboda na wengine fedha taslimu, wakati Grande Final tutakuwa na washindi saba na wenza wao kwa safari ya Dubai iliyolipiwa kila kitu na NMB," alisema Donatus. Alitoa wito kwa Watanzania na wateja wa NMB kuchangamkia zawadi zinazotolewa kwenye kampeni hiyo kwa kufanya malipo kwa njia ya kadi badala ya fedha taslimu, ili kujiongezea nafasi ya kuibuka washindi wa NMB MastaBata.

## Tril. 1/- kusambaza nishati salama ya kupikia vijijini

**Na Jenifer Gilla,** MISRI

WAKALA wa Nishati Vijijini (REA) umesema unatekeleza mradi wa kusambaza nishati safi ya kupikia vijijini utakaogharibu dola za Marekani milioni 450 (Sh. trilioni moja).

Lengo ni kupunguza matumizi ya nishati isiyo salama ya kupikia kutoka asilimia 85.7 mpaka asilimia 29 ifikapo mwaka 2030 ambao ni ukomo wa upimaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu.

Mkurugenzi wa Uendelezaji Masoko na Teknolojia kutoka REA, Advera Mwijage alisema hayo jana wakati wakala huo ulipowasilisha mkakati wa upatikanaji wa gesi salama na ya kisasa kwa asilimia 100 vijijini, mjini Sharm El She, Misri katika Mkutano wa 27 wa Nchi Wanachama wa Athari za Mabadiliko ya Tabianchi unaoendelea.

Alisema mradi huo umegawanyika katika mipango mitatu ikiwamo wa kusambaza gesi asilia unaotekelezwa katika mikoa ya Mtwara, Lindi na Pwani, ukijumuisha pia kusambaza mitungi ya gesi kupitia kampuni 13.

"Kwa huu wa mitungi ya gesi, tunaanza majaribio kwa kaya 100,000 nchi nzima kwa kuwa kila mtu anahitaji nishati salama ya kupikia, hivyo tutahakikisha kila mkoa unafikiwa ili wananchi waanze kuhamasika," alisema.

Alitaja mradi mwingine ni wa kutoa elimu ya namna ya kutengeneza mkaa mbadala kwa kutumia mabaki ya taka hasa zitokanazo na mpunga, mahindi na mbao. Alisema pia wameshaanza mazungumzo na kampuni zinazotengeneza umeme kwa kutumia kinyesi, ili kujenga mitambo kwa ajili ya kutengeneza nishati ya kupikia. "Tuliagizwa kwamba kila taasisi ambayo ina zaidi ya watu 300 tuangalie namna ya kuwapelekea nishati bora, kwa hiyo tumeshaanza kufuatilia kwenye shule na magereza na kadhalika," alifafanua.

Ofisa huyo pia alisema watatengeneza majiko yanayotumia nishati kidogo ili kupunguza matumizi ya nishati, ikiwa ni njia mojawapo ya kuwahamisha watumiaji hao katika matumizi ya nishati isiyo salama. Alisema mpaka sasa zimepatikana Sh. bilioni 23 kwa mwaka huu wa fedha na bajeti itaendelea kuongezwa kadri siku zinavyosogea kwa kuwa mahitaji ni makubwa, akiwa na angalizo kwamba kila mwaka ekari 400,000 za miti zinakatwa kwa ajili ya matumizi hayo.

Mkurugenzi wa Kampuni ya PaulSam Geo Engineering, Paul Gongo, inayojishughulisha na utunzaji wa mazingira Tanzania, alisema mradi huo ukikamilika utapunguza matumizi ya kuni ambayo ni moja ya vyanzo vya upotevu wa misitu. "Ni jambo zuri kwa kuwa upotevu wa misitu unachangia kutopea kwa vitu vingi ikiwamo hewa safi, na nafikiri ni vizuri ukaanzia vijijini kwa sababu ndiko kwenye matumizi makubwa ya nishati hiyo," alisema.

Mwenyekiti wa Shirikisho la Vyama vya Kilimo Kusini mwa Afrika (SACAU), Dk. Sinare Yusuph, alisema mradi huo utasaidia kuwapo misitu ya kutosha ambayo ni chanzo kikuu cha mvua na kuondoa ukame ambao umeziingiza nchi nyingi kwenye shida katika upatikanaji wa maji.

HABARI KITAIFA

## Waziri ajivunia utajiri makaa ya mawe nchini

**Na Mwandishi Wetu,** MBIGA

NAIBU Waziri wa Madini, Dk. Steven Kiruswa, amesema biashara ya makaa ya mawe inatarajia kuleta tija kwa Watanzania kutokana na uhitaji mkubwa wa madini hayo ndani na nje ya nchi.

Dk. Kiruswa alitoa kauli hiyo jana wilayani Mbinga mkoani Ruvuma alipotembelea mgodi wa uchimbaji wa makaa ya mawe wa Ruvuma Coal Ltd ili kujionea shughuli za uchimbaji zinazoendelea katika mkoa huo.

Alisema serikali imeweka mazingira wezeshi ya uwekezaji katika Sekta ya Madini yanayovutia wawekezaji kutoka nchi mbalimbali duniani kuja kuwekeza na kufanya biashara ya madini mbalimbali yakiwamo makaa ya mawe.

Alipongeza mikakati ya serikali kuboresha miundombinu ya barabara ili kurahisisha usafirishaji wa makaa ya mawe kutoka kwenye migodi hususan barabara ya kuelekea mkoani Mtwara ili kusafirisha makaa ya mawe hayo kupitia bandari.

Mkuu wa Wilaya ya Mbinga, Aziza Mangosongo, alisema kuwapo mgodi huo kumesaidia wilaya hiyo kupata faida nyingi katika kutekeleza shughuli za kijamii ikiwamo ujenzi wa shule na vituo vya afya.

Alisisitiza wadau wa makaa ya mawe katika wilaya hiyo kushiriki mkutano ulioandaliwa na Wizara ya Madini ili kujifunza uwajibikaji wa kampuni kwa jamii (CSR) katika siku zilizopangwa ili kupata uelewa zaidi.

Mbunge wa Mbinga Vijijini, Benaya Kapinga alisema makaa ya mawe yanahitajika kwa wingi duniani kwa sasa, akiitaka serikali itumie fursa hiyo kuhakikisha wilaya inapata faida ya kuwapo migodi kwa kutoa ajira na kuleta maendeleo kwa jamii zinazozunguka migodi hiyo.

Meneja Mkuu wa Mgodi wa Makaa ya Mawe Ruvuma, Benedicto Mshingwe, alisema kuwa hadi sasa mgodi huo umetoa ajira zaidi ya 700 kwa Watanzania hususan wanaozunguka mgodi.

Pia alisema mgodi umeendelea kushiriki katika shughuli za kijamii ikiwamo ujenzi wa madarasa na zahanati ili kujenga uhusiano mzuri na wenyeji.

Awali Dk. Kiruswa alikutana kwa mazungumzo na Mkuu wa Mkoa wa Ruvuma, Kanali Laban Thomas na wadau mbalimbali wa sekta ya madini, mazungumzo yao yakilenga shughuli za uchimbaji madini zinazofanyika katika mkoa huo na vikwazo wanavyopitia.



Mjumbe wa Bodi ya Wakurugenzi ya Benki ya Biashara ya DCB, Dk. Amina Baamary (wa tatu kulia), Mkurugenzi Mtendaji wa DCB, Godfrey Ndalahwa (wa nne kushoto), na baadhi ya wafanyakazi wa benki hiyo, wakishangilia baada ya kupokea tuzo ya mshindi wa kwanza ya Benki Bora kwa kutoa Huduma Bora kwa wateja nchini kwa mwaka 2022 katika hafla ya utoaji zawadi kwa washindi wa Tuzo za Chaguo la Walaji Afrika (CCAA) jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# TAKUKURU yarejesha fedha zilizofujwa miradi halmashauri

**Na Said Hamdani,** LINDI

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) mkoani Lindi imefanikiwa kuokoa na kuzirejeshwa kwenye akaunti ya miradi husika Sh. milioni 12.59 zilizokuwa zimefujwa na watumishi wa halmashauri za wilaya.

Mkuu wa taasisi hiyo mkoani hapo, Abnery Mganga, alitangaza hatua hiyo mwishoni mwa wiki alipotoa taarifa ya utendaji wao mbele ya waandishi wa habari kwa kipindi cha miezi mitatu kuanzia Julai hadi Septemba mwaka huu.

Alisema urejeshwaji huo umetokana na ushirikiano kati ofisi ya taasisi hiyo na watumishi katika kudhibiti vitendo vya uvujaji wa fedha zinazotolewa na serikali na kupelekwa halmashauri za wilaya na manispaa kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mganga alisema kupitia udhibiti wa vitendo vya rushwa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo, katika kipindi hicho, TAKUKURU Mkoa wa Lindi imefuatilia miradi 13 yenye thamani ya Sh. bilioni 5.42 katika sekta za maji, barabara, afya na elimu kwenye kata za Kilangala na Mingoyo (Wilaya ya Lindi), Marendego (Kilwa), Ruangwa na Lindi Manispaa.

Alisema ufuatiliaji huo ulibaini miradi mitatu, sawa na asilimia 23, ilikuwa na upungufu kidogo, ikiwamo kuchelewa kukamilika, matumizi ya fedha nje ya maelekezo, BOQ kutokuwapo eneo la kazi, kamati ya ununuzi kutoshirikishwa na baadhi ya miradi kujengwa maeneo yenye migogoro.

Alibainisha kuwa katika kipindi cha mwezi Julai hadi Septemba, taasisi hiyo imepokea malalamiko (36), huku vitendo visivyohusiana na rushwa vikiwa 19 na vinavyohusu rushwa vikiwa 17. Alisema serikali za mitaa zinaongoza kwa kulalamikiwa mara 10, zikifuatwa na utawala (6), ushirika (4), elimu na sekta binafsi (3 kila moja), wakati ardhi, fedha, afya, misitu, kilimo, Jeshi la Polisi na takwimu wakilalamikiwa mara mmoja kwa kila taasisi.

Alisema ofisi yake, ikishirikiana na mwendesha mashtaka itaendelea kuchunguza na kuchukua hatua stahiki dhidi ya watakaobainika kufuja mali za umma kwa kuwafikisha mahakamani.

Alisema katika robo ya pili ya mwaka, Oktoba hadi Desemba mwaka huu, taasisi hiyo imejipanga kutekeleza majukumu ya kudhibiti vitendo vya rushwa katika ununuzi wa umma, ukusanyaji mapato ya serikali, huduma muhimu, ufuatiliaji rasilimali za umma, miradi ya maendeleo na kukuza ushirikiano na wadau kwa kutumia mbinu mbalimbali.

# Vodacom yapongeza uamuzi kupitia upya tozo za miamala

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya mawasiliano ya Vodacom Tanzania imetangaza matokeo yake ya hesabu za fedha za nusu mwaka, zikionyesha kuongezeka kulinganisha na kipindi kama hicho mwaka uliopita.

Vilevile, uongozi wa kampuni hiyo umepongeza uamuzi wa serikali kupitia upya tozo za miamala ya kielektroniki, ukisifu kuwa ni hatua nzuri.

Imebainishwa kuwa katika kipindi hicho, kampuni hiyo imefanikiwa kuongeza asilimia 4.7 ya mapato ya huduma kutokana na utendaji mzuri katika maeneo ya mauzo ya data, kuongezeka tena kwa matumizi ya M-Pesa na mapato yameongezeka mara mbili kutokana na huduma nyinginezo zisizobadilika.

Katika taarifa yake kuhusu matokeo hayo ya kifedha, Mkurugenzi Mtendaji wa Vodacom Tanzania, Philip Besiimire, alisema jana kuwa: "Uamuzi wa serikali kupitia upya tozo za miamala ya kutuma na kutoa fedha kwa njia ya simu iliyoanzishwa tarehe 15 Julai 2021, ni hatua nzuri.

"Punguzo hili ni muhimu sana kwa watumiaji kufanya miamala ya kifedha na umewezesha kuchangia kuongezeka mapato katika kipindi cha robo ya pili cha mwaka na kufanikisha uwezo wetu wa kujumuisha Watanzania wengi kupata huduma rasmi za kifedha. Kwa sasa watumiaji wa M-Pesa wameongezeka tena kutoka milioni 7.7 hadi asilimia 19.6." Alisema mwelekeo wa mapato wa M-Pesa unaonyesha mwelekeo unaoendelea wa Vodacom katika kuendesha huduma za kibunifu, kutumia uwezo wa kimkakati kutoka kitovu cha M-Pesa Afrika na kuharakisha fursa katika maeneo mapya ya ukuaji ikiwa ni pamoja na mikopo ya kidijitali na huduma za mikopo ya kufanikisha biashara, bima na malipo ya kibiashara.

Alikumbusha kuwa M-Pesa ilichaguliwa kama huduma sahihi ya kusaidia mpango wa serikali wa kutoa fedha kusaidia kaya maskini chini ya Mfuko wa Maendeleo ya Jamii (TASAF).

"Katika kipindi cha miezi sita ya kwanza ya mwaka wa fedha, Vodacom Tanzania imewezesha wateja wake kuingia katika ulimwengu mpya wa kidijitali kwa mara ya kwanza kwa kuzindua mtandao wa intaneti wa 5G nchini, ambao ni hatua kubwa ya uvumbuzi na teknolojia nchini.

"Kampuni pia iliwekeza Sh. bilioni 74.9 katika matumizi ya mtaji ili kusaidia ukuaji wa biashara na usambazaji wa huduma za mawasiliano. Uwekezaji huu ulielekezwa kupanua mtandao, ikijumuisha ujenzi wa vituo vipya 159 vya kuwezesha intaneti ya 4G na vituo 63 vya awali vya kufanikisha intaneti ya 5G pamoja na uboreshaji wa miundombinu.

"Uwekezaji wa kipindi hicho umefanikisha ukuaji wa asilimia 30.1 wa matumizi ya data kwenye mtandao wa Vodacom. Hivi karibuni tulipata masafa ya kutuwezesha kuwa katika nafasi nzuri ya kuongoza katika soko kupitia mchakato wa mnada," alisema.

Alibainisha kuwa kwa mtazamo wa kibiashara, wigo wa wateja wa Vodacom uliongezeka kwa asilimia 5.1 kufikia milioni 16 wakati watumiaji wa data waliongezeka kwa asilimia 1.2 hadi milioni nane kutokana na uwekezaji mkubwa uliofanywa katika kipindi hicho.

Alisema Vodacom inaendelea kutumia majukwaa yake ya mifumo ya kidigitali inayojulikana kama M-Kulima na M-Mama ili kusaidia kuboresha huduma katika jamii.

# DC awaonya wanaochochea migogoro wakulima, wafugaji

**Na Said Hamdani,** LINDI

KATIKA kuhakikisha matukio ya mauaji na migogoro kati ya wafugaji na wakulima inadhibitiwa, Mkuu wa Wilaya ya Ruangwa mkoani Lindi, Hassani Ngoma, amesema atachukua hatua kali dhidi ya mtu yeyote atakayebainika kufanya vurugu.

Ngoma alitoa kauli hiyo wakati wa kikao kazi kilichowakutanisha Mkuu wa Mkoa huo, Zainabu Telak na wamiliki wa mifugo kilichofanyika mjini Lindi juzi.

Akichangia hoja kwenye kikao hicho, Ngoma alisema hakuna sababu serikali za mkoa na wilaya zilizopewa majukumu ya kuongoza wananchi na mali zao kufumbia macho mateso na mauaji wanayofanyiwa wakulima na baadhi ya wafugaji wasiofuata sheria na taratibu zilizowekwa.

Ngoma alifafanua kuwa wamiliki wa mifugo si tatizo, bali vijana wanaopewa kazi ya kuchunga wanyama wao, akisisitiza kuwa wengi wao wameonekana kuwa na 'mioyo ya ukatili' wanapotekeleza majukumu ya uchungaji kwa kufanya vitendo viovu dhidi ya wakulima.

Alisema ukatili walionao vijana hao unatokana na wamiliki wa mifugo kutowapa elimu, ikiwamo kuwazuia kupeleka wanyama wao kulisha katika mashamba ya wakulima, huku akibainisha kuwa ndani ya wilaya yake, watu watatu (bila kutaja majina) wameuawa na wachungaji wa mifugo.

"Hivi ninapoongea hapa leo hii, watu watatu wilayani kwangu waliuawa juzi kwa kuchomwa mikuki na wafugaji," alisema Ngoma.

Alibainisha kuwa katika Wilaya ya Ruangwa anayoiongozo, wafugaji wanaotambulika kisheria ni watatu na wamepewa eneo la kuishi na mifugo yao katika Kijiji cha Kiperemende.

Wamiliki wa mifugo walizungumza na Nipashe, walidai kuwa matatizo yote hayo yanachangiwa na baadhi ya wenyeviti wa vijiji, watendaji wa vijiji na kata kupokea kitu kidogo (rushwa) kutoka kwa wafugaji wanaoingia kinyemela bila kufuata taratibu zilizowekwa na mamlaka husika.



Meneja Biashara na Masoko Coca-Cola Kwanza, Wahida Mbaraka (katikati), akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni wa wiki wakati akitangaza Tamasha la Biriani Friday na Coke awamu ya pili ambalo litafanyika Dodoma mwishoni mwa mwezi huu. Lengo ni kuendeleza utamanduni wa msosi na Coca-Cola. Kulia ni Meneja wa Bendi ya Bushoke, Anileth Bushoke. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Bilioni 9/- zatengwa mafunzo uanagenzi

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imetenga Sh. bilioni tisa kwa ajili ya mafunzo ya uanagenzi kwa vijana yatakayowawezesha kuwa na ujuzi unaohitajika kwenye soko la ajira wanapohitimu masomo yao.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu (Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu), Prof. Joyce Ndalichako, alibainisha hayo mwishoni mwa wiki wakati akizungumza kwenye mahafali ya 57 ya CBE yaliyofanyika kwenye viwanja vya chuo hicho jijini Dar es Salam ambapo wahitimu 1,065 walitunukiwa vyeti vya ngazi mbalimbali.

Alisema serikali katika mwaka wa fedha wa 2021/22 ilitenga Sh. bilioni tisa ambazo ziliwezesha vijana zaidi ya 62,000 kupata mafunzo ya uanagenzi na katika mwaka wa fedha wa 2022/23 imetenga kiasi kama hicho tena kwa ajili ya kuendelea kutoa mafunzo ya uanagenzi.

Waziri alivitaka vyuo kuzingatia mafunzo ya vitendo kwa wanafunzi vyuoni ili kuondoa malalamiko kutoka kwa waajiri kwamba wahitimu wengi hawana ujuzi.

Alisema hali hiyo imekuwa ikisababishwa na mafunzo mengi kufanyika kwa nadharia, akikipongeza Chuo cha CBE kwa kuanzisha programu ya uanagenzi ambapo mwanafunzi anasoma nusu ya masomo chuoni na nusu akiwa kazini.

"Malalamiko ni kwamba wahitimu wengi wanatoka vyuoni wakiwa na ujuzi ule ambao siyo unaohitajika kwenye soko la ajira na soko linahitaji rasilimali kazi ambayo vyuo havitoi kwa ukamilifu wake kutokana na kukosekana kwa mafunzo kwa vitendo.

"Ndiyo sababu ninaipongeza CBE kwa kuanzisha programu ya uanagenzi ambayo mwanafunzi anakuwa darasani kwa asilimia 50 na anakuwa sehemu ya kazi kwa asilimia 50 na kwa kufanya hivi, mnatatua changamoto iliyokuwapo ya kuwa na wahitimu ambao hawana ujuzi sawasawa," alisema.

Alipongeza CBE kwa kuanzisha programu atamizi kutoa nafasi kwa vijana kuatamia ujuzi wao na alitaja vyuo vingine kama Mzumbe, Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) na Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA) vimeshaanzisha programu kama hizo.

Alimpongeza Prof. Emmanuel Mjema kwa kazi nzuri aliyoifanya akiwa mkuu wa chuo hicho kwa kipindi cha miaka 10 kwa kuwa chini yake chuo kimepata mafanikio makubwa kitaaluma, akikumbusha kuwa alikipokea kikiwa katika hali mbaya.

# Mbwa ajeruhi watu 6

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU sita akiwamo mtoto mwenye umri wa miaka mitatu, wote wakazi wa Kijiji cha Mchakama, Kata ya Mandawa, Wilaya ya Kilwa mkoani Lindi, wanauguza majeraha waliyoyapata baada ya kung'atwa na mbwa anayedaiwa kuwa na kichaa.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka kijijini huko zilizothibitishwa na uongozi wa kijiji hicho, tukio hilo lilitokea juzi majira ya saa tatu asubuhi.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mchakama, Mohamedi Mpinga alisema mbwa huyo anayedaiwa kutoka Kijiji jirani cha Mavuji, aliwashambulia watu hao eneo la soko na waliokuwa majumbani.

Mbinga aliwataja walioshambuliwa ni mtoto mwenye umri wa miaka mitano (jina tunalihifadhi) aliyeng'atwa miguu yote; Somoe Kampinji (mikononi na tumboni), Halima Mchelenga (miguu wa kushoto na mikononi), Yasini Ngachenga (miguu yote), Halima Saidi (paja la mguu wa kulia), Hadija Mkunjile (mikono yot) na Ndumbo Mkunjire.

Alisema kuwa kufuatia kitendo hicho, baadhi ya wananchi walichukua silaha za jadi kukabiliana na mbwa huo lakini jitihada zao hazikuzaa matunda kutokana na mbwa huyo kukimbilia porini.

Mwenyekiti huyo alisema majeruhi walipelekwa kwenye zahanati ya kijiji chao kwa ajili ya kupata matibabu lakini hawakupata huduma kutokana na zahanati hiyo kutokuwa na dawa za kutibu waliong'atwa na mbwa mwenye kichaa, hivyo kuelekezwa kwenda Hospitali ya Wilaya ya Kilwa (Kinyonga) iliyoko mji mkongwe wa Kivinje.

Aliendelea kubainisha kuwa walipofika hospitali huko, nako walikosa dawa hizo, majeruhi watatu kati ya sita (Yasini, Halima na Hadija) wakipelekwa Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Lindi.

Alishauri maofisa mifugo kuwa na utaratibu wa kupita majumbani kuchanja wanyama wote wakiwamo mbwa.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Mchakama, Mkwepu Mkwepu alikiri kutokea tukio hilo, akibainisha kuwa ni la kwanza kwake kulishuhudia kijijini huko.

# Tamasha la Coca-Cola awamu ya II mwezi huu

**Na Mwandishi Wetu**

KAMPUNI ya Coca-Cola Kwanza kupitia kampeni yake ya Biriani Friday na Coka iliyoanza rasmi mwaka jana na kuendelea mpaka sasa ikiwa na lengo la kuendeleza utamaduni wa chakula na Coca-Cola, litafanyika Novemba 26 mwaka huu jijini Dodoma.

Katika tamasha hilo, Coca-Cola hutembelea wadau wake mbalimbali wanaojishughulisha na upikaji biriani kila Ijumaa kwa kuwaunga mkono na kuhakikisha wanawapatia wateja wao wote vinywaji vya kampuni hiyo kwenye migahawa yao na kuwawezesha migahawa na vitendea kazi.

Imebainishwa na uongozi wa kampuni hiyo kuwa hadi sasa kampeni hiyo imeshafikia migahawa zaidi ya 50 katika mikoa ya Dar es Salaam, Dodoma, Morogoro, Tanga, Mtwara, Mbeya na visiwani Zanzibar.

Akizungumza jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki wakati wa kutangaza tamasha hilo, Meneja Biashara na Masoko Coca-Cola Kwanza, Wahida Mbaraka alisema tamasha la Birian Festival na Coke awamu ya pili litafanyika Dodoma mnamo tarehe 26 Novemba mwaka huu katika viwanja vya wajenzi Maili Mbili kuanzia saa nne asubuhi.

"Kwenye tamasha ili, tutawakutanisha kwa pamoja wapishi wa biriani wa mkoa huu na wateja wao, tamasha la mwaka huu litakuwa ni la kipekee kabisa na utofauti mkubwa kwa sababu tutapata ladha ya vyakula vya asili vya Dodoma, vionjo vingi vya kiasili ambavyo vinabeba utaifa wetu, na vilevile kuangalia mechi za Kombe la Dunia," alisema.

Meneja huyo alibainisha kuwa kutakuwa na migahawa zaidi ya 15, michezo ya watoto huku kukitolewa burudani kutoka bendi ya Bushoke na kwamba zawadi mbalimbali zitatolewa kwa washiriki.

"Kupitia jukwaa hili, ninapenda kuchukua nafasi hii kuwakaribisha watanzania wote, wapenzi na wadau wa biriani na Coca-Cola, familia, marafiki kuja kujionea na kushiriki kwenye utamaduni huu. Tanzania nchi yetu, Dodoma ndio makao makuu yetu, biriani na Coca-Cola ndiyo chaguo letu," alitamba.





## Serikali yatoa mil. 590/- upanuzi wa zahanati Kata ya Mwandeti

**Na Allan Isack,** ARUMERU

HATIMAYE serikali imewakumbuka wananchi wa Kata ya Mwandeti katika Wilaya ya Arumeru mkoani Arusha, waliokuwa wakitaabika kufuata huduma za afya kwenye vijiji vya jirani, baada ya kutoa Sh. milioni 590 kwa ajili ya upanuzi wa zahanati hiyo.

Zahanati hiyo iliyoko Halmashauri ya Arusha, ilikuwa katika hali duni kwa ukosefu wa miundombinu ya uhakika ya kuruhusu utoaji huduma kwa wananchi wa eneo hilo kwa wakati wote.

Taarifa kuhusu mpango wa upanuzi wa zahanati hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa halmashauri hiyo, Selemani Msumi.

"Lengo la serikali kutoa fedha hizo ni kuendelea kuboresha upatikanaji wa huduma za afya, kwa kuzisogeza karibu na wananchi kupunguza tatizo la vifo vya watoto na mama wajawazito wakati wa kujifungua.

"Hizo fedha ni mahususi kwa ajili ya ujenzi wa OPD (jengo la wagonjwa wa nje), jengo pacha la mama na mtoto, upasuaji, maabara, jengo la mionzi, sehemu ya kufulia na nyumba moja ya watumishi ya kuishi familia tatu."

Aidha, Msumi, alisisitiza kuwa Sh. milioni 500 zinatokana na tozo ya miamala ya simu, na Sh. milioni 90 ni za Mpango wa Maendeleo kwa Ustawi wa Taifa na Mapambano dhidi ya UVIKO-19.

Akizungumzia upanuzi huo, Diwani wa Kata ya Mwandeti, Logolie Lukumay, alisema zahanati hiyo itasaidia wananchi wake, kwa kuwa waliteseka kutafuta huduma za afya kwa gharama kubwa na wengine walipoteza maisha kwa kukosa huduma.

Mganga Kiongozi wa Zahanati ya Mwandeti, Dk. Aidan Martine, alisema kuwapo kwa nyumba za watumishi katika eneo lao la kazi, kutawaongezea ari ya kufanya kazi kwa weledi ili kutimiza majukumu yao ikiwamo utoaji wa huduma kwa wagonjwa kwa urahisi na kwa haraka kwa wakati wote.

"Daktari na wauguzi wanapoishi ndani ya eneo la kazi, inawarahisishia utekelezaji wa majukumu yao. Kwa mfano kuingia kazini kwa wakati, kutoa huduma kwa haraka hasa kwa huduma za dharura," alieleza Dk. Martine.

Zahanati ya Mwandeti, iko umbali wa zaidi ya kilomita 47 kutoka makao makuu ya Halmashauri ya Arusha.

Eneo ambalo wananchi wake, waliteseka kwa muda mrefu kwa kutembea umbali mrefu kutafuta huduma za afya jambo ambalo lilisababisha baadhi ya watu kupoteza maisha kwa kukosa au kwa kupata huduma kwa kuchelewa.

# Kampuni yafungua fursa masoko ya ndizi

**Na Mwandishi Wetu,** ROMBO

KAMPUNI ya Kimataifa ya East Africa Foods, imefungua milango ya masoko katika wilaya za Rombo na Moshi, mkoani Kilimanjaro, ili kuwawezesha wanufaike na fursa zilizoko pamoja na biashara katika kukua kiuchumi na kuchangia uchumi wa nchi.

Neema hiyo ya masoko ya uhakika ya zao la ndizi, inalenga kuwanufaisha wakulima zaidi ya 15,000 mwaka ujao, baada ya kufunguliwa kituo kipya cha kukusanyia ndizi eneo la Mamsera, Wilaya ya Rombo.

Akizungumza jana, wakati wa uzinduzi wa kituo hicho, Mkurugenzi Mtendaji wa Kampuni hiyo ya EA Foods, Elia Timotheo, alisema uamuzi wa kufungua soko hilo unatokana na wakulima wa ndizi kupata hasara kila mwaka kutokana na kukosa soko la uhakika, huku madalali wakijitajirisha nyuma ya jasho la mkulima.

"Zao la ndizi limekuwa likipata uharibifu, kwa sababu ya kukosa soko. Ndizi zinaharibika shambani, ndizi zinaharibika barabarani. Sisi tukaona hiyo ni fursa ya kuweza kuongeza kiwango cha kununua ndizi na kutumia utaalamu wa kuzihifadhi, kuzisafirisha na kuzisambaza kwa wateja ili kumaliza tatizo la ndizi kuharibika kwa kukosa soko.

"Tunao mkakati wa kufungua masoko ya nje katika nchi saba wanachama wa Jumuiya ya Afrika ya Mashariki. Huu tulioanza ni msingi kwa wakulima kuzalisha mazao mengi na bora zaidi. Soko ni kubwa na ndio maana jina letu ni EA Foods. Hiyo ni kwa sababu tunaamini kwamba lengo la kampuni ni kuweza kwenda katika nchi nyingine."

Kituo hicho cha Mamsera, kina uwezo wa kukusanya ndizi 1,000 kwa siku, tofauti na awali kilikuwa kikikusanya ndizi 500.

Kabla ya uzinduzi huo, Mratibu wa operesheni za ndizi wa EA Foods, katika mikoa ya Kanda ya Kaskazini, Firmina Joseph, alisema mnyororo wa thamani wa zao hilo ambao wanaufanya kupitia kampuni hiyo, una nia ya kufuta watu wanaoitwa madalali.

"Pia mnyororo huu wa thamani tunaoufanya unalenga kufanikisha biddhaa ya ndizi inayotoka shambani, inamfikia mlaji wa mwisho, ikiwa katika thamani yake ile ile.

Kama ndizi inauzwa Sh. 15,000 inatakiwa imfikie mlaji wa mwisho ikiwa na thamani ile ile badala ya kumfikia mlaji ikiwa na thamani ya Sh. 3,000 au 5,000 ni kosa.

EA ilikataa kuwatumia madalali, ikasema haiwezi kutoka Dar es Salaam iende ikanunue ndizi Moshi au Rombo impelekee Dar es Salaam, kwa sababu mwisho wa siku atawalangua wakulima."

Kwa mujibu wa mratibu huyo, uwezo wa kituo hicho kukusanya ndizi kutoka kwa wakulima kwa mwaka 2021 ulikuwa tani 5,400, lakini kufikia mwaka huu kiliongeza uwezo na kufikia 7,257.

Alisema zaidi ya wateja 7,000 wanategemea ndizi hizo kila siku katika Jiji la Dar es Salaam na muda mfupi ujao, kampuni hiyo itafungua masoko mengine katika visiwa vya Zanzibar na Jiji la Dodoma.

EA Foods, inanunua na kusafirisha mazao mengine kama mchele, vitunguu na viazi ambayo mahitaji ya sasa yalifikia tani 12,096 kwa mwaka 2021 na mwaka huu yamefikia tani 18,144.

Aidha, Diwani wa Mamsera, Sheldon Shayo, alisema namna wananchi wa Rombo walivyolipokea soko hilo maarufu 'Sokochap' alisema asilimia 98 ya wakulima, hasa wanawake wameanza kubadili mfumo wa maisha na utegemezi katika familia umepungua.

Mmoja wa wakulima, Beatrice Silayo, Mkazi wa Kata ya UbetuKahe, alisema yeye sasa ni wa tofauti kwa sababu amefanya biashara ya ndizi na madalali na amerushwa fedha zake na kujikuta akiwa masikini, lakini ujio wa 'sokochap' umemwezesha kusomesha watoto wake wawili shule za mchepuo wa Kiingereza ambazo anawalipia Shilingi milioni nne kwa mwaka.



Wananchi wa Wilaya ya Babati mkoani Manyara wakiwa kwenye mkutano kuhusu marekebisho ya bei za huduma za majisafi ambao umeandaliwa na Mamlaka ya Majisafi na Usafi wa Mazingira Babati (WSSA) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA) juzi. **PICHA: JALIWASON JASSON**

# Mamlaka yapandisha maji kumudu uendeshaji

**Na Jaliwason Jasson,** MANYARA

MAMLAKA ya Majisafi na Usafi wa Mazingira katika Mji wa Babati, mkoani Manyara, imeomba kibali cha kupandisha bei ya matumizi ya maji ili kumudu gharama za uendeshaji ambazo zimezidi kupaa.

Licha ya kupaa kwa gharama za uendeshaji, pia Babati WSSA inahitaji kufanya maboresho makubwa katika miundombinu yake ya maji ili kuongeza upatikanaji wa huduma hiyo.

Mapendekezo hayo yalitangazwa mwishoni mwa wiki na Mkurugenzi Mtendaji wa Babati-WSSA, Iddy Msuya, wakati akiongea na waandishi wa habari.

"Nia yetu ya kuja na marekebisho ya bei ya huduma za majisafi ni njema, na ndiyo maana tumekuja hapa mbele ya wadau wetu, ambao ni wateja kuomba kuwasilisha kwao mapendekezo ya kupandisha bei.

"Tunataka kuongeza ubora kwa kuwa na huduma zenye tija kwa wananchi tunaowahudumia. Bei zinazopendekezwa kwa mwaka 2022/2023 ni uniti moja kuuzwa kwa Sh. 2,481 kutoka 1,825 kwa uniti moja kwa bei ya sasa," alisema Msuya.

Alitaja sababu zinazowafanya wapandishe bei ni vifaa vya kuunganishia maji kuwa na gharama kubwa, ikilinganishwa na zamani.

Sababu nyingine miundombinu kuwa chakavu na kushindwa kumudu kutoa huduma kwa ufanisi na nia ya kutaka kuongeza mtandao wa maji zaidi ya kilometa 240 ifikapo mwaka 2025.

"Kuna gharama za uendeshaji, utawala na utumishi, lakini tunahitaji wateja waache kutumia vocha kutupigia wakiwa na shida tunataka tuwe na simu ya huduma kwa mteja gharama za kupiga ni zetu," alieleza zaidi Msuya.

Awali, Meneja Huduma kwa Wateja wa Babati-WSSA, Rashid Charahani, akizungumza kwenye mkutano huo wa wadau wa maji, alisema mabadiliko hayo yatasaidia kuongeza idadi ya wateja wa sasa 18,421 hadi kufikia 25,425.


"Tukikubaliwa kuongeza bei ya matumizi ya maji, tutaongeza mapato yetu tunayokusanya kutoa Sh. milioni 240 mpaka kufikia Sh. milioni 340 kwa mwezi mmoja," alisema Charahani.

Kuhusu upotevu wa maji, alisema utafiti wa Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), umegundua maji yaliyokuwa yanapotea katika kipindi cha nyuma ni asilimia 38.3, kwa sasa kimepungua kwa asilimia 23.

Aidha, alisema hali ya upatikanaji wa maji kwa Babati Mjini ni asilimia 94 huku maeneo na kiasi kinachopatikana ni Bashneti (55), Kateshi (51), Magugu (71) na Gallapo (45).

Baada ya kuwasilishwa pendekezo hilo, Kaimu Mkurugenzi wa EWURA, Walter Geofrey, alisema wanahitaji wananchi wapate maji kwa ubora unaotakiwa na bei hiyo inayopendekezwa itasaidia huduma kuwa endelevu.

Naye Ofisa Msaidizi Huduma kwa Wateja na Utawala wa Baraza la Ushauri la Watumiaji wa Maji na Nishati (EWURA CCC), Neema Nnko, alishauri kuongezwa idadi ya watumiaji wa maji na kupunguzwa kwa kiwango cha maji yanayopotea katika miradi ya mamlaka hiyo.





# Waendesha bodaboda, wanafunzi waingizwa mpango kukabili ajali

**Na Oscar Assenga,** TANGA

SHIRIKA la Amend Tanzania, limezindua mpango kazi wa safari salama na endelevu kwa waendesha pikipiki (bodaboda), wanafunzi wa shule za msingi na sekondari, unaolenga kupunguza idadi ya vifo na majeruhi vinavyotokana na ajali za barabarani nchini.

Kwa mujibu wa Meneja Mkazi wa Shirika hilo, Saimon Kalolo, msukumo wa kuanzisha mpango huo unatokana na takwimu za ajali kuonyesha waathirika wengi zaidi ni watoto na vijana wenye umri kati ya miaka mitano mpaka 29.

Klolo alikuwa akizungumza mwishoni mwa wiki jijini Tanga, wakati wa uzinduzi wa mpango huo, unaofadhiliwa na Botnar Foundation, Halmashauri ya Jiji la Tanga na wadau wengine.

"Hawa ndiyo waathirika wakubwa zaidi wa ajali za barabarani katika Bara la Afrika, Tanzania na ulimwenguni kote. Ni kundi ambalo linalohitaji elimu, kwa sababu wapo barabarani siku zote wakitafuta maisha.

"Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, zinapoteza zaidi ya asilimia tatu ya pato la taifa kila mwaka kutokana na ajali za barabarani hivyo lazima jitihada zichukuliwe kwa kasi zaidi."

Mkuu wa Wilaya ya Tanga, Hashim Mgandilwa, wakati anazindua mpango huo alisema, elimu itakayotolewa na shirika hilo, itawafanya wananchi wa wilaya hiyo waone umuhimu wa kulinda miundombinu ya barabara.

"Mradi huu umekuja wakati mwafaka, kwa sababu kwenye kila miradi ya ujenzi wa barabara inayofanywa na serikali, huenda sambamba na uwekaji alama za barabarani na wakati mwingine huwekwa mpaka kamera, lakini huripotiwa baadhi ya watu kuong'oa na kuiba baadhi ya vifaa vya usalama barabarani.

"Hapa Tanga tulikuwa na mradi wa kufunga taa za barabarani, lakini baadhi ya watu bila aibu wanapita na kuziiba. Kwa elimu itakayoanza kutolewa, tunaamini watazilinda hizo rasilimali."

Awali, Kaimu Mkuu wa Kikosi cha Usalama Barabarani, Mkoa wa Tanga, George Elihaki, alisema kwa kushirikiana na Shirika la Amend, wametoa elimu ya usalama barabarani kwa waendesha bodaboda 500.

# Walalamikia ukosefu huduma ya vipimo hospitalini

**Na Godfrey Mushi,** LONGIDO

KUKOSEKANA kwa baadhi ya huduma muhimu ikiwamo vipimo katika Hospitali ya Wilaya ya Longido, mkoani Arusha, kumezua manung'uniko kwa wakazi wa wilaya hiyo, huku wakiwatuhumu viongozi wao kushindwa kutafuta ufumbuzi wa kudumu wa tatizo hilo.

Hospitali hiyo iliyoanza kujengwa mwaka 2018, hadi sasa haina watumishi wa kutosha, vipimo na baadhi ya wodi, jambo linawasababishia wagonjwa hasara ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma hizo katika Jiji la Arusha na Wilaya jirani ya Siha.

Kwa nyakati tofauti, baadhi ya wakazi wa wilaya hiyo akiwamo Maiyasa Olekumbe, wameeleza masikitiko yao kuhusu mkwamo wa ukamilishaji wa majengo, kukosekana wataalamu na kusuasua kwa mradi huo kukamilika.

"Nikwenda hosptalini hapo kutafuta huduma kutokana na baadhi yake kutopatikana kwenye Kituo cha Afya cha Longido, lakini cha ajabu nimekosa huduma za matibabu kutokana na kutokamilika kwa majengo.

"Tangu saa 3:00 asubuhi mpaka sasa, hakuna kipimo chochote amefanyiwa mgonjwa wangu na nimeshatoa 40,000 za kuchangia huduma, bila kujua mgonjwa wangu anasumbuliwa na tatizo gani.

Aidha, Neema Laizer, mkazi wa Longido, alisema haoni sababu viongozi wasiwajibike kwa kushindwa kushughulikia tatizo hilo, kwa kuwa wanaoteseka ni wananchi hasa wanawake, wazee na watoto.

Alipoulizwa kuhusu mradi huo, Mwenyekiti wa Halmashauri ya Wilaya ya Longido, Simon Oitesoi, alisema ujenzi wa hospitali hiyo unasuasua, kwa kuwa kuna majengo ambayo hayajakamilika.

"Ni kweli bado huduma haziko sawa na kunahitajika jitihaa za makusudi kupata ufumbuzi wa tatizo hilo la kukosekana baadhi ya huduma. Tayari tumemaliza jengo la OPD (jengo la wagonjwa wa nje) na limeanza kufanya kazi.

"Hakuna ubishi kwamba kuna majengo yameanza kujengwa kutoka mwaka 2018, na mimi nimeyakuta. Hayo majengo yana upungufu na hayajakamilika mpaka leo hii. Ni majengo zaidi ya manne."

Kutokana na mkwamo huo, Oitesoi, alisema halmashauri hiyo imeamua kuchukua makusanyo ya ndani ili kuhakikisha majengo hayo yanakamilika na kuanza kutoa huduma kwa wananchi.

Akijibu malalamiko kuhusu kukosekana vipimo na baadhi ya huduma nyingine, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, Stephen Ulaya, alikiri kuwa hospitali hiyo inakabiliwa na upungufu wa watumishi wa huduma za mionzi (X-Ray),

Alisema wakati anasubiri wataalamu kutoka serikalini, ameamua kuchukua watumishi wawili wa idara ya afya na kuwapeleka kwenye mafunzo ya muda mfupi ili wakirejea wakatoe huduma za mionzi.



Mkazi wa Kijiji cha Kimanganuni kilichoko Kata ya Uru Kusini wilayani Moshi Vijijini, Livinus Mushi (kulia), akishirikiana na wageni wanaojitolea kutoka nchini Belgium kwenye ujenzi wa madarasa katika Shule ya Msingi Okaseni mwishoni mwa wiki. **PICHA: JAMES LANKA**

# Watafiti wakutana kujifunza njia za kidijitali upimaji afya

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WATAALAMU wa utafiti wa utambuzi na upimaji wa hali ya umaskini kutoka mataifa 27 duniani wamekutana jijini hapo, kujadili pamoja na mambo mengine, njia za kidijitali za upimaji umaskini, kwa kiwango kinacholingana katika nchi hizo.

Akizungumza wakati wa ufunguzi wa mkutano huo, Spika mstaafu wa Bunge, Anne Makinda, alisema kuwa kati ya watalamu hao, 13 wanatoka Bara la Afrika, Asia, Amerika na Ulaya.

"Tumekutana hapa (Arusha), kwa ajili ya kutazama namna gani tutakuja na takwimu na vipimo vinavyolingana kwa nchi zote masikini. Wataalamu wetu wanashauri kwamba kuna umuhimu kuwa na kipimo kimoja cha upimaji wa hali ya umasikini kinachoweza kulinganishwa.

"Wataalamu hawa hivi sasa watafanya utafiti wao katika kila taifa, kwa kuangalia ni kipimo gani ambacho kinaweza kutoa majibu yenye ulinganisho kwa nchi zinazoendelea na zilizoendelea."

Kwa mujibu wa Makinda, moja ya mambo yanayowaumiza kichwa kwa sasa ni watafiti hao kufanya kazi katika mazingira magumu.

"Mazingira hayo yanachagizwa na majanga mbalimbali, ikiwamo ukame na tishio la ugonjwa wa UVIKO-19. Kwa pamoja mambo hayo husababisha mazingira ya kufanya kazi hiyo kutofautiana kutoka nchi moja hadi nyingine."

Kabla ya ufunguzi huo, Mtakwimu Mkuu wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, Salum Kassim Alli, alisema mkutano huo umewajumuisha wataalamu wa takwimu na uchumi, kwa ajili ya kufanya uchambuzi na kutafsiri taarifa za kitakwimu zinazohusiana na masuala ya kipato cha mtu mmoja mmoja, familia na nchi kwa ujumla.

"Mkutano huu ulikuwa ufanyike miaka miwili iliyopita, lakini kutokana na tishio la ugonjwa wa UVIKO-19, haukuweza kufanyika. Washiriki wa mkutano wa sasa ni wabobezi wa kutambua na kuchambua taarifa za kipato cha mwananchi mmoja mmoja," alisisitiza.

Vilevile, alisema katika mkutano huo, watafiti hao watawasilisha mawasilisho ya kitaalam kuhusu upimaji wa hali ya umaskini yasiyopungua 20 na kujadiliwa.

Alisema kwa wataalamu kutoka Tanzania Bara na Visiwani, kupitia mkutano huo, watajengewa uwezo kwa kuwa waliotoka nje ya nchi ni wabobezi uchambuzi wa taarifa za kipato.

Kwa upande wake, Balozi Mohamed Haji Hamza, ambaye ni Kamisaa wa Sensa ya Watu na Makazi Zanzibar, alisema Tanzania imekuwa ikijitahidi kupambana na umaskini kwa kuwajengea uwezo wananchi na kuwatafutia fursa mbalimbali zilizoko ili kuongeza kipato chao.

"Umaskini hauwezi kuondolewa kwa kuwapa watu fedha, bali utaondolewa kwa kuwajengea uwezo, ikiwamo kuwapatia mikopo, kuwapa elimu na kuwatafutia masoko, ambayo yatawasaidia kuuza kidhaa zao," alieleza zaidi Balozi Mohamed.

# Nipashe Spotika



WACHEZAJI KIWANGO WA BRAZIL WALIOACHWA KOMBE LA DUNIA UK.16



## ISIKUPITE

Bingwa wa Kombe la Dunia atapokea kitita cha Sh. bilioni 97.8 za Tanzania, mshindi wa pili Sh. bilioni 93.1, wa tatu Sh. bilioni 62.8, wa nne Sh. bilioni 58.2, timu zitakazotinga robo fainali Sh. bilioni 39.5 kila moja na zitakazoingia hatua ya 16- bora Sh. bilioni 30.2.

## MTIFUANO...

Mshambuliaji wa Arsenal, Gabriel Jesus (kulia) na beki wa Wolverhampton Wanderers, Toti Gomes, wakiwania mpira kwa kichwa kwenye ya Ligi Kuu England iliyopigwa katika Uwanja wa Molineux juzi na Arsenal kuibuka na ushindi wa mabao 2-0. Ushindi huo unaifanya Arsenal kuelekea mapumziko ya kupisha Kombe la Dunia nchini Qatar 2022, ikiwa kileleni mwa msimamo wa Ligi Kuu kwa pointi 37, tano zaidi ya Manchester City iliyopo nafasi ya pili baada ya timu hizo kila moja kushuka dimbani mara 14. **PICHA: MTANDAO**

# MAKIPA WA4 WA VIWANGO ZAIDI LIGI TANO BORA ULAYA

**LONDON,** England

MAGOLIKIPA katika kila klabu ya soka ni muhimu sana na maonyesho yao ni kati ya vitu muhimu kwa timu.

**Msimu unaondelea wa 2022-23 kati ya ligi tano bora za Ulaya, kumekuwa na ushindani mkubwa na tumeshuhudia utendaji mzuri wa washindani mbalimbali wa mataji katika ligi zao za ndani.**

Wakati huohuo, ligi kadhaa za ndani kote barani Ulaya ziliingia kwenye mapumziko kutokana na mashindano yajayo ya Kombe la Dunia Qatar 2022.

Hadi sasa msimu huu, makipa kadhaa wamefanya vema, huku uchezaji wao ukiwa umefikisha pointi muhimu kwa timu zao.

Kwa maelezo haya, tuwatazame makipa wanne wanaofanya vizuri zaidi katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu, haya sasa...

**#4. IVAN PROVEDEL - LAZIO**

Ivan Provedel amekuwa katika kiwango cha hali ya juu msimu huu, huku uchezaji wake ukiwa umeisaidia sana Lazio.

Muitaliano huyo ameruhusu mabao nane pekee, huku akicheza mechi nane bila kuruhusu bao kati ya 13 za Serie A. Zaidi ya hayo, alicheza mechi moja bila kuruhusu bao katika mechi sita za hatua ya makundi ya Ligi ya Europa.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 28 kwa sasa, ndiye mlinda mlango aliye na idadi kubwa ya pasi safi kwenye Serie A msimu huu na anabakia kuwa kiungo muhimu kwa kikosi cha Lazio.

**#3. MARC-ANDRE TER STEGEN - BARCELONA**

Kiwango cha Marc-Andre ter Stegen kimekuwa kikubwa katika goli la Barcelona msimu huu.

Ameruhusu mabao manne pekee na amecheza bila kuruhusu bao katika mechi 11 kati ya mechi 13 za LaLiga kwenye msimu huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ujerumani alifungwa katika mechi tano za Ligi ya Mabingwa Ulaya huku Barca wakitolewa katika hatua ya makundi. Lakini uchezaji wake bora kwenye LaLiga unahalalisha kujumuishwa kwake kwenye orodha hiyo.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, hajaruhusu bao lolote katika mechi saba zilizopita kwenye Uwanja wa Camp Nou na bado ni mchezaji muhimu kwenye goli la Barcelona.

**#2. EDERSON MORAES - MANCHESTER CITY**

Mbrazil huyo bila shaka ni mmoja wa makipa waliofanya vizuri zaidi katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu. Uwapo wake langoni umekuwa muhimu sana kwa Manchester City.

Ederson ameruhusu mabao 14 na amecheza bila kuruhusu bao katika mechi sita kati ya 13 za Ligi Kuu. Zaidi ya hayo, alicheza mechi nne bila kurushu bao katika mechi nne za Ligi ya Mabingwa Ulaya.

Kwa kuzingatia kiwango chake cha kuvutia katika mashindano yote, anaweza kushiriki katika goli la Brazil mbele ya Alisson Becker kwenye Kombe la Dunia nchini Qatar.

**#1. MARK FLEKKEN - SC FREIBURG**

Mholanzi huyo amekuwa kipa bora zaidi katika ligi tano bora za Ulaya msimu huu, huku kiwango chake kikiwa cha muhimu kwa Freiburg.

Mark Flekken ameruhusu mabao 13 na amecheza bila kufungwa katika mechi nane kati ya 13 za Ligi Kuu Ujerumani, Bundesliga, kwenye msimu unaoendelea.

Kipa huyo mwenye umri wa miaka 29, amekuwa na mchango mkubwa nyuma ya Freiburg ambayo kwa sasa inakamata nafasi ya pili kwenye msimamo wa Bundesliga. Pia ameokoa penalti tatu kwenye Ligi ya Europa.



MARK FLEKKEN

MICHEZO

# FETTY DENSA: CAF IMETUFUNGULIA NJIA KUCHEZA ULAYA




**Na Somoe Ng'itu,** RABAT

NEEMA na safari ya mafanikio kwa wachezaji wa Simba Queens kwenda kucheza soka la kulipwa nje ya Tanzania inatarajiwa kuanza baada ya mawakala waliokuwa wakifuatilia fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake kuvutiwa na nyota kadhaa wa kikosi hicho.

**Mmoja wa nyota hao ni beki kisiki na tegemeo, Fatuma Issa 'Fetty Densa', ambaye kiwango chake alichokionyesha katika fainali hizi zilizomalizika jana usiku kimewavutia makocha wa Mamelodi Sundowns Ladies ya Afrika Kusini na wameahidi kufanya mazungumzo na mabosi wa 'Wekundu wa Msimbazi', kwa ajili ya kumnasa mchezaji huyo 'kiraka'.**

Mkuu wa Idara ya Ufundi wa Klabu ya Mamelodi Sundowns, Shawn Bishop, amemwambia mwandishi wetu katika mahojiano maalum kuwa Fetty Densa ameonyesha uwezo mkubwa katika mechi zote alizocheza na wanatamani kumsajili akaongeze nguvu katika kikosi chao.

Bishop alisema beki huyo ana uzoefu mkubwa na wanafahamu kutokana na kushiriki mashindano ya COSAFA akiwa katika kikosi cha Timu ya Soka ya Taifa ya Wanawake (Twiga Stars), ambacho kimeshinda mataji mbalimbali au kufika fainali kwenye michuano ya ukanda huo kila wanapoalikwa, anaweza kuisaidia sana timu yako.

Kiongozi huyo alisema ofisini yake pia imevutiwa na Mghana, Philomena Abakah na mara watakaporejea kwao wataanza mazungumzo rasmi na viongozi wa Simba Queens.

"Mna wachezaji wazuri, mna timu nzuri sana, niwe mkweli hata kama mmepoteza mechi ya leo (juzi), yule anayevaa jezi namba tano (Fetty Densa) na jezi namba sita (Philomena Abakah), ni wazuri sana," alisema mkufunzi huyo.

**FETTY DENSA AFURAHIA OFA SAUZI**

Beki huyo wa zamani wa Evergreen Queens ya Temeke, Dar es Salaam, kwa upande wake anasema amefuatwa na Kocha Mkuu wa Mamelodi Sundowns Ladies, Jerry Tshabalala, na kumweleza wakati umefika kwenda kujiunga na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Wanawake Afrika Kusini.

Densa anasema amefurahi kusikia kauli ya viongozi hao wa Mamelodi Sundowns Ladies na kuongeza pia anatakiwa na klabu nyingine ya Ulaya, ingawa wakala aliyefikisha salamu hakutaja jina lake.

"Nimeambiwa kuna timu zaidi ya moja inatuhitaji wachezaji wa Simba Queens, ni jambo la faraja kwetu kwa sababu ndoto ya kila mchezaji ni kucheza soka la kulipwa au kusonga mbele," alisema beki huyo.

Aliongeza kuwa Kocha Tshabalala alimweleza licha ya timu yake kuwafunga, lakini Simba Queens iliwapa wakati mgumu na hata wangewavua ubingwa, isingekuwa bahati mbaya bali ni kwa uwezo waliokuwa nao.

"Kama timu malengo yetu katika mashindano haya ya CAF (Shirikisho la Soka Afrika), yalikuwa ni kufika nusu fainali, tunashukuru Mungu tumefika, na tulikuwa pia na nafasi ya kufanya vizuri zaidi lakini hatukuwa na bahati hiyo, waamuzi hawakuwa upande wetu, lakini tulifahamu yatafuatiliwa na mawakala, hivyo kila mmoja alikuwa akijituma kuonyesha kiwango chake ili kuzivutia timu nyingine," Densa aliongeza.

**BARBARA AFUNGUKA**

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, amesema sera na misingi ya klabu hiyo siku zote ni kusimamia maslahi ya mchezaji na si jambo lingine tofauti.

Kiongozi huyo ambaye alishuhudia mechi ya hatua ya nusu fainali ambapo timu yake ilifungwa bao 1-0 na Mamelodi Sundowns Ladies, ambao walikuwa mabingwa watetezi, alisema amepata taarifa za awali za nyota wake kutakiwa na klabu mbalimbali za Morocco na nchi nyingine.

Alisema milango ya Simba kufanya mazungumzo na timu yoyote iko wazi kwa sababu inathamini vipaji vya wachezaji wake na inajua kila mmoja anahitaji kutimiza ndoto zake.

"Tuko tayari kuruhusu mchezaji ambaye atapata ofa nzuri, tunazingatia sana maslahi ya mchezaji na si kumuuza tu, haitakuwa busara kumuuza mchezaji kwa klabu ambayo itamlipa mshahara mdogo kuliko anaopata hapa Simba, haitaleta maana kwake na kwetu pia," alisema Barbara.

Naye Meneja wa Simba Queens, Selemani Makanya, amesema, binafsi kwake anaona wakati wa Fetty Densa kwenda kucheza soka nje ya Tanzania umefika na endapo mchakato huo utatimia kwa beki huyo anamtakia kila la kheri.

"Mimi pia nimeulizwa kuhusu Fetty, kwangu kwa roho safi ninamtakia kila la kheri, sina deni naye, kwa umri wake kumzuia kuondoka kwa sasa haitakuwa vema, tutamruhusu akacheze," alisema Makanya.

Aliongeza anafurahi kuona wachezaji wa Simba Queens wamekuwa gumzo katika michuano hiyo na anaamini mwakani endapo watapata tiketi ya kushiriki fainali hizo, watakuja wakiwa imara zaidi.

"Tumejifunza vitu mbalimbali, tunarudi nyumbani tukiwa na vitu vya kwenda kuvifanyia kazi, heshima tumeweka na historia tumeiandika," Makanya aliongeza.

Simba Queens imemaliza fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake katika nafasi ya nne baada ya kukubali kichapo cha bao 1-0 kutoka kwa Bayelsa Queens FC ya Nigeria katika mechi ya kutafuta mshindi wa tatu iliyochezwa kwenye Uwanja wa Prince Heritier Moulay El Hassan juzi usiku.

Fainali za michuano hiyo inayodhaminiwa na UMBRO na Tiktok ambapo bingwa atapata zawadi ya Dola za Marekani 400,000 huku mshindi wa pili akiondoka na Dola za Marekani 250,000 zilifanyika jana usiku kwa kuwakutanisha wenyeji, ASFAR FC dhidi ya Mamelodi Sundowns Ladies.

Simba Queens na Bayelsa Queens kila moja atapokea zawadi ya Dola za Marekani 200,000 wakati Green Buffalo ya Zambia na TP Mazmbe ya Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) zenyewe zimepata Dola za Marekani 150,000 huku Wadi Degla ya Misri na Determine Girls kutoka Liberia kila moja akiondoka na kifuta jasho cha Dola za Marekani 100,000 kwa kushiriki fainali hizo.

**NJE YA UWANJA**

HADI Gerard Pique anaamua kutundika daluga wiki iliyopita, kwa ujumla katika wasifu wake kisoka amecheza chini ya makocha 12, akishuka dimbani mara 667 na kufunga mabao 68, pasi za mwisho 14, kadi za njano 165 na nyekundu tano huku akishinda makombe 34 akiichezea Manchester United na Barcelona.



# WACHEZAJI KIWANGO WA BRAZIL WALIOACHWA KOMBE LA DUNIA

**DOHA,** Qatar

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Brazil, Tite, amewapa mashabiki wa soka mwonekano wa kwanza wa kikosi cha 'Selecao' hao kitakachoshiriki Kombe la Dunia la FIFA 2022 nchini Qatar. Huku mashindano hayo yakiwa yamebakiza wiki moja pekee kabla ya kuanza, makocha wa timu za taifa wameanza kutoa orodha yao ya mwisho ya kikosi cha wachezaji 26.

**Brazil ni miongoni mwa wanaopewa nafasi kubwa ya kuibuka mabingwa wa dunia kwa mara ya kwanza tangu 2002. Wana kikosi chenye vipaji vya ajabu kinachoongozwa na nyota wa Paris Saint-Germain, Neymar Jr.**

Selecao wameshinda Kombe la Dunia la FIFA mara tano na watakuwa wakitafuta kupanua rekodi yao huko Qatar msimu huu. Kocha Tite ana mchanganyiko mzuri wa vijana na uzoefu wa kuchagua kwa ajili ya mashindano.

Kwa kuzingatia ubora, wababe hao wa Amerika Kusini, baadhi ya wachezaji bora wameachwa kwenye kikosi chao cha wachezaji 26 kwa ajili ya Kombe la Dunia la FIFA la 2022.

Bila kuchelewa, hii hapa ni orodha ya wachezaji watano bora waliokosa kujumuishwa katika kikosi cha Brazil kitakachoshiriki Kombe la Dunia nchini Qatar...

### #5. MATHEUS CUNHA

Mshambuliaji wa Atletico Madrid, Matheus Cunha alikuwa mmoja wa mastraika waliotajwa sana wakati alipohamia Ulaya akiwa kijana. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 23, ameona muda wake umekuwa mdogo kwani ameshindwa kuendana na mbwembwe alizofika nazo.

Cunha ameondolewa kwenye kikosi cha Kombe la Dunia baada ya kuwa na wakati mgumu hadi sasa akiwa na Atletico Madrid. Bado hajafunga bao lolote katika mechi 16 alizowachezea Wahispania hao msimu huu na ana pasi mbili pekee za mabao kwa jina lake.

Cunha aliachwa nje ya kikosi cha Selecao kwenye Copa America 2021. Hatakuwapo Qatar kwa Kombe la Dunia pia, huku Tite akichukuwa wachezaji ambao wameanza msimu wakiwa katika kiwango bora zaidi.

Cunha ameichezea Brazil mechi nane katika maisha yake ya soka, huku mechi ya mwisho akicheza mechi ya kirafiki dhidi ya Ghana, Septemba 2022. Mchezaji huyo wa zamani wa RB Leipzig bado hajaiwakilisha nchi yake katika michuano ya wakubwa, huku mechi zake zote za awali akicheza za kufuzu na kirafiki.

### #4. GABRIEL BARBOSA

Mshambuliaji mwingine aliyekosa orodha ya Selecao kwa Kombe la Dunia la FIFA la 2022 ni Gabriel "Gabigol" Barbosa. Mshambuliaji huyo wa Flamengo ni mmoja wa wachezaji motomoto zaidi kwenye Ligi Kuu Brazil, Serie A na ameshangaa kukosa orodha hiyo.

Baada ya kuvumilia kipindi kibaya huko Ulaya akiwa na Inter Milan na Benfica, 'Gabigol' ameibuka tena kuwa mmoja wa wachezaji bora zaidi nchini Brazil. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, alifunga katika fainali ya Copa Libertadores (Ligi ya Mabingwa Amerika Kusini) wiki chache zilizopita huku Flamengo ikitwaa taji hilo.

Gabigol ameichezea nchi yake mara 18, zikiwamo Copa America 2021 na Copa America Centenario mwaka 2016. Mechi yake ya mwisho kuichezea Brazil ilikuwa Januari 2022. Ana mabao matano kwa Selecao na atakosa nafasi ya kuichezea Brazil.

### #3. DOUGLAS LUIZ

Kiungo wa kati wa Aston Villa, Douglas Luiz ameachwa nje ya kikosi kitakachoshiriki Kombe la Dunia la FIFA 2022 na Tite. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, amekuwa akifanya vema kwenye Ligi Kuu England akiwa na Villa tangu ajiunge nayo akitokea Manchester City.

Luiz amekuwa katika kiwango cha kuvutia katika klabu yake hiyo ya England kwa mwaka huu 2022, na alikuwa karibu sana kujiunga na Arsenal katika dirisha la usajili la majira ya joto. Kiungo huyo wa kati wa safu ya ulinzi ameichezea Aston Villa mara 14 katika mashindano yote msimu huu na ana mabao mawili, yote ya kuvutia kutokana na mipira ya kona ya moja kwa moja.

Lakini yeye na Villa wamekuwa na msimu usio wa kuvutia sana hadi sasa na pengine hiyo ndio sababu ya kutemwa kwenye kikosi cha Brazil.

Luiz ameichezea Selecao mara tisa katika maisha yake ya soka na kushiriki katika Copa America ya 2021. Mara yake ya mwisho kuichezea nchi yake ilikuwa Oktoba 2021 katika mechi ya kufuzu Kombe la Dunia.

### #2. GABRIEL MAGALHAES

Beki wa Arsenal, Gabriel Magalhaes amekuwa mmoja wa wachezaji bora wa kikosi chake kwenye Ligi Kuu England msimu huu.

Hata hivyo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, aliondolewa kwenye kikosi cha Brazil kwa ajili ya Kombe la Dunia la FIFA 2022 licha ya kuonyesha kiwango kizuri katika ngazi ya klabu. Ni miongoni mwa majina ya watu mashuhuri waliokosa nafasi ya kushiriki Kombe la Dunia mwaka huu.

Magalhaes ameunda ushirikiano mzuri wa ulinzi na William Saliba katika Klabu ya Arsenal. Ameichezea klabu yake mara 18 katika michuano yote na ameisaidia timu hiyo kufika kileleni mwa jedwali la Ligi Kuu na Ligi ya Europa. Beki huyo wa Brazil pia ana mabao mawili kwa jina lake msimu huu.

Magalhaes bado anasubiri kuonekana kwake kwa mara ya kwanza katika ngazi ya juu kwa nchi yake. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 24, alikosa Olimpiki ya 2020 kutokana na jeraha na amepuuzwa tena kwenye uteuzi.

### #1. ROBERTO FIRMINO

Mshambuliaji wa Liverpool, Roberto Firmino, huenda ndiye mchezaji aliyeshangaza zaidi kuachwa kwenye kikosi cha Brazil kitakachoshiriki Kombe la Dunia la FIFA. Fowadi huyo mwenye umri wa miaka 31, amefurahia mwanzo mzuri wa msimu wa 2022-23 akiwa na timu hiyo ya England.

Firmino amejitambulisha tena kama mchezaji muhimu wa Jurgen Klopp katika klabu ya Liverpool msimu huu baada ya kukosa kwenye msimu wa 2021-22. Fowadi huyo ana mabao sita na asisti tatu katika mechi 12 za Ligi Kuu kwa 'Wekundu' hao msimu huu.

Firmino amekuwa akiichezea nchi yake mara kwa mara tangu mwaka 2014 na amecheza katika mashindano makubwa manne kwa Selecao. Ana mabao 17 na asisti saba katika mechi 55 alizoichezea nchi yake, na alikuwa mshiriki wa kikosi kilichoshinda Copa America 2019.

### KIKOSI CHA WACHEZAJI 26 WA BRAZIL WA KOMBE LA DUNIA LA FIFA 2022:

Alisson Becker, Ederson Moraes, Weverton, Dani Alves, Danilo, Alex Sandro, Alex Telles, Gleison Bremer, Eder Militao, Marquinhos, Thiago Silva, Bruno Guimaraes, Casemiro, Everton Ribeiro, Fabinho , Fred, Lucas Paqueta, Antony, Gabriel Jesus, Gabriel Martinelli, Neymar, Pedro, Raphinha, Richarlison, Rodrygo na Vinicius Jr.



ROBERTO FIRMINO

## Nukuu

"Ilikuwa [PSG] uzoefu tuliohitaji, uzoefu wa kuishi na nyota wakubwa na kuchangamana katika ngazi ya juu ya soka. Ilikuwa changamoto ya kujiweka katika hali ngumu na kujaribu kuifanya klabu maalum kufanya kazi. Unahitaji kuzoea kila mara kwa sababu kulikuwa na ukuu mwingi. Kwa Barca kuwa na Messi au kwa Madrid kuwa na Cristiano ni baraka. Lakini unapoweka wachezaji wengi ambao wote wanahitaji nafasi yao na kuwa namba moja, kunaweza kutokea mkanganyiko," **Kocha wa zamani wa Paris Saint-Germain, Mauricio Pochettino akikiri kuwa kuongoza mastaa kama Lionel Messi, Neymar, na Kylian Mbappe ilikuwa ni kazi ngumu.**



Ukiangalia mechi zetu anatumika, Moses Phiri na anafanya vizuri sana kwenye nafasi hiyo [mshambuliaji wa kati], lakini kiasili eneo ambalo amekuwa akicheza ni nyuma ya mshambuliaji, lazima tulete straika katika usajili wa dirisha dogo," **Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda.**



"Sijazungumza na Joao kuhusu hilo, alizingatia sana mambo ambayo tulikuwa tunaifanyia Arsenal ya kesho. Yeye ni mtaalamu sana, nina hakika atatafakari juu ya kutochaguliwa na atasikitishwa na Ronaldo kwenda [Kombe la Dunia Qatar] umri huo. Kocha anapaswa kufikiria juu ya uwiano wa kikosi, ni muhimu kwa kocha yeyote, hivyo labda hiyo ilikuwa sehemu ya uamuzi," **Kocha wa Mpito wa Wolverhampton Wanderers, Steve Davis, akishangazwa na Kocha Mkuu wa Ureno, Fernando Santos, kumjumuisha Straika wa Manchester United, Cristiano Ronaldo katika kikosi chake cha Kombe la Dunia 2022.**





Beki wa pembeni wa Yanga, Kibwana Shomari, akimiliki mpira dhidi ya straika wa Club Africain kwenye mechi ya mchujo, Kombe la Shirikisho Afrika iliyopigwa Tunisia na Yanga kushinda bao 1-0. **PICHA: YANGA**

# NI MWAKA WA YANGA KUZIKA MZIMU REKODI MBAYA MAKUNDI CAF?

**Na Adam Fungamwango**

JUMATANO iliyopita timu ya Yanga iliwashtusha mashabiki wa soka Afrika ilipofanikiwa kutinga kibabe hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika kwa kuifunga bao 1-0 Club Africain ya Tunisia kwao kwenye Uwanja wa Olympique Hamad Agrebi.

**Hii ni baada ya kutoka suluhu kwenye mechi ya kwanza iliyopigwa Uwanja wa Benjamin Mkapa, Novemba 2, mwaka huu. Yanga imefanikiwa kuingia kwenye hatua hiyo kwa mara ya kwanza baada ya miaka minne.**

Rekodi zinaonyesha kuwa pamoja na timu hiyo kushindwa kuingia makundi kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika kwa miaka 24 tangu 1998, lakini kwao huwa si vigumu sana kutinga hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho.

Kwa misimu saba sasa, timu hiyo imetinga hatua hiyo mara tatu, mara ya mwisho ikiwa ni 2018. Mara ya kwanza Yanga ilikuwa ni mwaka 2016 na mara zote hizo ilikuwa imetoka kutolewa kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika.

Katika makala haya tunakuletea rekodi za safari ya Yanga kwenye makundi Afrika Kombe la Shirikisho na kufanikiwa kutinga mara zote hizo...

**SAFARI YA MAKUNDI 2016**

Kama ilivyoandikwa juu mara zote tatu Yanga haikuanzia moja kwa moja Kombe la Shirikisho, badala yake ilikuwa inatolewa kwenye Ligi ya Mabingwa na kuangulia kombe hilo.

Mwaka 2016 ilitolewa kwenye Ligi ya Mabingwa na timu ya Al Ahly ya Misri. Kwenye mechi ya kwanza nchini timu hizo zilitoka sare ya bao 1-1, lakini marudiano nchini Misri, Yanga ilichapwa mabao 2-1, ikaangukia kwenye Kombe la Shirikisho hatua ya mchujo.

Ikacheza na Sagrada Esperanca ya Angola na kuifunga jumla ya mabao 2-1, ikishinda 2-0 nyumbani na kufungwa bao 1-0 ugenini, hivyo kutinga hatua ya makundi kwa mara ya kwanza.

Katika makundi ikapangwa Kundi A na timu za TP Mazembe ya DR Congo, Mo Bejaia ya Algeria na Medeama ya Ghana. Ilimaliza nafasi ya mwisho ikiwa na pointi nne.

**SAFARI YA MAKUNDI 2018**

Mwaka 2018 kama kawaida ilianza kwenye Ligi ya Mabingwa Afrika, lakini ikatolewa na timu ya Township Rollers ya Botswana kwa jumla ya mahao 2-1. Yanga ilifungwa nyumbani mabao 2-1, kabla ya kwenda kusuluhu ugenini.

Ikatupwa kwenye Kombe la Shirikisho na kucheza dhidi ya Welayta Dicha ya Ethiopia. Kwenye mechi ya kwanza nchini, ilishinda mabao 2-0, lakini ilikwenda kupoteza ugenini bao 1-0. Kwa matokeo hayo ikatinga kwa mara ya pili hatua ya makundi Kombe la Shirikisho kwa jumla ya mabao 2-1.

Kwenye hatua ya makundi ilipangwa Kundi D na USM Alger ya Algeria, Rayon Sports ya Rwanda, na Gor Mahia ya Kenya, na kwa mara nyingine tena ilishika mkia kwenye kundi hilo na pointi zake nne.

**SAFARI YA MAKUNDI 2022**

Ilianza safari yake kwenye Ligi ya Mabingwa msimu huu na kutolewa na Al Hilal ya Sudan. Katika mechi ya kwanza Uwanja wa Benjamin Mkapa, Dar es Salaam, Yanga ililazimishwa sare ya bao 1-1, na kwenda kudunguliwa bao 1-0 jijini Khartoum.

Ni matokeo ambayo yaliiondoka kwenye Ligi ya Mabingwa na kuangukia Kombe la Shirikisho, ikipangwa kucheza dhidi ya Club Africain ya Tunisia.

Mechi ya kwanza ililazimishwa suluhu nyumbani, lakini kwenye mechi ya marudiano, Yanga 'ilipindua meza' na kushinda bao 1-0. Ushindi huo ikiipa tiketi ya kufuzu hatua ya makundi ikiwa ni mara ya tatu sasa kwenye historia ya klabu hiyo katika hatua hiyo, lakini pia inafanya hivyo ndani ya miaka saba.


Droo ya CAF kupanga hatua ya makundi inatarajiwa kuchezeshwa keshokutwa, Jumatano wiki hiiili kujua safari hii itapangwa kundi lipi na timu gani kwenye kombe hilo, huku mashabiki wa timu hiyo wakisubiri kuona kama inaweza kumaliza mzimu unaoitafuna katika hatua ya makundi kwa kumaliza ya mwisho.

**NDANI YA 18**



HADI kumalizika kwa hatua ya makundi ya Ligi ya Mabingwa Ulaya, Kylian Mbappe (PSG) na Mohamed Salah (Liverpool), ndio wanaongoza kwa kufunga mabao mengi kila mmoja akicheka na nyavu mara saba wakifuatiwa na Erling Haaland (Man City), Mehdi Taremi (Porto) na Robert Lewandowski (Barca) wenye mabao matano kila mmoja.

# SOKA



## MKALI WA WIKI

**JINA KAMILI:** Philip Walter Foden
**KUZALIWA:** Mei 28, 2000 (umri miaka 22)
**ALIPOZALIWA:** Stockport, England
**KIMO:** 5 ft 7 in (1.71 m)
**NAFASI:** Winga
**KLABU:** Manchester City
**JEZI NAMBA:** 47

**HADI SASA MSIMU HUU 2022/23**
Kacheza mechi: 13
**Alizoanza:** 10
**Dakika:** 810
**Mabao:** 7
**Asisti:** 3
**Kimahesabu**
Anafunga ama kutoa pasi ya mwisho kila baada ya dakika 81

KOCHA wa Timu ya Taifa ya Brazil, Tite, amewapa mashabiki wa soka mwonekano wa kwanza wa kikosi cha 'Selecao' hao kitakachoshiriki Kombe la Dunia la FIFA 2022 nchini Qatar. Huku mashindano hayo yakiwa yamebakiza wiki moja pekee kabla ya kuanza, makocha wa timu za taifa wameanza kutoa orodha yao ya mwisho ya kikosi cha wachezaji 26.

**Uk. 16-17**



N'GOLO KANTE

# SABABU 4 KWA NINI CHELSEA INAWEZA KUKOSA NNE BORA

**LONDON,** England

CHELSEA ilikutana na kichapo cha nyumbani dhidi ya Arsenal Jumapili ya Novemba 6, mwaka huu kwa kupigwa bao 1-0.

**Bao la Gabriel Magalhaes la dakika ya 63 kutokana na mpira wa kona, lilitosha kuwapa 'The Blues' hao vipigo mfululizo vya Ligi Kuu England chini ya kocha Graham Potter.**

Klabu hiyo ya London Magharibi ilionekana kuwa duni kwa wapinzani wao Arsenal, huku timu ya Mikel Arteta ikidhihirisha kwa mara nyingine kuwa washindani wakubwa wa taji msimu huu, lakini kwa bahati mbaya tena 'The Blues' hao juzi ugenini dhidi ya Newcastle United wakapigwa tena bao 1-0.

Kipigo hicho kwa sasa kinaiacha Chelsea katika nafasi ya nane baada ya michezo 14. 'The Blues' hao pia wako pointi 16 nyuma ya vinara wa ligi Arsenal na nane nyuma ya Tottenham Hotspur walio katika nafasi ya nne.

Tayari kuna wasiwasi juu ya The Blue hao kukosa kushiriki Ligi ya Mabingwa Ulaya msimu ujao kutokana na kiwango chao cha sasa.

Makala haya inaangalia sababu nne zinazoweza kuifanya timu hiyo ya Potter kushindwa kumaliza kwenye nne bora msimu huu, hizi hapa...

**#4. MAJERUHI**

Wakati majeraha ni sehemu ya soka kutokana na umbile la mchezo huo, bado linaathiri sana maandalizi na mwenendo wa timu.

Hii inaweza kusemwa kuhusu Chelsea msimu huu, kwani wachezaji kadhaa wa kikosi cha kwanza wamekumbwa na majeraha katika wiki za hivi karibuni. The Blues hao kwa sasa hawana wachezaji kama Reece James, N'Golo Kante, Ben Chilwell, Kepa Arrizabalaga, na Wesley Fofafa kutokana na majeraha.

Wachezaji wote watano ambao kwa sasa hawapo kwa sababu ya majeraha ya muda mrefu ni sehemu muhimu ya kikosi cha kwanza cha The Blues na pengo lake linaonekana wazi.

Iwapo klabu hiyo ya London Magharibi itaendelea kupoteza wachezaji wengi wa kikosi cha kwanza kutokana na majeraha, inaweza kuhatarisha nafasi yake ya kumaliza katika nafasi nne za juu. Kumbuka kwamba Chelsea walipata hali kama hiyo msimu uliopita walipompoteza nyota wao kama James na Chilwell.

**#3. KIWANGO KIBOVU DHIDI YA SITA BORA**

Hadi sasa msimu huu, Chelsea haijaonekana kushawishi dhidi ya klabu yoyote ya juu ya Ligi Kuu England ambayo wamekutana nayo.

Hawajapata ushindi wowote dhidi ya timu yoyote ya sasa katika sita bora msimu huu. Kumbuka Chelsea ilitoka sare dhidi ya Spurs (2-2) na Manchester United (1-1).

Pia walipoteza ugenini kwa Brighton, ambao wako nafasi ya sita (4-1), na kudondosha pointi tatu nyumbani dhidi ya Arsenal (1-0) kabla ya juzi kupigwa tena 1-0 dhidi ya Newcastle United iliyoko nafasi ya tatu kwenye msimamo wa ligi hiyo.

Kiwango chao duni cha nyumbani dhidi ya timu kubwa kinaweza kuwa pigo kubwa katika harakati zao za kufuzu kwa hatua ya nne bora. Wakiwa wamevuna pointi mbili pekee nyumbani dhidi ya timu za juu kwenye ligi msimu huu.

**#2. UKOSEFU WA MABAO**

Sababu nyingine kwa nini Chelsea wanaweza kukosa kufuzu katika nafasi nne za juu msimu huu ni kiwango chao duni cha mabao mbele ya lango.

Ingawa The Blues wamekuwa imara katika safu ya ulinzi msimu huu, hasa chini ya Potter, mashambulizi yao yameonekana kuwa butu.

Klabu hiyo ya London Magharibi hadi sasa imefunga mabao 17 ya Ligi Kuu msimu huu na kuruhusu 17. Hii inawafanya kuwa timu iliyofunga mabao machache zaidi kati ya klabu tisa bora kwenye ligi kwa sasa.

Timu zenye viwango vya chini kama vile Fulham (23), Brentford (23), na hata Leeds United (22) zimefunga mabao mengi zaidi ya The Blues msimu huu.

**#1. USAJILI WA JANUARI**

Dirisha la usajili la majira ya baridi la Januari linaweza kuwa fursa nyingine kwa The Blues kuimarisha kikosi chao litakapofunguliwa.

Nafasi kadhaa katika timu ya Chelsea ni wazi zinahitaji uimarishaji. Jinsi watakavyoitikia Januari inaweza kuongeza nafasi ya kumaliza msimu kwa kiwango cha juu.

Klabu hiyo ya London Magharibi inahitaji mlinzi wa kumsaidia beki wa kulia James, huku Azpilicueta akiwa hayupo kwenye kiwango kabisa.

"Chelsea itatafuta nafasi ya kuleta kiungo Januari. Kuna hitaji la wazi katika safu ya kati na sasa wanajua kwamba Kanté atakuwa nje kwa miezi michache zaidi."

Klabu hiyo pia haina mchezaji mbunifu na kiungo anayeshinda mpira ili kuongeza utulivu kwenye safu yao ya kiungo. Kukosekana kwa Kante kumeacha ombwe kubwa kwenye safu ya kiungo ya The Blues msimu huu. Hivyo wakifanya vibaya kwenye usajili wa dirisha dogo la Januari, itakuwa sababu nyingine ya kushindwa kumaliza kwenye nne bora.

**JE, WAJUA?**



KATIKA Ligi Kuu ya England, Miguel Almirón wa Newcastle United ndiye mchezaji wa nafasi ya kiungo anayeongoza kwa kufunga mabao mengi hadi sasa akiwa amecheka na nyavu mara nane akifuatiwa na James Maddison – (Leicester City – 6), Phil Foden (Man City – 6) na Pascal Groß (Brighton – 5).



# Mahakama yaendelea kusikiliza ushahidi kesi ya ulawiti

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

KESI ya unajisi inayomkabili Daniel Mchone (23), mfanyabiashara na mkazi wa Ilemi jijini Mbeya, imeendelea kusikilizwa katika Mahakama ya Wilaya ya Mbeya, baada ya upande wa Jamhuri kuwasilisha ushahidi wake kuhusu tuhuma za kijana huyo kumlawiti mtoto wa kiume mwenye umri wa miaka 10 mwanafunzi wa darasa la kwanza katika shule moja jijini humo.

Kesi hiyo ya jinai ilianza kusikiliwa juzi mbele ya Hakimu Mkazi Wilaya ya Mbeya, Paul Rupia, ambapo tayari upande wa Jamhuri umewasilisha vielelezo ili kuthibitisha tuhuma hizo.

Akitoa ushahidi wake mahakamani hapo mtoto huyo (jina limehifadhiwa), alidai anamfahamu mshtakiwa kwa kuwa miaka miwili iliyopita walikuwa majirani na Oktoba 10, 2022 majira ya saa sita mchana alikutana na mshtakiwa wakati akirudi kutoka shuleni na kumwita na kumchukua kisha kumzungusha maeneo kadhaa eneo la Ilemi hadi kwenye pagale moja alikotekeleza tukio hilo.

Alidai kijana huyo mfanyabiashara mdogo alimsihi asipige kelele na kumwingilia kinyume cha maumbile na baada ya kumaliza azma yake hiyo aliondoka na mtoto huyo aliamua kwenda kusema nyumbani kwao.

Kwa mujibu wa sheria madai hayo ni kinyume na kifungu namba 154 (1) na (2) a cha Sheria ya Kanuni za Adhabu Sura ya 16 kilichofanyiwa marekebisho mwaka 2022.

Baada ya ushahidi huo wa serikali kutoka kwa mwathiriwa, mwendesha mashtaka wa serikali wakili Davice Msanga, aliiomba mahakama kuahirisha shauri hilo hadi tarehe nyingine kwa ajili ya kuendelea na uwasilishaji ushahidi wao.

Hakimu Mkazi katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Mfawidhi wilayani Mbeya, Paul Rupia, aliahirisha kesi hiyo hadi Novemba 17 na mshtakiwa alirudishwa mahabusu baada ya kukosa mtu wa kumwekea dhamana.

# Tani 21.7 mbegu ya alizeti kusambaziwa wakulima

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

TANI 21.7 za mbegu ya alizeti, zinatarajiwa kusambazwa kwa wakulima wa mikoa ya Nyanda za Juu Kusini kukabiliana na tatizo la uhaba wa mbegu hizo nchini na kuwawezesha wakulima hao kulima kwa wakati.

Kati ya hizo tani 18 zimechukuliwa na Wakala wa Mbegu wa Serikali (ASA) kwa ajili ya kuwauzia wakulima kwa bei nafuu ya Sh. 3,000 kwa kilo moja.

Kaimu Meneja wa Kampuni ya Highland Seed Growers Limited, iliyopo mkoani Mbeya, Elizabeth Mallya, alitoa maelezo hayo mwishoni mwa wiki wakati wa ziara kuangalia hatua iliyofikiwa katika uzalishaji wa mbegu za alizeti iliyoandaliwa na Taasisi ya Uboreshaji wa Mifumo ya Masoko ya Kilimo nchini (AMDT) kwa kushirikiana na Taasisi ya Utafiti wa Kilimo nchini (TARI), Kituo cha Ilonga kilichoko mkoani Morogoro.

Katika kutatua tatizo la upatikanaji wa mbegu bora za mazao nchini AMDT, TARI na Taasisi ya Udhibiti wa Ubora wa Mbegu nchini (TOSCI) pamoja na kampuni ya uzalishaji wa mbegu, Mtaalamu wa Masoko kutoka AMDT, Clarence Chitemi, alisema wanatekeleza mradi wa upatikanaji wa mbegu bora za alizeti nchini.

Chitemi alisema mradi huo unatekelezwa kwa kipindi cha miaka kumi na unafadhiliwa na nchi za Denmark na Sweden, Sh. milioni 500 zimetolewa kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mbegu bora za alizeti kwa mikoa yote nchini.

"Kwa kutambua uhaba wa mafuta nchini, serikali kupitia Wizara ya Kilimo kwa kuwatumia watafiti kutoka TARI, TOSCI, wazalishaji wa mbegu pamoja na sisi AMDT tulikaa meza moja na kujadiliana ni kwa namna gani tunaweza kusaidia upatikanaji wa mafuta hapa nchini, tumeanza kujikita katika kuhamasisha kilimo bora cha alizeti kwa kuzalisha mbegu bora hapa nchini," alisema Chitema.

Alisema kuwa kwa mkakati huo, wamepanga kuzalisha tani 50 za alizeti na zinatarajiwa kuingia sokoni kwa ajili ya kutumika msimu ujao wa kilimo.

Meneja mradi wa uzalishaji na upatikanaji wa mbegu bora za alizeti nchini na Mratibu wa utafiti wa zao hilo, Frank Reuben, alisema mahitaji ya mafuta nchini ni makubwa ukilinganisha na upatikanaji uliopo.

Alisema licha ya kuwapo kwa uhitaji mkubwa wa mafuta nchini lakini bado zao la alizeti linachukua asilimia 83 ya uzalishaji wa mafuta ya kula ukilinganisha na mazao mengine.

"Serikali yetu inatekeleza mpango huu ili kuhakikisha tunakabiliana na uhaba wa mafuta ya kula nchini sasa tumeanza kuzalisha mbegu bora za zao hili ili zijibu mahitaji ya wananchi kuwa na uhakika wa bidhaa hiyo ambayo kwa sasa inauzwa kwa gharama kubwa," alisema Reuben.

Victoria Silungwe, mkulima wa alizeti kutoka mkoani Songwe, alisema ukosefu wa mbegu bora husababisha uzalishaji kuwa mdogo kwa wakulima wadogo. Alisema mradi huo utawasaidia kupata mbegu bora ambazo zitaongeza uzalishaji wa mazao yao ikilinganishwa na misimu ya kilimo iliyopita.

"Tunawashukuru wadau wengi kwa kuja na ufumbuzi wa upatikanaji wa mbegu bora, mwaka jana nililima ekari tatu, lakini niliambulia gunia moja, licha ya kutumia gharama kubwa ya ununuzi wa mbegu ambazo zilitoka nje ya nchi ni matumaini yetu kwamba mbegu hizi ambazo zinazalishwa nchini zitajibu matarajio yetu," alisema Silungwe.

Pia uhaba wa mvua kwa msimu uliopita umechangia wakulima kupata mavuno kidogo.

Angela Andrea, alisema analitegemea zao la alizeti kuendesha maisha yake na kupatikana kwa mbegu bora msimu huu kutasaidia kuongeza uzalishaji na kupata mavuno mengi kwa kuwa tayari bei elekezi ya serikali imetolewa kuhusu gharama.



Msimamizi wa Kiwanda cha kuzalisha mbegu cha Highland Seed Growers Limited jijini Mbeya, Aidan Levy (kulia), mwishoni mwa wiki alitoa ufafanuzi wa namna mbegu za alizeti zinavyopimwa na kupakiwa kwenye kifungashio kwa wadau wa kilimo nchini (hawapo pichani). **PICHA: GRACE MWAKALINGA**

# RC Homera aviagiza vyuo vikuu utafiti sekta kilimo

**Na Grace Mwakalinga,**
MBEYA

MKUU wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, amevitaka vyuo vya elimu ya juu nchini, kufanya utafiti wa kisayansi kwenye sekta ya kilimo ili kuwasaidia wakulima kupata taarifa sahihi za kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi.

Aidha, utafiti huo wa kisayansi ambao utasheheni maarifa na ujuzi na kutolewa kwa wakulima utasaidia kukidhi mahitaji ya soko la ndani na nje ya nchi katika uzalishaji wa mazao.

Homera alitoa kauli hiyo mwishoni mwa wiki, akimwakilisha mgeni rasmi, Waziri wa Kilimo, Hussein Bashe, katika kongamano la siku ya kumbukizi ya 19 ya Hayati Mwalimu Julius Nyerere lililofanyika Chuo Kikuu Mzumbe Ndaki ya Mbeya.

Alisema Nyerere aliamini kilimo ndio uti wa mgongo na kupitia elimu, nchi ingepata wataalamu lukuki ambao wangeongeza thamani ya mazao ya kilimo na viwanda vya uchakataji.

"Hayati Mwalimu Nyerere anakumbukwa kwa mengi likiwamo kuanzisha taasisi za elimu za juu za ndani ya nchi yetu, nanyi Mzumbe ni zao la mtazamo huu hasa katika nyanja za uongozi," alisema Homera.

Alisema katika kuhakikisha taasisi za elimu zinasaidia kukuza na kuendeleza sekta ya kilimo nchini marais waliopita walikuwa mstari wa mbele katika kutengeneza ajenda za kuhakikisha kilimo kinakuwa na tija kwa mtu mmoja mmoja na taifa kwa ujumla.

Hata Rais wetu Samia Suluhu Hassan, ametekeleza hayo kwa vitendo kwa kusaini mikataba zaidi ya 21 ya skimu za umwagiliaji kwa ajili ya kuongeza uzalishaji wa mazao na kutoa elimu ya kilimo chenye tija nchini.

Aliongeza kuwa, Mkoa wa Mbeya una skimu 13 za umwagiliaji kwa ajili ya kuwasaidia wakulima kujikitiza kwenye kilimo biashara kuliko ilivyo sasa.

Kwa upande wake, Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Makongoro Nyerere, alisema historia ya Mwalimu Nyerere, ilichagizwa na juhudi, kufanya kazi, kutokata tamaa, uzalendo, uadilifu, tabia na mwenendo ndizo zilileta mafanikio kwenye kilimo na elimu.

Profesa Samwel Kabote akimwakilisha Makamu Mkuu wa Chuo cha Sokoine, alisema sekta ya kilimo itazidi kuongeza uzalishaji kama wakulima wataacha kilimo cha mazoea.

Kaimu Makamu Mkuu wa Chuo Kikuu cha Mzumbe, Prof. William Mwegoha, alisema endapo mtazamo wa Mwalimu Nyerere ukieleweka na kutumika vyema utasaidia kutimiza azma ya nchi ya kukuza maendeleo kwa wananchi na jamii.





# Prof. Mkenda aiagiza Bodi NECTA kuimarisha usimamizi mitihani

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, Prof. Adolf Mkenda, ameitaka Bodi mpya ya Baraza la Mitihani Tanzania (NECTA), kuimarisha usimamizi wa mitihani na mifumo ya utoaji taarifa ili kuondoa dosari za mara kwa mara.

Prof. Mkenda alibainisha hayo juzi jijini hapo alipokuwa akizindua bodi hiyo.

Aliitaka kusimamia kuimarishwa kwa mfumo wa usimamizi wa uendeshaji mitihani na upokeaji taarifa za kusaidia Baraza kuendelea kupata taarifa za dosari mbalimbali ikiwamo za udanganyifu wa mitihani inapotokea.

"Kazi kubwa iliyoko ni kuboresha pale walipoachia watangulizi wenu, endeleeni kuboresha mifumo ukiwamo ule wa usahihishaji kielektroniki.

Pia tunajua bado kuna changamoto hasa ipo kule tunapopeleka mitihani, hivyo Bodi na Baraza endeleeni kufuatilia na kuhakikisha mnasimamia kwa kushirikiana na kamati husika," alisisitiza Prof. Mkenda.

Aliagiza kupitia kamati za mitihani kuona kama zinajitosheleza au zinahitaji kuboreshwa ikiwa ni pamoja na kupitia upya vituo vya usahihishaji mitihani.

"Angalieni vituo vya usahihishaji wa mitihani mnavichaguaje na kwa vigezo gani na kufanya mapitio," aliagiza.

Vilevile, alimpongeza Prof. William Anangisye kwa kuteuliwa na Rais kuwa Mwenyekiti wa Baraza la NECTA pamoja na wajumbe aliowateua.

Pia alilipongeza Baraza lililomaliza muda wake kwa kutekeleza majukumu kwa mafanikio makubwa.

Katika hatua nyingine, Prof. Mkenda alipongeza Baraza la Mitihani la Tanzania kwa kuanzisha mfumo wa kielektroniki wa usahihishaji mitihani(E-Marking) na kuwataka kuongeza nguvu kwenye kuimarisha usalama na kuhakikisha mfumo huo unapunguza gharama bila kuathiri maslahi ya watumishi, wasahihishaji na wasimamizi.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya NECTA, Prof. William Anangisye, aliahidi kwa niaba ya wajumbe wa Bodi hiyo kufanyia kazi maelekezo yote yaliyotolewa na Waziri wa Elimu kwa uadilifu na ufanisi mkubwa ili kufikia malengo mapana ya baraza hilo.



Ofisa Elimu Msingi wa Halmashauri ya Jiji la Dodoma, Prisca Mayalla, akizungumza na wazazi, walezi wenye watoto wanaosoma Shule ya Msingi Mlimwa (A) jijini humo kuhusu uwajibikaji wa malezi kwa watoto wao juzi. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Shekhe afanya dua kuombea mvua dhidi mabadiliko tabianchi

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

SHEKHE wa Baraza Kuu la Waislamu Tanzania, Mkoa wa Dodoma, Mustaph Rajabu, amesema kutokana na mabadiliko ya tabianchi yanayotokea hapa nchini wakulima wa Kanda ya Kati, wanatakiwa kuandaa mazao yenye uhitaji wa mvua chache.

Kiongozi huyo aliyasema hayo mwishoni mwa wiki wakati akitoa mawaidha kwa waumini katika sala maalumu ya dua ya kuombea mvua iliyofanyika msikiti mkuu wa Gadaff, mkoani hapa.

Alisema kutokana na mabadiliko hayo ya tabianchi wakulima wa kanda hiyo wanatakiwa kuzingatia ushauri wa wataalamu kutumia mvua zilizoko kupanda mazao yanayostahimili uchache wa mvua.

"Andaeni mashamba na mbegu bora ambazo zitakazoendana na mvua za msimu zinazotarajia kunyesha ili kupata mavuno ya kutosha," alisema.

Aliwahimiza viongozi wa misikiti wa wilaya, kata hadi vijijini kuwahamasisha wakulima kuandaa mashamba mapema pamoja na mbegu bora zitakazoendana na mvua hizo.

"Himizeni waumini kufanya dua ya mara kwa mara ya kuomba mvua ili kuondokana na ukame, pia dua zifanyike kupitia mihadhara na misikiti kwa mujibu wa maelekezo ya Mufti Shekhe Mkuu wa Tanzania, Dk. Abubakar Zuberi."

"Ameelekeza viongozi wote wa dini ya Kiislamu pamoja na waumini tufanye dua kwenye maeneo mbalimbali ya kumwomba Mungu kwenye kipindi hiki tunachotarajia mvua za msimu huu," alisema.

Pia aliwaomba kumwomba Mungu aziondoe ajali zinazotokea mara kwa mara na kusababisha watu kupoteza maisha na wengine kupata ulemavu.

# Serikali kuzipatia alama ubora bidhaa za wajasiriamali

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

KATIBU Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wanawake na Makundi Maalum, Dk. Zainab Chaula, ameshauri kufanyika utafiti wa bidhaa zinazozalishwa na wajasiriamali wa ndani zinazokidhi vigezo ili kupatiwa alama za ubora.

Dk. Chaula alitoa rai hiyo jana aliotembelea wanufaika wa mikopo inayotolewa kupitia wizara hiyo jijini hapo.

Aliagiza zote ziwekewe alama itakayoitambulisha bidhaa husika ili iwe nyepesi kutambulika kwenye mfumo wa ulipaji wa kodi ya serikali kwenye mamlaka za Serikali za Mitaa.

Alifafanua kuwa mikopo ya zaidi ya Sh. milioni 170 iliyotolewa na serikali kupitia wizara hiyo imewanufaisha wajasiriamali wa Jiji la Dodoma na kuwaongeza kwa mafanikio wanayoyapata.

"Ziara yetu hii tumekuja kuamsha ari na kuchochea morali kwa wanajamii wao wenyewe watumie rasilimali zinazowazunguka ili waweze kuzibadilisha changamoto kuwa fursa," alisema.

Aziza Abdi, Mkurugenzi wa Kampuni inayojishughulisha na uchakataji wa taka za plastiki ambaye alipokea Sh. milioni 100, alishukuru serikali kwa kuwawezesha mikopo ambayo imesaidia kupanua biashara hiyo na kwa sasa wana uwezo wakuchakata tani 130 kwa mwezi tofauti na awali walipoanza mwaka 2013 walikuwa wakizalisha tani 40 pekee.

"Kwa sasa nimenunua gari, moja nimefanikiwa kuongeza ajira kutoka 20 hadi 60 za kudumu sambamba na kuboresha maslahi yao, lakini wafanyakazi wa kutwa wanafikia 300 kwa sasa," alisema Aziza.

Naye Yolanda Kaswalala, anayejishughulisha na uchakataji wa bidhaa za mazao ikiwamo mafuta ya alizeti, alipata mkopo wa Sh. milioni 50 ambao umesaidia kuongeza mashine.

Akiongea wakati wa ziara hiyo, Mkurugenzi wa Maendeleo ya Jamii, Patrick Golwike, alisema Sera ya Maendeleo ya Jamii inawataka Maofisa Maendeleo ya Jamii kuamsha ari na kuleta uchechemuzi miongoni mwa jamii ili kujiletea maendeleo kwa kutumia rasilimali zinazowazunguka.

# Zanzibar yakabiliwa wagonjwa wengi tatizo la macho

**Na Mwandishi Wetu**

ZANZIBAR ina wagonjwa wengi wenye matatizo ya macho, misaada kutoka taasisi za ndani na nje ya nchi ni muhimu.

Akizungumza juzi Ikulu na kikundi cha madaktari kutoka Taasisi ya 'Association Vission-for-Puma (Germany), Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema pamoja na Zanzibar kuwa na hospitali ya macho katika Hospitali Kuu ya Mnazimmoja, bado inakabiliwa na changamoto kubwa ya ukosefu wa vifaa muhimu pamoja na wataalamu.

Dk. Mwinyi aliipongeza timu ya madaktari hao kwa ujio wao pamoja na kazi kubwa waliyofanya ya kuwapatia huduma wagonjwa katika Hospitali ya Kikosi cha Kuzuia Magendo Zanzibar (KMKM).

Alisema serikali itaangalia namna ya kuendeleza ushirikiano ulioanza na taasisi hiyo katika siku zijazo ili wananchi wapate huduma bora za afya.

Naye kiongozi wa timu hiyo ya madaktari kutoka Taasisi ya 'Association Vission–for–Puma (Germany) Dk. Frank Klemm, alipongeza ushirikiano mkubwa walioupata kutoka uongozi wa kikosi cha KMKM pamoja na madaktari wa hospitali hiyo iliyopo Kibweni katika kipindi chote walichotoa huduma.

Alisema wagonjwa 100 walipatiwa huduma za macho katika kliniki hiyo iliodumu kwa siku 12, huku wengine wakipatiwa miwani ya macho.

**Alisema serikali itaangalia namna ya kuendeleza ushirikiano ulioanza na taasisi hiyo katika siku zijazo ili wananchi wapate huduma bora za afya**

# Wajawazito wenye kisukari waitwa Mnazimmoja kwa uangalizi maalum

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAJAWAZITO wanaoishi na maradhi ya kisukari wametakiwa kutumia Kliniki ya Hospitali ya Mnazimmoja kwa ajili ya uangalizi wa afya zao.

Daktari Bingwa wa Wanawake na Uzazi wa hospitali hiyo, Ummulkurthum Omar Hamad, alitoa wito huo jana kwenye jumuiya ya watu wanaoishi na maradhi ya yasiyoambukiza, Mpendae wakati akizungumza na waandishi wa habari.

Alisema wajawazito wenye kisukari wanahitaji uangalizi mkubwa kulingana na hali zao ili kunusuru afya zao pamoja na watoto.

Alisema, kipindi cha ujauzito kwa mama mwenye kisukari ni kigumu kwa sababu kinasababisha mama na mtoto kuwa katika hatari.

Aidha, alisema kipindi hicho sukari huzidi hupanda au kushuka jambo ambalo ni hatari kwa afya ya mama na mtoto.

Aliwataka kinamama kuchukua tahadhari mapema na kufuata ushauri wa wataalamu wa afya kabla ya ujauzito, baada na wakati wa kujifungua ili wawe katika mazingira salama.

Naye Mshauri wa Saikolojia kutoka Hospitali ya Kidongo Chekundu, Asha Udi Mwinyi, alisema kuna uhusiano mkubwa kati ya magonjwa ya kimwili na afya ya akili kwa sababu huwa yanategemeana.

Alisema akili ni kazi ya ubongo ambayo husaidia kufikiria mambo mbalimbali na kutoa uamuzi sahihi na mtu anapokosa afya nzuri ya akili hushindwa kutatua changamoto.

Alisema changamoto ni nyingi za maradhi, kimaisha, kijamii na kifamilia zinazosababisha mtu kuingia katika kutetereka afya ya akili.



Wafanyabiashara wa mayai wakiyauza kando ya Soko Kuu la Darajani Zanzibar kupisha ukarabati wa soko hilo jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Kilimo matango bahari, mwani chaleta tija uchumi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MKURUGENZI Idara ya Ushirikiano wa kikanda, Wizara ya Mambo ya Nje na Ushirikiano wa Afrika Mashariki, Balozi Agnes Richad Kayola, amesema kilimo cha mwani na ufugaji wa matango bahari kimeonekana kuwa na tija kubwa kwa uchumi wa Zanzibar.

Aliyasema hayo jana wakati akifunga mkutano wa siku tano wa kilimo cha vifaranga vya matango bahari na mbegu bora ya kilimo cha mwani.

Kayola ambaye ni mratibu nchi za pembezoni mwa Bahari ya Hindi, alisema wajumbe wa mkutano wa nchi za pembezoni kwa Bahari ya Hindi wamefurahishwa na hatua iliyofikiwa Zanzibar kuhusu kilimo hicho ambacho soko lake ni kubwa duniani.


Alisema wajumbe hao walijadili na kuona jinsi Zanzibar ilivyopiga hatua katika uchumi wa buluu na uvuvi na kuridhishwa na hatua zilizofikiwa katika uchumi wa buluu ikiwamo ufugaji wa vitango bahari.

Aidha, alisema lengo la Serikali ya Zanzibar ni kuona kuwa mazao ya bahari yanakuza uchumi wa nchi kwa maendeleo ya taifa. "Wajumbe wa mkutano huu wanafanya kazi kwa pamoja ili kuona namna gani wanapiga hatua katika kukuza uchumi kupitia mazao ya mabaharini," alisema.

Naye Mkurugenzi wa uchumi wa buluu wa taasisi ya ukanda wa pembezoni mwa Bahari ya Hindi, Rina Sety Awati, alisema wamejifunza mambo mengi juu ya kuboresha kilimo hicho ili kuwa cha manufaa makubwa kwa nchi wanachama wa Jumuiya ya Afrika Mashariki.

Alisema wameridhishwa na hatua iliyofikiwa na Serikali ya Zanzibar katika kukimarisha kilimo cha mwani ambacho asilimia 90 kinalimwa na wanawake pamoja na ufugaji wa matango bahari.

Kwa upande wao washiriki wa mkutano huo walisema wamejifunza mambo mengi ya ufungaji wa matango bahari na mbegu bora ya kilimo cha mwani na kuona Zanzibar ilivyojipanga kuhakikisha mazao ya bahari yanatunzwa.





# DC Mboneko ataka kasi ujenzi vyumba madarasa

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

MKUU wa Wilaya ya Shinyanga, Jasinta Mboneko, ametaka kasi iongezeke kwenye ujenzi wa vyumba vya madarasa ili vitumiwe na wanafunzi watakaoingia kidato cha kwanza mwakani.

Akizungumza juzi wakati wa ziara ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa vyumba hivyo katika Manispaa na Halmashauri ya Shinyanga, alisema maendeleo ya ujenzi unaridhisha, huku akiagiza kasi zaidi ili wanafunzi watakapoanza kuwe na mazingira mazuri wafanye vizuri kitaaluma.

"Rais Samia Suluhu Hassan katika halmashauri hizi mbili Manispaa ya Shinyanga na Wilaya ya Shinyanga, ametoa kiasi cha Sh. bilioni 2.2 kwa ajili ya ujenzi wa vyumba vya madarasa 109, ikiwa ni manispaa vyumba 61 na Wilaya ya Shinyanga 45 ambavyo vitatumiwa na wanafunzi wa kidato cha kwanza mwakani," alisema Mboneko.

Pia aliwataka mafundi kufanya kazi hiyo kwa uaminifu mkubwa kwa ubora ili kazi iendane na thamani ya fedha.

Naye Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kolandoto, Manispaa ya Shinyanga, Deus Maganga, alisema ujenzi wa vyumba saba vya madarasa shuleni hapo, umeondoa upungufu uliokuwapo na sasa hawana tena tatizo hilo na wanafunzi watasoma bila ya kubanana, darasa moja walikuwa wakisoma wanafunzi 70 badala ya 40.

Josephine Juma ni mwanafunzi wa kidato cha kwanza Shule ya Sekondari Kolandoto, alisema wanafunzi wanaposoma wakiwa wamesongamana darasani kuelewa masomo inakuwa vigumu.



Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu Kazi, Ajira, Vijana na Wenye Ulemavu, Prof. Joyce Ndalichako, akimkabidhi cheti Praise Mwiruki ambaye ni mwanafunzi bora katika mahafali ya 57 ya Chuo cha Elimu ya Biashara (CBE) mwishoni mwa wiki. Mwanafunzi huyo alipata wastani wa juu wa ufaulu wa GPA 4.9. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

## Makundi mawili kuongezwa tuzo za EJAT 2022

**Na Restuta Damian,** BUKOBA

BARAZA la Habari Tanzania (MCT), limesema litaongeza makundi mawili kwenye habari za kushindaniwa katika Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT), kwa mwaka huu.

Hayo yamesemwa mwishoni mwa wiki na Katibu Mtendaji wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Kajubi Mkajanga, wakati akizindua Tuzo za Umahiri wa Uandishi wa Habari Tanzania (EJAT) mwaka 2022, mjini Bukoba.

Alisema tuzo za mwaka huu zitahusisha makundi mapya mawili ambayo yatafanya kuwa na idadi ya jumla ya makundi 18 yenye kushindaniwa kutokana na ombi la serikali na wadau wa habari.

"Makundi mapya ya habari yatakayoongezwa ni pamoja na yale ya habari za sensa limeongezwa kufuatia ombi la serikali lilitolewa Mei 28, mwaka huu na kundi la pili ni la habari za tozo na mapato lililotokana na maombi ya wadau," alisema Mkajanga.

Aidha, alisema lengo la kuwapo na tuzo hizo ni kutambua na kuwatunza waliofanya kazi zao vizuri kutokana na makundi yanayoshindaniwa, ikiwa hii ni mara ya 14 kamati ya maandalizi (EJAT) ikiongozwa na (MCT) kuandaa mashindano hayo tangu mwaka 2009.

"Tumeweka habari za uchumi, biashara na fedha, michezo na utamaduni, kilimo na biashara ya kilimo, elimu, utalii na uhifadhi, uchunguzi, data, haki za binadamu, utawala bora na uwajibikaji, jinsia na watoto, gesi mafuta na uchimbaji madini, walemavu, afya, teknolojia, ushirika, kodi tozo na mapato, habari za sensa na kundi la wazi," alisema Mkajanga.

Aidha, alisema yapo makundi yaliyoondolewa kutokana na kuwa na mwitikio mdogo kwa miaka kadhaa kwenye makundi ya mpigapicha bora gazetini, runinga na mchora katuni.

# Wazazi, watoto wenye vichwa vikubwa wasaidiwa malazi

**Na Vitus Audax,** MWANZA

ZAIDI ya wazazi 700 kutoka mikoa mbalimbali ndani na nje ya Kanda ya Ziwa hufika katika Hospitali ya Rufani Kanda Bugando kwa mwaka kushughulikia matibabu ya watoto wenye ugonjwa wa vichwa vikubwa na mgongo wazi huku robo tatu ya wazazi hao hukosa malazi katika kipindi cha kusubiri matibabu ya watoto wao.

Wazazi hao hulala vibarazani huku wengine wakiishi na kulala sehemu za wagonjwa kusubiri huduma kutokana na uhaba wa fedha za gharamia malazi katika kipindi hicho.

Janeth Mussa, mama wa mtoto mwenye ugonjwa wa kichwa kikubwa kutoka katika Wilaya ya Mpanda, mkoani Katavi, alifika Mwanza kwa ajili ya kumpatia mtoto wake huduma ya upasuaji baada ya kupata misaada kutoka kwa wasamaria wema mkoani Katavi.

Aliliambia gazeti hili kuwa baada ya kufika katika Hospitali ya Rufani Bugando Machi 2022, alibahatika kuanza huduma ya matibabu kwa mtoto wake, lakini tatizo kubwa ilikuwa ni mahala pa kuishi na kulala wakati akiendelea na huduma.

Alisema hakuwa na namna yakufanya bali kulala katika vibaraza vya hospitali hiyo akivumilia baridi akitumaini kuwa mtoto wake anaendelea kupata huduma.

Shirika lisilo la kiserikali la Child Help kupitia mwanzilishi wake nchini Janeth Manoni, limejenga nyumba ya matumaini kwa ajili ya kuhifadhi wazazi pamoja na watoto wao wanaposubiri huduma ya matibabu.

Akizungumza na gazeti hili, Janeth alisema dhumuni la nyumba hiyo ambayo kwa Kanda ya Ziwa imejengwa katika Kijiji cha Kitongo, Kata ya Lugeye wilayani Magu mkoani Mwanza, ni kuhudumia watoto zaidi ya 200 kwa mwaka.

"Katika nyumba yetu ya matumaini tunawahifadhi wazazi pamoja na watoto wao waliofikishwa hospitalini kwa ajili ya huduma ya upasuaji ambayo huchukua muda mrefu kukamilika, ikiwa tunawahudumia malazi, chakula, usafiri wa kwenda na kurudi hospitalini pamoja na mahitaji mengine," alisema.

Kwa mujibu wa Daktari Daraja la Pili kutoka Idara ya Upasuaji Ubongo na Mfumo wa Fahamu hospitalini humo, David Kambale, ugonjwa wa kichwa kikubwa kitaalamu hujulikana kwa jina la 'Hydrocephalus' ikiwa jina hilo linatokana na neno la kigiriki lenye maana ya maji ndani ya kichwa, si kila mwenye kichwa kikubwa ana 'hydrocephalus'.

Aidha, licha ya kuwa na uhitaji wa kuwahudumia watoto wengi bado kituo hicho kina uhitaji wa vitanda pamoja na magodoro ya kutosha ikiwa ni pamoja na mahitaji ya eneo kwaajili ya kuzidisha ujenzi wa kituo ili kiwe kikubwa zaidi.

"Bado kama wadau wa watoto wenye ugonjwa huu tunatatizwa na upatikanaji wa bima za afya kutokana na ugumu wa upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa kwa watoto hawa," alisema Abdulhakim Bayakub Mkurugezi Child Help Tanzania.

Akizungumza kwa niaba ya Mkuu wa Wilaya ya Magu wakati wa ufunguzi wa Nyumba ya Matumaini juzi, Ofisa Tawala Wilaya ya Magu, Anna Mbao, aliwahakikishia kuwapa ushrikiano na waanaendelea na shughuli zao za kuwasaidia watoto kupata matibabu.

Wataendelea kutoa ushirikiano kwa shirika hilo na kutoa elimu kwa jamii juu ya namna rahisi ya upatikanaji wa vyeti vya kuzaliwa ili kutatua changamoto ya upatikanaji wa bima za afya kwa watoto hao.

"Tutahakikisha tunaboresha miundombinu katika shule mbalimbali ili kuwezesha wanafunzi wenye tatizo hilo wanapata elimu katika mazingira mazuri na wezeshi kwa manufaa ya maisha yao ya baadaye," alisema Mbao.

## Ataka fedha ujenzi madarasa zitumike kwa kazi hiyo

**Na Julieth Mkireri,** CHALINZE

MWENYEKITI wa Halmashauri ya Chalinze, Hassan Mwinyikondo, amewataka wanaosimamia fedha za ujenzi wa vyumba vya madarasa halmashauri hiyo kusimamia na kutumika kama zilivyoelekezwa na ujenzi unakamilika kwa wakati.

Akizungumza mwishoni mwa wiki kwenye Baraza la Madiwani, alisema wanafunzi wote watakaochaguliwa kuanza kidato cha kwanza mwakani lazima wapate na hawategemei kikwazo kutoka kwa wasimamizi.

Alisema halmashauri hiyo imepokea Sh. bilioni 1.2 kwa ajili ya vyumba vya madarasa 60 malengo ni kukamilisha ujenzi ndani ya miezi mitatu ambao ulianza Oktoba, mwaka huu.

"Tunamshukuru Rais Samia Suluhu Hassan fedha tulizopokea tutazisimamia vizuri, hakuna mwanafunzi atakayekwama kwenda shule kwa kukosa nafasi," alihakikisha.

Mwinyikondo alisema kwa kushirikiana na Mkurugenzi wa halmashauri hiyo wanasimamia kwa karibu na wameweka utaratibu wa kufanya ukaguzi kujiridhisha na mwenendo wa ujenzi na matumizi ya fedha.

Akizungumzia suala la wanafunzi wa Shule ya Sekondari ya Kiwangwa ambao bado wanatumia madarasa kama bweni, alisema wanajipanga kuongeza jengo lingine kuondoa tatizo hilo baada ya kufanya ukaguzi wa matumizi ya Sh. milioni 100, zilizotolewa na halmashauri hiyo.

Katika kikao hicho, Diwani wa Kata ya Kibindu, Ramadhani Mkufya, aliomba ufafanuzi kwa mkurugenzi kuhusu malipo ya wakulima wa pamba ambao imeshanunuliwa.

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Chalinze, Ramadhani Possi, alisema Bodi ya Pamba imeanza kulipa pamba iliyonunuliwa hivi karibuni na zaidi ya Sh. milioni 40 zimeshalipwa na wakulima waliosalia watalipwa leo.

# Vikao vya juu CCM vyateua wagombea nafasi nyeti

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

VIGOGO mbalimbali wa Chama Cha Mapinduzi (CCM) wameteuliwa kugombea nafasi za uongozi ndani ya CCM na jumuiya zake katika ngazi ya Mkoa na Taifa.

Uteuzi huo ulifanywa jana na Halmashauri Kuu ya CCM Taifa (NEC), katika kikao chake kilichofanyika chini ya Mwenyekiti wake Rais Samia Suluhu Hassan jijini hapo.

Kwa mujibu wa taarifa iliyotolewa na Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi, Shaka Hamdu Shaka, uteuzi huo umefanyika kwa mujibu wa Katiba ya CCM ya Mwaka 1977, toleo la 2022 Ibara ya 82(1).

Alitaja wagombea wa nafasi ya Mwenyekiti na Makamu Mwenyekiti wa Jumuiya za CCM ngazi ya Taifa walioteuliwa nafasi ya Mwenyekiti wa UVCCM Taifa ni Farid Mohamed Haji, Kassim Haji Kassu, Mohamed Ali Mohamed (Kawaida) na Abdallah Ibrahim Natepe.

Nafasi ya Makamu Mwenyekiti UVCCM ni Khadija Khalid Ismail, Dorice John Mgetta, Victoria Charles Mwanziva na Rehema Sombi Omary.

Mwenyekiti wa UWT Taifa ni Gaudentia Mugosi Kabaka, Kate Sylvia Kamba, Dk. Wemael Allen Chamshama, Mariam Mohamed Lulida na Mary Pius Chatanda, huku nafasi ya Makamu Mwenyekiti walioteuliwa kuwania ni Latifa Nasser Ahmed, Thuwaybah Edington Kissasi, Hafsa Said Khamis na Zainab Khamis Shomari.

Shaka aliwataja walioteuliwa kuwania nafasi ya Mwenyekiti wa Wazazi Taifa kuwa ni Dk. CPA. Edmund Bernard Mndolwa, Fadhili Rajabu Maganya, Bakari Nampenya Kalembo, Said Mohamed Mohamed (Dimwa), Mwanamanga Juma Mwanduga, Ally Maulid Othman, Ali Khamis Masudi na Hassan Haji Zahara.

"Nafasi ya Makamu Mwenyekiti wa Wazazi Taifa walioteuliwa ni Haidar Haji Abdalla, Dk. Wemael Allen Chamshana, Fatma Abeid Haji, Rachel Ntiganyigwa Kabunda, Neema George Mturo, Zahoro Salehe Mohamed na Dogo Idd Mabrouk.

Alisema uhaguzi wa viongozi wa jumuiya hizo kwa ngazi ya Taifa utafanyika Novemba 24-29, mwaka huu.

"Wagombea wote wanakumbushwa kuheshimu kanuni za uchaguzi za CCM na misingi ya chama kwa kufanya siasa safi na kuzingatia maadili ya chama wakati wote," alisema.

Alisema orodha ya majina ya wagombea uongozi Chama na Jumuiya zake ngazi ya mkoa yatatumwa katika mikoa husika.




Meneja Mawasiliano na Utawala Tanzania Breweries Limited (TBL), Catherine Mabula, akifungua mafunzo ya kuongoza waendesha pikipiki kutumia alama za barabarani kwa maofisa wa usalama barabarani ikiwa ni kampeni ya TBL ya "Okoa Maisha". Kushoto ni Mwanasheria wa Kikosi cha Usalama Barabarani na Mkuu wa Dawati la Elimu, SP Deus Sokoni na (katikati) Mkuu wa Kikosi Kanda ya Dar es Salaam, ACP William Mkonda. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# 'Uhamasishaji ulipaji wa kodi ni kazi ya kila mtu'

**Na Elizabeth Zaya**

CHUO cha Kodi kimesema kazi ya kuhamasisha wananchi umuhimu wa kulipa kodi si ya taasisi moja pekee inatakiwa kufanywa na kila mtu katika nchi.

Kauli hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki jijini Dar es Salaam na Naibu Mkuu wa Chuo hicho, Emmanuel Masalu, wakati akizindua Chama cha Washauri wa Kodi Tanzania.

Alisema kodi ni ajenda kubwa duniani inayoshughulikiwa na watu wengi, kuna haja ya kila mtu nchini kutumia nafasi yake kuhamasisha ulipaji kwa maendeleo ya nchi.

"Kodi ni ajenda inayoshughulikiwa na wengi, sio kazi ya taasisi moja au mbili na ikumbukwe kuwa kushughulika na masuala haya ya kodi ni kupambana na kujali maendeleo ya watu katika nchi, ni kushughulika na uhai wa taifa," alisema Masalu.

"Hapa kwetu serikali imekuwa ikituhamasisha na inaendelea kutuongoza kukusanya kodi, sio kwa nia nyingine ni kwa sababu katika maendeleo yetu ya taifa, tunahitaji kodi hiyo." Alikitaka chama hicho kuongeza nguvu zaidi kuwahamasisha Watanzania umuhimu wa kulipa kodi.

"Na kadiri mnavyoongeza nguvu katika kuhamasisha Watanzania kujitoa katika kulipa kodi, mtakuwa mnamuunga mkono Rais wetu kwa kazi ambayo amekuwa akihamasisha kila siku," alisema Masalu.

"Ninaamini kwamba chama hiki kitakuja na nguvu mpya ya pamoja, kitakuwa na sura ya weledi zaidi na kitashirikiana vyema na vyombo vya sekta ya umma kusimamia kwa umakini mkubwa jambo hili la ulipaji kodi."

Kwa upande wake, Mwenyekiti wa muda wa chama hicho, Felician Busigara, alisema wapo tayari kuifanya kazi ya kuhamasisha Watanzania kulipa kodi na wanapita katika kila taasisi kuzungumza nao kuhusu umuhimu wake.

"Tunaomba ushirikiano wa Watanzania, tunapowatembelea kwa ajili ya kufanya kazi hii ya uhamasishaji, wawe wawazi, wasifiche chochote, kazi hii ya kujenga nchi ni yetu sote," alisema Busigara.

# Polisi yashikilia wahamiaji haramu 38 raia wa Ethiopia

**Na Boniface Gideon,** TANGA

JESHI la Polisi mkoani Tanga linawashikilia wahamiaji haramu 38 walioingia nchini bila kibali wakiwa kwenye gari namba KBR911Z aina ya Benz tela namba 2D2426 mali ya Kampuni ya Enterprises ya Mombasa nchini Kenya.

Akithibitisha mwishoni mwa wiki kukamatwa kwa raia hao wa kigeni, Kamishna Msaidizi Mwandamizi Jeshi la Polisi Mkoa wa Tanga, Henry Mwaibambe, alisema tukio hilo limetokea Novemba 10 majira ya saa tatu asubuhi katika Kata ya Kitumbi, Tarafa ya Mazingira, wilayani Handeni, mkoani Tanga.

Alisema wahamiaji hao walikamatwa baada ya askari kulisimamisha gari lililokuwa limewabeba huku dereva na utingo wakitoroka na kulitelekeza gari hilo pembeni mwa Barabara ya Mkata - Segera.

Polisi mkoani Tanga imewataka wananchi wote kujiepusha na vitendo vya uhalifu kwa kufanya shughuli halali.

Aliwataka wananchi wenye mapenzi mema ya nchi waendelee kutoa taarifa kwa Jeshi la Polisi ili liweze kupambana na uhalifu.

Kwa upande wake Kamishna Msaidizi wa Jeshi la Uhamiaji mkoani humo, Kagimbo Hosea, alisema wamepokea wahamiaji haramu 38 raia wa Ethiopia wote wakiwa wanaume walioingia nchini kinyume cha Sheria ya Uhamiaji kifungu cha 45(1) (i) sura ya 54 iliyofanyiwa marejeo mwaka 2016.

Alisema uchunguzi unaonesha gari hilo liliingia Tanzania kupitia mpaka wa Tarakea Mkoa wa Kilimanjaro Septemba 19, mwaka huu na mifumo inaonesha gari hilo lilitakiwa kuondoka Desemba 18, mwaka huu.

"Jukumu la kuzuia wahamiaji haramu ni la kila mwananchi, hivyo kila mwananchi anatakiwa kujua madhara ya wahamiaji haramu kwani wengine wanakuja wakitokea nchi ambazo kuna milipuko ya magonjwa mbalimbali kama ebola ni hatari sana kwa afya zetu kama wataingia wakiwa na maambukizi ya magonjwa hayo," alisisitiza Hosea.




Mwanzilishi wa Kampuni ya WESE, Fransis Ekeng, akipeana mkono na Abdirahman Ahmed, Mkurugenzi wa Lake Oil, wakati wa hafla ya utiaji saini iliyofanyika Makao Makuu ya Lake Oil, Kurasini jijini Dar es Salaam mwishoni mwa wiki. Hafla hiyo inaashiria ushirikiano kati ya Lake Oil na WESE nchini kuwawezesha madereva kupata mafuta kupitia Mpango wa Nunua Sasa Lipa Baadaye Bila Riba. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Wawili wafariki dunia ajali ya kugonga 'power tiller'

**Na Gurian Adolf,** NKASI

WATU wawili akiwamo mwanafunzi wa Chuo cha Utabibu cha Mtakatifu Bakhita, Wilaya ya Nkasi mkoani Rukwa, wamefariki dunia papo hapo baada ya gari walilokuwa wakisafiria kugonga power tiller, kuacha njia na kutumbukia mtaroni.

Akitoa taarifa za tukio hilo jana, Kamanda wa Polisi mkoani Rukwa, Theophista Mallya, alisema ajali hiyo ilitokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa 4:15 usiku katika Barabara ya Sumbawanga - Mpanda eneo la Kijiji cha Ntatumbila.

Alisema, waliopoteza maisha ni dereva wa gari dogo aina ya Toyota Sienta yenye namba za usajili T 544 DVV Joseph Razaro (27), lililokuwa lilitokea Sumbawanga mjini kwenda Namanyere, wilayani Nkasi.

Mwingine aliyefariki katika ajali hiyo ni mwanafunzi wa Chuo cha Udaktari cha Mt. Bakhita kilichopo wilayani Nkasi, Maiko Mkambi (25) ambaye alikua ni abiria.

Kamanda Mallya alisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendokasi wa dereva aliyekuwa kwenye mwendo mkali na kukutana na power tiller hiyo, ambaye licha ya kujitahidi kulikwepa hakufanikiwa na kuligonga na kutumbukia kwenye mtaro.

Alisema watu hao walipoteza maisha papo hapo na miili ya marehemu hao imehifadhiwa hospitali teule mjini Namanyere.

Kamanda Mallya, amekiagiza kikosi cha usalama barabarani mkoani humo kumfutia leseni dereva yeyote atakaye sababisha ajali na vifo kwa sababu za kizembe zinazotokana na mwendokasi.

**Watu hao walipoteza maisha papo hapo na miili ya marehemu hao imehifadhiwa hospitali teule mjini Namanyere.**

# Madiwani waagizwa kusimamia miradi fedha za serikali

**Na Thobias Mwanakatwe,**

**IKUNGI**

MADIWANI wa Halmashauri ya Ikungi, mkoani Singida, wameagizwa kusimamia fedha zinazotolewa na serikali za kutekeleza miradi ya maendeleo katika kata zao zinatumika kama ilivyokusudiwa.

Mwenyekiti wa Halmashauri ya Ikungi, Ally Mwanga, alitoa agizo hilo wakati akifungua kikao cha siku ya pili cha Baraza la Madiwani wa halmashauri hiyo.

Alisema serikali inatoa fedha nyingi, ni wajibu wa kila diwani kusimamia matumizi. Aliagiza madiwani kusimamia miradi inayotekelezwa katika maeneo yao na kukamilika kwa wakati kwa kiwango kinachotakiwa.

Naye Mkurugenzi wa Halmashauri ya Ikungi, Justice Kijazi, alisema kumekuwa na changamoto ya baadhi ya watendaji kushindwa kusimamia miradi ipasavyo kwa kutoa visingizio vingi ambavyo havina mashiko ikiwa ni pamoja na kukosa usafiri wa kwenda kukagua miradi.

Kijazi alisema pamoja na serikali kutoa fedha nyingi, kuna changamoto ya maeneo ya utekelezaji wa miradi, ambapo kuna baadhi ya maeneo hayaendani na fedha zinazotolewa kutokana na jiografia ya maeneo husika.

Mgeni rasmi katika kikao hicho Katibu Tawala Mkoa wa Singida, Dorothy Mwaluko, amewataka maofisa ununuzi na wahandisi kuwa kitu kimoja usimamizi wa miradi kwa manufaa ya taifa na kuondoa tofauti.

Alisema kumekuwa na tofauti kati ya maofisa ununuzi na wahandisi hasa mhandisi anapopeleka mahitaji ya mradi kwa maofisa ununuzi, baadhi yao hutoa sababu mbalimbali na kusababisha utekelezaji wa miradi kusuasua kutokana na kutokununuliwa kwa mahitaji hayo.

Mwaluko pia aliwataka wahandisi wa miradi kutembelea na kukagua miradi maeneo yao ili ikamilike ikiwa na ubora unaotakiwa.

Kwa upande wao baadhi ya madiwani walisema watahakikisha wanasimamia fedha zinazotolewa na serikali za utekelezaji wa miradi ya maendeleo wanazisimamia ipasavyo katika kata zao na zinatumika kwa malengo yaliyokusudiwa.

Wamesema watasimamia miradi ya ujenzi wa madarasa unaoendelea katika kata zao na kukamilika kwa wakati na ubora ili kupunguza uhaba wa madarasa katika maeneo yao.

# Msechu aonyesha mjengo wake

**Na Mwandishi Wetu**

MSANII wa Bongo Fleva na mshindi wa pili wa mashindano ya Bongo Star Seach wa mwaka 2009, Peter Msechu, ameonyesha nyumba yake mpya ya kuishi aliyoijenga Kibamba, Dar es Salaam.

Msechu amesema amekuwa akidunduliza fedha kidogo kidogo yeye na mke wake kuanzia miaka 13 iliyopita (mwaka 2009) ambapo walikuwa wakihifadhi asilimia 50 ya kila fedha waliyokuwa wakiipata.

Msechu amesema fedha yake ya kwanza kuikata nusu kwa asilimia 50 ilikua ni shilingi milioni tano aliyoshinda kama mshindi wa pili kwenye Bongo Star Search (BSS) ikiwa ndio kubwa kuishika kwa mara ya kwanza toka azaliwe.

"Nilipoamua kuwa na familia na kuishi kama baba nilijiwekea malengo ya kuhakikisha naipa furaha na amani familia yangu kwa namna yoyote ile.

"Kuanzia mwaka 2009, mara tu baada ya kumalizika shindano la BSS mimi na mke wangu mama Lolo tulifanya maamuzi ambayo yalikuwa hayavumiliki wala kuwezekana kwani tulipitia magumu na yasiyoelezeka tulipokubaliana kuanza kusevu asilimia 50 ya kila pesa nitakayoingia kwa kazi yoyote ile ili tuweze kujenga.

"Haikuwa rahisi kwani kuna muda niligombana sana na mama Lolo kwani alitaka kujua kila hela ninayopata na alidai na kuhakikisha ile asilimia 50 tuliyokubaliana inatengwa na haitumiki kwa vyovyote vile.

"Tuligombana, tulikwazana tulifokeana ila leo hii mimi na mke wangu mama Lolo, watoto wetu watatu Lauren, Lian na Levin kwa furaha kubwa tunapenda kuwakaribisha nyumbani kwetu," alisema Msechu.

Nyumba hii ambayo alianza kujenga mwaka 2017 ikiwa ni miaka 8 tangu aanze kudunduliza kidogo kidogo ina vyumba vinne vya kulala vyote vikiwa na choo na bafu ndani, sebule, dining na ofisi.





# 50 CENT KUCHEZA TAMTHILIA YA UTAPELI WA HUSHPUPPI

**LOS ANGLES,** Marekani

RAPA wa Marekani, 50 Cent, ametangaza kuwa anatengeneza msururu wa vipindi vya televisheni kuhusu maisha ya mfungwa tapeli sugu Mnigeria na mshawishi wa mtandao wa Instagram, Hushpuppi.

Tangazo hilo la 50 Cent limezua mjadala mtandaoni huku baadhi wakiunga mkono wazo hilo, huku wengine wakisema utawafanya Wanigeria waonekana vibaya.

Akituma ujumbe huo kwenye ukurasa wa Instagram, 50 Cent ambaye jina lake halisi ni Curtis Jackson, alisema kuwa ilimbidi afanye hivyo: "Ni lazima nifanye hili, msururu wa Hushpuppi unakuja karibuni".

Msanii huyo wa muziki wa rap ana historia ya kuandaa vipindi vya televisheni ikiwa ni pamoja na msururu wa maigizo ya Power, ambao kwa mara ya kwanza ulianza kutangazwa mwaka 2014.

Hushpuppi, ambaye jina lake halisi ni Ramon Abbas, kwa sasa anatumikia kifungo cha miaka 11 jela kwa utapeli.

Hushpuppi alikuwa maarufu kwenye mtandao wa Instagram ambao aliutumia kuonyesha utajiri wake mkubwa kwa wafuasi wake milioni 2.8 hadi alipokamatwa mjini Dubai mwaka 2020, na akaunti yake kufungwa.

Kwenye mtandao wa Twitter baadhi ya watu wanaonyesha furaha yao juu ya mpango wa 50 Cent.

# *Niffer, Patrick Kanumba wapenzi?*

**Na Mwandishi Wetu**

MREMBO na mfanyabiashara maarufu kwenye mitandao, Niffer, anadaiwa kuwa yupo kwenye penzi zito na Patrick Kanumba.

Licha ya Niffer mwenyewe kutotaka kuweka bayana hilo, lakini mahojiano aliyoyafanya na redio moja, yamedhihirisha kwamba huenda wawili hao ni wapenzi.

"Patrick Kanumba ana miaka 25, mimi nina miaka 23, alipost Instagram, Patrick ni rafiki yangu. Ni mtu ambaye ni mzuri anajua vitu vingi ananishauri vingi. Tulikutana 2020 KFC tukala piza basi," alisema Niffer huku akidai licha ya kujua umri wake na mambo mengine, wao ni marafiki tu.

Alipoulizwa Ochu huwa ananyoa saluni gani, Niffer alijisahau akataka kutaja anaponyoa kisha akajishtukia katikati na kufumba mdomo kuashiria amevujisha siri ya kambi.



# RAIS SAMIA AIPONGEZA SIMBA QUEENS KUMALIZA YA NNE CAF

**Na Somoe Ng'itu,** RABAT

WAKATI Rais wa Tanzania, Samia Hassan Suluhu, akiipongeza Simba Queens baada ya kumaliza nafasi ya nne kwenye michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika kwa Wanawake, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Charles Lukula, amesema sasa wanarudisha nguvu zao kwenye Ligi Kuu Tanzania Bara.

Rais Samia kupitia mtandao wake wa kijamii wa twitter jana , mbali na kuipongeza Simba Queens kwa nafasi iliyomaliza kwenye michuano hiyo, alisema anaamini watajipanga vizuri kwa ajili ya mashindano ya mwakani ili kufanya vizuri zaidi.

Katika michuano hiyo iliyomalizika nchini Morocco jana, Simba Queens ilifungwa bao 1-0 juzi na Bayelsa Queens FC kutoka Nigeria na kumaliza katika nafasi ya nne ikiwa inashiriki kwa mara ya kwanza fainali hizo zinazofanyika kwa mara ya pili barani Afrika.

Lukula alisema kikosi chake kimejifunza mambo mbalimbali muhimu kupitia michuano hiyo na mazuri atayachukua kwa ajili ya kujiimarisha ili kufanya vema katika Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo anaamini msimu ujao utakaonza Desemba 5, mwaka huu utakuwa mgumu na wenye ushindani.

"Kumaliza katika nafasi ya nne katika michuano ya Afrika si jambo dogo, najua tutakutana na ushindani mkubwa kwenye ligi ya nyumbani kwa sababu kila timu inahitaji kuifunga Simba Queens ili kutengeneza habari kubwa na furaha kwao," alisema kocha huyo raia wa Uganda.

Lukula aliwapongeza pia wachezaji wake kwa kupambana katika michuano hiyo na anaamini kama angekuwa na wachezaji wazoefu zaidi, angefanya makubwa zaidi ya walichokifanya mwaka huu.

"Tutaifanyia sana kazi nafasi ya mshambuliaji, tumeshindwa kutumia nafasi nyingi tulizotengeneza, nadi nyumbani katika mazoezi kurekebisha idara hiyo, hata Mamelodi Sundowns Ladies ambao wametufunga, wao tayari ni wazoefu, walifanya vizuri mwaka jana na msimu huu wakaja imara, ninawashukuru wote, wachezaji, mashabiki wa Simba, msimu huu haukuwa wetu," Lukula aliongeza.

Alisema pia benchi lake la ufundi limejifunza mambo mengi mazuri na kuongeza hakuna mechi ambayo kwake ilikuwa rahisi hata zile ambazo timu yake iliibuka na ushindi. Nahodha Msaidizi wa Simba Queens, Fatma Issa 'Fetty Densa', alisema matokeo waliyopata ni mabaya na hayakuwafurisha wachezaji wote.

Densa alisema nia ya kila timu ilikuwa ni kucheza fainali na kwa sababu hiyo, Simba Queens haikuwa na bahati ya kufika hatua hiyo na kuishia nusu fainali.

"Mashindano haya yalikuwa magumu sana, kila mmoja alipambana kuhakikisha tunafika fainali, lakini haikuwa bahati yetu, sasa akili na nguvu zote tunazielekeza katika Ligi Kuu ya Tanzania," alisema beki huyo.

Golikipa chaguo la kwanza la Simba Queens, Gelwa Yona, alisema amejifunza mambo mbalimbali kupitia michuano hii na anaamini wakirudi Tanzania watayafanyia kazi ili wapate tiketi ya kushiriki tena fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunataka tena ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania ili twende tena CECAFA na turudi tena katika fainali za Ligi ya Mabingwa Afrika mwakani, tunarudi nyumbani kujipanga upya, " Gelwa, kipa wa zamani wa Kigoma Sister's ya mkoani Kigoma alisema.

Kikosi cha Simba Queens, ambao ndio mabingwa wa CECAFA na mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara kinatarajia kuanza safari ya kurejea nyumbani Dar es Salaam leo mchana kupitia Instabul, Uturuki na nyumbani kitatua keshokutwa, Jumatano alfajiri.

FAINALI...




Waziri wa Utamaduni, Sanaa na Michezo, Mohamed Mchengerwa (katikati), akirusha mpira juu kuashiria kuanza kwa mchezo wa fainali wa mpira wa Kikapu kati ya Dar es Salaam na Unguja (Wanawake) wa mashindano ya CRDB Bank Taifa Cup yaliyofanyika mwishoni mwa wiki katika viwanja vya Bandari jijini Tanga. Aliyevaa kofia huku akipiga makofi ni Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya CRDB, Abdulmajid Nsekela. **MPIGAPICHA WETU**

# Kocha aitesa Polisi Tanzania

**Na Saada Akida**

UONGOZI wa Klabu ya Polisi Tanzania, umesema upo katika mchakato wa kutafuta kocha mkuu ambaye atakuja kukinoa kikosi cha timu hiyo kwenye mikikimikiki ya Ligi Kuu Tanzania Bara msimu wa 2022/23 unaoendelea.

Polisi Tanzania hivi karibuni ilimfuta kazi kocha wake raia wa Burundi, Joslin Sharif, kutokana na mwenendo mbaya wa timu hiyo katika michezo waliyocheza ya ligi hiyo.

Akizungumza na gazeti hili jana, Makamu Mwenyekiti wa Polisi Tanzania, Robert Munisi alisema mchakato wa kuimarisha benchi la ufundi unaenda vizuri na watakahikisha wanapata watu sahihi wa kukinoa kikosi cha timu yao.

Alisema msimu huu timu yao haijafanya vizuri kwani imepata ushindi mechi moja, sare tatu na amepoteza saba katika michezo 11 waliocheza hadi sasa, jambo ambalo linalowaumiza na kuwatafakarisha.

"Tumepata ufumbuzi, kwanza tumeanza na mchakato wa kuboresha uwanja wetu wa Ushirika mjini Moshi ambao umeruhusiwa sasa kuendelea kutumia, lakini kusaka makocha kwa ajili ya kukinoa kikosi chetu.

"Tunakumbuka hivi karibuni tuliwaondoa makocha wetu kwa sababu ya mwenendo mbaya wa matokeo tunayoyapata, hadi sasa bado hatujatangaza kocha mkuu na hilo linafanyiwa kazi haraka kumpata na msaidizi wake iwe ndani au nje ya nchini," alisema Munisi.

## Minziro azitaka pointi tatu za Prisons

**Na Hadija Mngwai**

BAADA ya kupata pointi moja dhidi ya KMC, Kocha wa Geita Gold FC, Fred Felix Minziro, amesema anaelekeza nguvu zote katika mchezo unaofuata dhidi ya Tanzania Prisons ili kupata pointi zote tatu.

Geita Gold inatarajia kuvaana na Tanzania Prisons keshokutwa, Jumatano katika Uwanja wa Kumbukumbu ya Sokoine jijini Mbeya, ikiwa ni mwendelezo wa Ligi Kuu Bara.

Akizungumza na Nipashe jana, Minziro alisema wanajipanga kuhakikisha wanafanikiwa kuibuka na pointi zote tatu dhidi ya Tanzania Prisons.

"Matokeo ya mpira ndivyo yalivyo, tumepata pointi moja dhidi ya KMC, tunaelekeza nguvu zetu katika mchezo wetu dhidi ya Tanzania Prisons.

"Nashukuru wachezaji wangu wapo vizuri isipokuwa mchezaji mmoja George Mpole ndio majeruhi, hatokuwapo katika mchezo dhidi ya Prisons, wachezaji wengine waliobaki wapo vizuri.

"Ligi ni ngumu, kila timu inajipanga kufanya vizuri, hivyo tunahitaji kujipanga kuhakikisha tunafanya vizuri kila mchezo ulio mbele yetu," alisema Minziro.

Timu hizo zitavaana zote zikiwa na pointi 14, lakini Tanzania Prisons yenyewe ikishika nafasi ya tisa na Geita Gold ya 10, kutokana na tofauti ya nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

## Zimamoto yapania pointi 3 za Mafunzo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

BAADA ya kupoteza michezo miwili mfululizo ya mzunguko wa 11 na 12 ya Ligi Kuu Zanzibar timu ya Zimamoto, imesema sasa inajipanga kuhakikisha mechi tatu zilizobaki inapata ushindi.

Akizungumzia na gazeti hili jana, Kocha Mkuu wa timu hiyo, Mohmed Ali Hilali, alisema wanataka kuhakikisha michezo mitatu iliyobaki wanashinda licha ya kutambua itakuwa vigumu.

Alisema anajua mchezo wao wa 13 dhidi ya Mafunzo Novemba 21, mwaka huu utakuwa mgumu kwa kuwa wapinzani wao wamepoteza katika mchezo wa 12.

"Tumepoteza mchezo dhidi ya Polisi, lakini tumefungwa ugenini Kisiwani Pemba, hivyo sikikatai makosa kwenye kikosi changu bali najua ni kawaida katika mchezo wa mpira kushinda na kupoteza, kikubwa nawajaza hamasa wachezaji wangu ili kuhakikisha tunashinda mchezo wa mbele yetu," alisema.

# HABARI MICHEZO

## ZISIKUPITE

**MOUNT BADO CHELSEA**
KIUNGO wa Kati wa England, Mason Mount, bado hajakubali kusaini mkataba mpya na Chelsea baada ya mazungumzo ya kuongeza mkataba wake na Blues unaotarajiwa kuingia miezi 18 iliyosalia kufikia tamati. (***Suday Telegraph***)

**SON ATAKIWA PSG**
KLABU ya Paris St-Germain inaweza kumnunua mshambuliaji wa Tottenham Hotspur, Son Heung-min, huku Real Madrid wakiwa na mashaka ya kumsajili mchezaji huyo wa kimataifa wa Korea Kusini mwenye umri wa miaka 30. (***El Nacional***)

**FIRMINO KUFUNGWA LIVERPOOL**
KOCHA wa Liverpool, Jurgen Klopp, amesema mazungumzo yanafanyika na mshambuliaji Roberto Firmino kuhusu kuongeza mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 31, huku mkataba wa sasa wa mchezaji huyo wa kimataifa wa Brazil ukikamilika msimu wa majira ya joto. ***(Liverpool Echo)***

**GAKPO AJIWEKA SOKONI**
WINGA wa Uholanzi, Cody Gakpo, ambaye alihusishwa na kuondoka PSV Eindhoven msimu wa joto, amesema atakuwa "tayari kuchukua hatua hiyo" mwishoni mwa msimu na kwamba itakuwa "heshima" kuichezea timu yoyote kati ya "Real Madrid, Barcelona, Manchester United, Manchester City na Liverpool". ***(NOS, via Goal***)

**DE GEA KUKATWA MSHAHARA**
GOLIKIPA wa Manchester United, David de Gea, mwenye umri wa miaka 32, atalazimika kukatwa mshahara wa pauni 100,000 kwa wiki ikiwa anataka kuongeza muda wake wa kukaa na klabu hiyo. ***(Daily Star Sunday***)

**SANCHEZ AWINDWA UNITED**
GOLIKIPA wa Brighton na Hispania, Robert Sanchez, mwenye umri wa miaka 24, anafuatiliwa na Chelsea na Manchester United. (***Mirror***)

**ENDRICK AITAKA CHELSEA**
KLABU ya Palmeiras imekataa ofa kutoka kwa Paris St-Germain kwa ajili ya mshambuliaji wa Brazil, Endrick. Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 16 anapendelea kwenda Chelsea, huku klabu hiyo ya Stamford Bridge ikiwa tayari katimiza kipengele cha kuwezesha kuruhusiwa kwake cha euro milioni 60. (***ESPN Brazil***)

**TUCHEL KUMRITHI SIMEONE**
KOCHA wa zamani wa Chelsea, Thomas Tuchel, ndiye anayepewa nafasi kubwa kuchukua nafasi ya Kocha wa Atletico Madrid, Diego Simeone, iwapo klabu hiyo ya Hispania itaamua kuachana na Muargentina huyo. (***Fichajes***)

**TEN HAG NA VAN DE BEEK**

KOCHA wa Manchester United, Erik ten Hag amesema kiungo wa kati wa Uholanzi, Donny van de Beek mwenye umri wa miaka 25, "athibitishe au aende". (***Sunday Mirror***)

**CHUKWUEZE ATAKIWA VILLA**
KLABU ya Aston Villa inalenga kumnunua winga wa Nigeria, Samuel Chukwueze mwenye umri wa miaka 23, ambaye anaichezea klabu ya zamani ya Kocha Unai Emery, Villarreal. (***Football Insider)***

**MILAN YAMTAKA VAZQUEZ**
KLABU ya Inter Milan inataka kumsajili beki wa kushoto wa Hispania, Jesus Vazquez mwenye umri wa miaka 19, kutoka Valencia na mshambuliaji wa Borussia Monchengladbach na Ufaransa, Marcus Thuram mwenye umri wa miaka 25. (***Gazzetta Dello Sport, via Football Italia***)

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA



# NEYMAR: KOMBE LA DUNIA QATAR LA MWISHO KWANGU

### ●●● Siwezi kuhakikisha kwamba nitacheza tena michuano hii, nitacheza kama ni ya mwisho kwangu...

**PARIS,** Ufaransa

NEYMAR hana uhakika kama atapata fursa ya kuiwakilisha Brazil kwenye Kombe lingine la Dunia baada ya mashindano hayo ya mwaka huu nchini Qatar.

"Ninazungumza na baba yangu, huwa tunazungumza. Nitacheza kila mchezo kana kwamba ni wa mwisho kwa sababu hujui kitakachotokea kesho.

> **"Siwezi kuhakikisha kwamba nitacheza Kombe la Dunia lingine. Kwa kweli sijui. Nitacheza kama ni fainali.**

Fowadi huyo wa Paris Saint-Germain atashiriki Kombe lake la tatu la Dunia, ambapo atakuwa akitafuta kuiongoza Brazil kwa ushindi wao wa kwanza kwenye michuano hiyo kwa miaka 20.

Neymar atakuwa na umri wa miaka 34, wakati Kombe la Dunia la 2026 likianza, na hivyo ana uhakika mdogo kama atashiriki katika michuano hiyo, hivyo anatumaini kuimarisha nafasi katika historia ya soka kwa kuiongoza Brazil kutwaa taji hilo nchini Qatar.

"Nitacheza kama ni ya mwisho," alisema Neymar akiiambia Globo.

"Ninazungumza na baba yangu, huwa tunazungumza. Nitacheza kila mchezo kana kwamba ni wa mwisho kwa sababu hujui kitakachotokea kesho.

"Siwezi kuhakikisha kwamba nitacheza Kombe la Dunia lingine. Kwa kweli sijui. Nitacheza kama ni fainali.

"Labda nitacheza tena. Labda sivyo. Inategemea. Kutakuwa na mabadiliko ya ukufunzi wakati Tite atakapoondoka baada ya Kombe la Dunia na sijui kama kocha huyo atanipenda.

"Tayari nimejenga historia ndefu katika timu ya taifa na kwa hakika, nataka kuimaliza vema.

"Nina furaha, napenda kucheza mpira na napenda kushinda, napenda kuwa bora kuliko nilivyo kila siku, napenda kusaidia wachezaji wenzangu, jambo la msingi, natumaini jina langu limechorwa katika soka."

Alipoulizwa kuhusu nafasi ya Brazil ya kubeba kombe Qatar, Neymar aliongeza: "Nataka kucheza kombe hili, kujitolea kwa hilo, kwa sababu nina uhakika tuna uwezo wa kufika mbali sana.

"Ingawa watu wengi hawatuamini, tutathibitisha vinginevyo. Naona timu hii ya taifa ina mambo mengi mazuri, na naona tunaweza kufika mbali sana."

Wakati huo huo, mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 30, amefunga mara 75 katika mechi 121 alizoichezea Brazil.

SportPesa
LIVE IN PLA

MECHI KALI
TONDELA
VERSUS
MOREIRENSE
1 | 2.71
X | 3.15
2 | 2.51

PIGA *150*87#
Karibu SportPesa
1. Bet Sasa
2. Michezo zaidi
3. JACKPOT
4. Weka Pesa
5. Akaunti yangu
6. Toa Pesa
7. Matokeo ya Bet/Mechi
00. Toka

SportPesa
SPORTPESA.CO.TZ
HUDUMA KWA WATEJA MASAA 24, TUPIGIE:
18+ 0764115588, 0677115588
0685115588 GBT:0249
@TZSportPesa @SportPesaTZ @tzsportpesa

# ARTETA AIMWAGIA SIFA ARSENAL



**LONDON,** England

MIKEL Arteta alisifu 'ukomavu' wa wachezaji wake wa Arsenal walipoibuka na ushindi wa mabao 2-0 dhidi ya Wolverhampton Wanderers na kuendeleza uongozi wao kileleni mwa Ligi Kuu England.

Huku Manchester City ikipata kichapo cha kushtukiza nyumbani kutoka kwa Brentford katika mechi ya kwanza ya mchana, jukumu lilikuwa kwa Arsenal kupata matokeo chanya dhidi ya Wolves.

Mabao mawili ya kipindi cha pili kutoka kwa nahodha Martin Odegaard yalitosha kunyakua ushindi kwa upande wa Arteta na kuendeleza uongozi wao kileleni mwa jedwali hadi pointi tano kuelekea mapumziko ya Kombe la Dunia.

Akionyesha sababu chanya baada ya mchezo huo, Arteta aliambia BBC: "Shukrani kwa mashabiki kwa sapoti na jinsi walivyosaidia kubadilisha klabu hii na nguvu ya kila mtu na wanapaswa kufurahia kuwa juu ya ligi.

"Tulionyesha ukomavu wa aina nyingine leo kucheza mchezo wao, katika dakika 20-30 za kwanza tulijitahidi kuwavunja. Tulikuwa bora zaidi kipindi cha pili na tulikuwa na ujasiri zaidi na kuchukuwa hatari lakini pia bila kuwaruhusu."

Alipoulizwa kuhusu mawazo na moyo ndani ya kambi ya Arsenal, Arteta alijibu: "Bila watu hawa tusingekuwa katika nafasi tuliyonayo. Wanaongezeka siku baada ya siku."



## *Klopp afunguka usajili*

**LIVERPOOL,** England

KOCHA Jurgen Klopp amedokeza kuwa Liverpool itajaribu kuleta sura mpya wakati wa usajili wa Januari, lakini amesisitiza kuwa klabu hiyo itatafuta mchezaji sahihi.

'Wekundu' hao wamekumbwa na majeraha nyakati fulani msimu huu, huku mastaa kama Ibrahima Konate, Joel Matip na Diogo Jota wakiwa miongoni mwa wale ambao wamekosa muda mrefu wa msimu huu.

Klabu hiyo ilimsajili kiungo Arthur Melo kwa mkopo kutoka Juventus ili kuimarisha safu yao ya kiungo, lakini wakampoteza Mbrazil huyo kutokana na jeraha la muda mrefu wiki chache tu tangu atue Anfield.

Akizungumza baada ya ushindi wa Liverpool dhidi ya Southampton juzi, Klopp alikiri kwamba Liverpool ingependa kuleta wachezaji wapya waliosajiliwa katika dirisha lijalo la usajili - lakini ikiwa tu hali inaruhusu.

"Siku zote tuko wazi kwa mambo kama haya, lakini si lazima tufungue mjadala huo," alisema Klopp.

"Haisaidii sasa kwa sababu siku zote ni sawa, huwa tunazungumza sawa, huwa ni sawa - ikiwa kuna jambo linalowezekana kwetu, tutalifanya.

HABARI MICHEZO

Y
CHEZA USHINDE KASINO

# ZANZIBAR YAPITIA VIGEZO USAJILI MCHEZO WA NGUMI

**Na Saada Akida**

KAMISHNA wa Idara ya Michezo Zanzibar, Ameir Mohamed Makame, amesema baada ya serikali kuruhusu mchezo wa ngumi visiwani humo, mchakato unaoendelea kwa sasa ni kupitia miongozo waliyopewa na Baraza la Michezo la Taifa (BMT) kabla ya kuusajili mchezo huo.

**Akizungumza na gazeti hili jana, Ameir alisema serikali kupitia wizara husika wanaendelea na mipango hiyo kwa kupitia miongozo ya BMT husuan Katiba ya Kamisheni na Shikikisho la Ngumi za Ridhaa.**

Alisema baada ya kupata mafuzo na jinsi ya kupata uzoefu kwa kubadilishana mawazo na wenzao wa Bara sasa wako katika mchakato huo kabla ya kuusajili mchezo huo.

"Tuvute subra tunaweka mambo ya usajili sawa tukimaliza hili, tunaanza mafunzo na usajili wa mashirikisho na vyama vyote vitaenda kwa wakati mmoja tukimaliza hapo ngumi zitachapwa," alisema Ameir.

Alisema hivi karibuni walienda Tanzania Bara kuangalia changamoto wanazokumbana nazo BMT kuhusu mchezo huo na kujua jinsi ya kukabiliana nazo watakapokamilisha mchakato wote wa usajili.

"Tulikutana na kuzungumza na vyama vya waamuzi, mashirikisho, promota na kamisheni za ngumi za ridhaa zinazosimamiwa na kujifunza zaidi kutoka kwao hukusu huu mchezo ukizingatia Zanzibar haukuwapo kwa miaka mingi," alisema Kamishna huyo wa Idara ya Michezo Zanzibar.

Ni takriban miezi miwili sasa tangu Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imetangaza rasmi kuruhusu mchezo wa ngumi kuanze kufanyika visiwani humo baada ya kupigwa marufuku Januari 12, 1964 na Rais wa Kwanza, Abeid Amaan Karume. Waziri wa Habari, Utamaduni, Sanaa na Michezo Zanzibar, Tabia Maulid Mwita, alitangaza uamuzi huo katika kikao cha Baraza la Wawakilishi baada ya kupata maoni ya wananchi mbalimbali waliohojiwa na kupata baraka za Baraza la Mapinduzi.



Mkuu wa Wilaya ya Iringa, Mohamed Moyo (katikati aliyevaa pensi), akiongoza mbio za Kilomita 10, zilizofanyika barabara za mji wa Iringa juzi, ikiwa ni mwendelezo wa maonyesho ya 'Utalii na Uwekezaji Kusini Fahari Yetu mwaka 2022' yanayofanyika kwa siku tano mkoani Iringa. **PICHA: STEVEN WILLIAM**

# Kocha wa viungo aja Simba

INATOKA UKURASA 32

mara, Mgunda alisema ikifika muda ataeleza juu ya hilo ila kwa sasa anaangalia zaidi maboresho ya kikosi chake kuelekea mechi zijazo.

Akizungumzia mchezo wa juzi, licha ya kuibuka na ushindi, Mgunda alisema ameona mapungufu katika kikosi chake kwani pamoja na kutengeneza nafasi nyingi, walishindwa kuzitumia.

Alisema ameona mapungufu hayo, anarudi uwanja wa mazoezi kwa ajili ya kufanyia kazi hasa safu yake ya ushambuliaji kwa kujenga utulivu wanapokuwa katika eneo la kufunga.

"Ni kweli tunatengeneza nafasi lakini tunatumia chache, nimeliona hilo naenda kufanyia kazi upungufu wote kuumaliza au kupunguza, lakini pia hata yale mazuri kuyaboresha.

"Licha ya upungufu huo niwapongeze wachezaji wangu kwa kupambana kupata pointi tatu leo (juzi) dhidi ya Ihefu FC kwa sababu mechi haikuwa rahisi kikubwa tumepata pointi tatu," alisema Mgunda.

Alisema ligi imekuwa ngumu kwani kila timu imejipanga vizuri hasa timu ambazo zinashika nafasi ya chini katika msimamo na ndivyo ilivyokuwa kwa Ihefu FC hali iliyomlazimu kubadili mbinu katika kipindi cha pili.

"Tuliingia na mbinu tofauti kipindi cha pili hii ni kulingana na mpinzani wangu, Ihefu FC walikuwa na nguvu na madhaifu yao, hivyo tukayatumia kupata matokeo," alisema Mgunda.

# Yanga kileleni

INATOKA UKURASA 32

ndani ya eneo la hatari la Yanga kutoka kwenye winga ya kushoto, lakini Meshack Abraham alishindwa kuunganisha licha ya kunyoosha mguu wake ili auguse mpira.

Dakika moja kabla ya mapumziko, Kagera Sugar ilifanya shambulizi la hatari kwenye lango la Yanga, lakini mastraika wake Mbaraka Yusuph, Kagawa walishindwa kuuweka mpira wavuni, huku shuti la Meshack liligonga mwamba wa juu.

Pamoja na timu zote kufanya mabadiliko ya kipindi cha pili, lakini matokeo yalibaki kama yalivyo na kuifanya Kagera Sugar kubaki na pointi zake 11, ikiwa nafasi ya 13 kwa mechi 11 ilizocheza mpaka sasa na Yanga kupepea kileleni.

SCAN HAPA KUPAKUA APP YETU!
SPORTPESA APP
PAKUA APP YETU, BET LEO UWE MILIONEA

MECHI ZA USHINDI
"1" - NI TIMU YA NYUMBANI KUSHINDA
"X" - NI TIMU KUTOKA SARE
"2" - NI TIMU YA UGENINI KUSHINDA.

JUMATATU - 14/11/2022

| MUDA | GAMEID | MICHEZO | NYUMBANI 1 | SARE X | UGENINI 2 |
|---|---|---|---|---|---|
| 14:00 | 2746 | FC Metalist Kharkiv vs FC Kryvbas Kriviy Rih | 2.58 | 3.16 | 2.53 |
| 14:00 | 3649 | Sudeva Delhi FC vs Kenkre FC | 1.60 | 3.45 | 5.45 |
| 15:00 | 2369 | Teuta Durres vs KF Erzeni | 3.65 | 3.02 | 2.02 |
| 15:00 | 5391 | Chernomorets Odessa vs FK Lviv | 2.00 | 3.20 | 3.49 |
| 15:00 | 5762 | Korabi Diber vs Skenderbeu | 1.81 | 3.31 | 4.08 |
| 16:00 | 3292 | Almopos Arideas vs Panserraikos | 8.53 | 4.46 | 1.32 |
| 16:00 | 4917 | Rukh Vinnyky vs FC Minaj | 1.93 | 3.21 | 3.70 |
| 16:15 | 5794 | Proodeftiki FC vs Kallithea FC | 4.09 | 3.12 | 1.87 |
| 16:30 | 4844 | Minerva FC vs Sreenidi Deccan FC | 1.85 | 3.60 | 3.55 |
| 17:00 | 2115 | Olympiacos Youth vs AEK Athens U19 | 1.70 | 3.65 | 4.19 |
| 17:00 | 3664 | Hellas Verona Youth vs Frosinone Youth | 2.57 | 3.54 | 2.34 |
| 17:00 | 5962 | Birmingham U21 vs Cardiff City U21 | 1.92 | 3.75 | 3.21 |
| 17:25 | 3672 | Al Qadisiyah vs AL Qaisoma | 2.10 | 3.05 | 3.75 |
| 17:30 | 1883 | Um Alhassam vs Al Shabbab | 6.83 | 4.88 | 1.34 |
| 17:30 | 5103 | Al-Tadamun Buri vs East Riffa | 11.63 | 6.79 | 1.15 |
| 17:30 | 5213 | Hajer Club vs AL Khlood | 2.57 | 2.72 | 2.91 |
| 17:30 | 5219 | Qalali vs Al Hala Muharraq | 7.20 | 4.87 | 1.32 |
| 17:30 | 5573 | Sitra Club vs Muharraq SC | 4.67 | 3.60 | 1.64 |
| 17:50 | 5882 | AL Arabi (SA) vs Alshoulla | 3.15 | 2.81 | 2.34 |
| 18:00 | 2635 | Partizani Tirana vs Bylis Ballsh | 1.51 | 4.10 | 6.20 |
| 19:00 | 3198 | Asteras Tripolis vs Ionikos Nikea FC | 1.75 | 3.37 | 4.86 |
| 19:00 | 4775 | Universitatea Cluj vs Argesul Pitesti | 2.03 | 2.98 | 3.97 |
| 19:40 | 2671 | Najran SC vs Al Orubah | 2.57 | 2.86 | 2.77 |
| 20:00 | 1265 | FK Trajal vs FK Zeleznicar Pancevo | 3.11 | 2.96 | 2.27 |
| 20:00 | 1284 | El Fahem vs Hapoel Rishon Lezion | 2.71 | 2.86 | 2.86 |
| 20:00 | 2597 | Hapoel Kfar Saba vs Nazareth Ilit | 2.59 | 2.74 | 3.14 |
| 20:00 | 4145 | Hapoel Petah Tikva vs Hapoel Acre | 1.99 | 3.20 | 3.91 |
| 20:00 | 5224 | Sakaryaspor vs Caykur Rizespor | 2.82 | 3.21 | 2.30 |
| 20:00 | 5519 | Goeztepe vs Keciorengucu | 2.33 | 3.16 | 2.82 |
| 20:30 | 2318 | OFI Crete vs Levadiakos | 1.88 | 3.18 | 4.38 |
| 21:00 | 1948 | 1860 Munich vs RW Essen | 1.91 | 3.57 | 3.62 |
| 21:00 | 2013 | Tondela vs Moreirense | 2.71 | 3.15 | 2.51 |
| 21:00 | 3322 | Sonderjyske vs Vejle BK | 2.53 | 3.41 | 2.43 |
| 21:00 | 4783 | Mafra vs Leixoes | 2.16 | 3.35 | 3.10 |
| 21:15 | 2855 | Beitar Jerusalem vs Bnei Sakhnin | 2.63 | 3.27 | 2.42 |
| 22:00 | 1356 | Zulte Waregem U21 vs Kortrijk U21 | 2.10 | 3.83 | 2.76 |
| 22:00 | 2143 | Jong Utrecht vs Maastricht | 2.38 | 3.65 | 2.56 |
| 22:00 | 2319 | KAA Gent U21 vs Oostende U21 | 2.78 | 3.56 | 2.18 |
| 22:00 | 2386 | Westerlo U21 vs Lierse SK U21 | 2.01 | 3.85 | 2.92 |
| 22:00 | 3325 | AS Eupen U21 vs Standard Liege U21 | 2.44 | 3.80 | 2.34 |
| 22:00 | 3713 | Maghreb Tetouan vs FAR Rabat | 3.69 | 2.82 | 2.11 |
| 22:00 | 4127 | Jong Ajax vs Den Bosch | 1.71 | 4.14 | 3.84 |
| 22:00 | 4264 | Botosani vs Hermanstadt | 2.73 | 2.83 | 2.78 |
| 22:00 | 5644 | Mechelen U21 vs Lommel U21 | 1.66 | 4.47 | 3.64 |
| 22:30 | 2257 | Estrella Grana EL Palmar CF vs Racing Murcia | 3.55 | 3.00 | 2.20 |
| 22:30 | 4322 | Virtus Entella vs Cesena | 2.27 | 3.05 | 3.30 |
| 22:45 | 3746 | Chelmsford vs Barnet | 2.36 | 3.41 | 2.72 |
| 22:45 | 5824 | Crusaders Belfast vs Ballymena Utd | 1.25 | 5.64 | 7.97 |
| 23:00 | 1204 | Nancy vs Sedan | 1.83 | 3.59 | 3.84 |
| 23:15 | 1888 | Santa Clara vs GD Estoril | 2.29 | 3.13 | 3.13 |

CHEZA KWA WAJIBU | KIWANGO CHA MAKATO YA SIMU KUZINGATIWA.

Michezo
Jumatatu Novemba 14, 2022
Nipashe



‘Kombe la Dunia Qatar la mwisho kwangu’ UKURASA 29

HESABU...



Mfungaji wa bao pekee la Yanga wakati ikiibuka na ushindi wa 1-0, Clement Mzize, akipiga hesabu za kumtoka beki wa Kagera Sugar, Datius Peter, kwenye mechi ya Ligi Kuu Bara iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza jana. **MPIGAPICHA WETU**

# Kocha wa viungo atua kuisuka Simba

**Na Saada Akida**

WAKATI Kaimu Kocha Mkuu wa Simba, Juma Mgunda, akilia na kuzaliwa kwa majeruhi wapya katika kila mechi, uongozi wa klabu hiyo upo hatua za mwisho kupata dawa ya tatizo hilo baada ya mazungumzo na kocha wa viungo kuelekea kukamilika, imefahamika.

Simba imekuwa ikiandamwa na majeruhi katika kikosi chake kila inaposhuka dimbani, na wiki iliyopita tu dhidi ya Singida Big Stars, ilizalisha majeruhi mpya, Peter Banda aliyeumia kifundo cha mguu ‘enka’, hivyo sasa kulazimika kukaa nje ya uwanja kwa wiki nne, huku katika mechi dhidi ya Ihefu FC Uwanja wa Benjamin Mkapa juzi, Pape Sakho, naye akishindwa kumaliza dakika 90 kutokana na kuumia.

Kutokana na mabalaa hayo, uongozi wa Simba wanaamini shida kukosekana kwa kocha wa viungo, hivyo ipo hatua za mwisho za mazungumzo na Kocha wa idara hiyo, Mkenya Michael Igendia ili kuwa sehemu ya benchi la ufundi la timu hiyo.

Igendia ambaye amewahi kuwa mwalimu wa viungo wa Timu ya Taifa ya Kenya, Harambee Stars, tayari yuko nchini kwa ajili kwa kukamilisha mazungumzo ya kuwapasha misuli wachezaji wa Simba.

Nipashe limemshuhudia kocha huyo aliyetua nchini juzi na kwenda uwanjani kuiangalia Simba ikiibuka na ushindi wa bao 1-0 dhidi ya Ihefu FC katika Uwanja wa Benjamin Mkapa.

Kwa upande wa Mgunda alisema: “Tumekuwa na majeruhi kila mechi, wengine wanapona na kurejea ila bahati mbaya hivi karibuni tumepata majeruhi mengi kwa kijana wangu, Peter Banda, ameumia enka na atakuwa nje ya uwanja kwa wiki nne na Okwa [Nelson] bado akiendelea na matibabu”.

Alisema Okwa, anasumbuliwa na majeraha ya nyonga hali inayomlazimu kutokuwapo katika kikosi kinachocheza kwa siku za hivi karibuni.

Kuhusu kukosekana kwa kocha wa viungo kuwa moja ya sababu ya wachezaji kupata majeraha ya mara kwa

INAENDELEA UK. 31

# YANGA YARUDI KILELENI

## ●●● Kinda Clement Mzize airudisha kupigwa na ‘baridi’ baada ya kuitungua Kagera Sugar...

**Na Adam Fungamwango**

KINDA kutoka kikosi cha vijana cha Yanga, Clement Mzize, jana alifunga bao lake la kwanza akiipa ushindi wa 1-0, akianza kwa mara ya kwanza kwenye mechi ya Ligi Kuu dhidi ya Kagera Sugar, iliyopigwa Uwanja wa CCM Kirumba jijini Mwanza, hivyo kuirudisha kupigwa na ‘baridi’ la kileleni mwa msimamo wa ligi hiyo.

**Bao hilo lilifungwa dakika ya 18 kwa kichwa kutokana na uzembe wa kipa Said Kipao kuchelewa kudaka mpira wa krosi iliyokuwa haina madhara kutoka kwa Feisal Salum.**

Baada ya kuipiga, kipa huyo alionekana kutofanya juhudi zozote za kutokea na kuudaka, badala yake aliusubiri umfikie mikononi, ndipo straika huyo alipouwahi na kuupiga kichwa ukajaa wavuni.

Ushindi huo wa bao 1-0 ni kama iliopata Jumatano iliyopita nchini Tunisia ilipoichapa Club Africain kwenye mechi ya marudiano kuwania kufuzu hatua ya makundi ya Kombe la Shirikisho barani Afrika na kufanikiwa kusonga mbele.

Ni ushindi uliowarudisha mabingwa hao watetezi juu ya msimamo wa ligi, ikiwa imetimiza pointi 23 sawa na Azam, lakini ina tofauti nzuri ya mabao ya kufunga na kufungwa.

Pia Yanga inatimiza mechi 46 bila kupoteza, tangu ilipopoteza mara ya mwisho msimu uliopita, Aprili 26, mwaka jana, ilipofungwa bao 1-0 dhidi ya Azam FC.

Kagera Sugar itabidi ijilaumu yenyewe kwa kushindwa kupata angalau sare, kwani pamoja na kuumiliki kwa kiasi kikubwa mchezo huo, lakini ilikosa mkwaju wa penalti dakika ya 68 baada ya Erick Mwijage kumpeleka Djigui Diarra upande ule ule wa kushoto ambao kipa huyo alikuwa amekwenda.

Tuta hilo lilitokana na Diarra mwenyewe kumuangusha straika aliyeingia kipindi cha pili, Hamisi Kiiza ndani ya eneo la hatari.

Mbali na hilo, Kagera Sugar ilikosa mabao ya wazi kipindi cha pili, hasa dakika 20 za mwisho ambazo walikuwa wameikamata mechi.

Mechi hiyo iliyochezwa kwenye uwanja uliokuwa na vidimbwi kadhaa vya maji, kutokana na mvua iliyonyesha jijini humo, ilishuhudiwa dakika 13 za mwanzo zikichezwa bila shambulizi lolote la maana hadi dakika ya 14, Kagera Sugar ilipofanya shambulizi la kwanza kwa krosi iliyopigwa na Datius Peter, lakini Kibwana Shomari aliutoa na kuwa kona.

Ni kona iliyozua kizaazaa, kwani Ally Nassor ‘Ufudu’ aliipiga na kuunganishwa na Ally Ramadhani ‘Kagawa’, lakini kipa Diarra alikaa imara na kuudaka.

Dakika ya 20, nusura Mzize apachike tena bao la pili, alipowafungasha tena mabeki wa Kagera Sugar kwenye winga ya kushoto, akawahadaa na kuingia ndani kabla ya kuachia shuti kali, lakini safari hii Kipao alifanya kazi ya ziada akiruka na kuupangua.

Fiston Mayele aliikosesha Yanga bao dakika ya 30, alipomegewa pande safi na kubaki peke yake na kipa, lakini shuti lake liliokolewa na Kipao kwa mguu wa kulia.

Ufudu kwa mara nyingine alipiga krosi

INAENDELEA UK. 31

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >